

**ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI
ZANZIBAR**

MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais
2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani.
3.Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais
4.Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu
5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa
6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
8.Mhe. Hamad Masoud Hamad	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ole.
9.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge
10.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa
11.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa.
12.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Gando.
13.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Kuteuliwa.
14.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Jang'ombe
15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
16.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Kazi, Uwezesaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la Makunduchi
18.Mhe. Mansoor Yussuf Himidi	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Kiembesamaki
19. Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni
20.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
21.Mhe. Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu
22.Mhe. Issa Haji Ussi	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka

23.Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais
25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
26.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni
28.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
29.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
30.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
31.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini
32.Mhe. Ali Mzee Ali	Kateuliwa na Rais
33. Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
34.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake
35. Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
36.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
37.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
38.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
40.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
42.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
43.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
44.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
45.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
46.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
47.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
48.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Jimbo la Kikwajuni
49.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
50.Mhe. Marina Joel Thomas	Kateuliwa na Rais

51.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa	Jimbo la Mkwajuni
52.Mhe. Mgeni Hassan Juma	Nafasi za Wanawake
53.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma	Jimbo la Bumbwini
54.Mhe. Mohammed Haji Khalid	Jimbo la Mtambile
55.Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali	Jimbo la Uzini
56.Mhe. Mohammed Mbwana Hamad	Jimbo la Chambani
57.Mhe. Mohammed Said Mohammed	Jimbo la Mpendae
58.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	Nafasi za Wanawake
59.Mhe. Mussa Ali Hassan	Jimbo la Koani
60.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	Nafasi za Wanawake
61.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake
62.Mhe. Nassor Salim Ali	Jimbo la Rahaleo
63.Mhe. Omar Ali Shehe	Jimbo la Chake-Chake
64.Mhe. Panya Ali Abdalla	Nafasi za Wanawake
65.Mhe. Rashid Seif Suleiman	Jimbo la Ziwani
66.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake
67.Mhe. Rufai Said Rufai	Jimbo la Tumbe
68.Mhe. Saleh Nassor Juma	Jimbo la Wawi
69.Mhe. Salim Abdalla Hamad	Jimbo la Mtambwe
70.Mhe. Salma Mohammed Ali	Nafasi za Wanawake
71.Mhe. Salma Mussa Bilali	Nafasi za Wanawake
72.Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni
73.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	Nafasi za Wanawake
74.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	Jimbo la Mwanakwerekwe
75.Mhe. Shawana Bukheti Hassan	Jimbo la Dole
76.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni
77.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde
78.Mhe. Ussi Jecha Simai	Jimbo la Chaani

79.Mhe. Viwe Khamis Abdalla

Nafasi za Wanawake

80.Mhe. Wanu Hafidh Ameir

Nafasi za Wanawake

Ndugu Yahya Khamis Hamad

Katibu wa Baraza la Wawakilishi

Kikao cha Kumi na Nane – Tarehe 10 Julai, 2012

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika (Pandu Ameir Kificho) alisoma dua

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 178

Kuondolewa kwa Uzio

Mhe. Asha Abdu Haji – Aliuliza:-

Katika miaka ya nyuma serikali iliweka uzio pembezoni mwa bahari kutoka Malindi kuelekea Forodhani, pamoja na kuifanya mandhari kuwa ni ya kupendeza lakini pia ilikuwa ni moja ya sababu za kupunguza ajali katika eneo lile, ukingo ule ulikuwa ni kinga muhimu ya kutumbukia baharini kwa watoto wadogo, lakini pia kwa ajali ndogo ndogo zinazoweza kutokea pale.

- (a) Je, ni sababu zipi zilizopelekea uzio ule kuondolewa (kuvunjwa).
- (b) Serikali haioni kuwa kuondosha uzio ule kumepunguza haiba na kuwa chanzo cha ajali katika eneo hilo.
- (c) Kwa nini serikali haiurejeshi uzio ule ili kuweka mandhari nzuri ya eneo lile.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 178 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:

Mhe. Spika, ni kweli kwamba katika miaka ya nyuma serikali iliweka uzio pembezoni mwa bahari kutoka Malindi kuelekea Forodhani na kuifanya mandhari kuwa ya kupendeza pale na pia kuweka usalama kwa wapita njia.

- (a) Uzio uliokuwepo hapo awali Mhe. Spika, pembezoni mwa ukingo wa pwani ya Malindi kuelekea Forodhani uliwekwa na serikali katika miaka ya 1970. Uzio huo uliharibika kwa kumung'unyuka kidogo kidogo hadi kutoweka kabisa kutokana na sababu mbali mbali ikiwemo uchakavu, lakini hata pia kuvunjwa bila ya sababu na vijana wapita njia, na wale wanaotaka kuogelea baharini nyakati za jioni.
- (b) Nakubaliana na Mhe. Mwakilishi kwamba kutokuwepo kwa uzio huo kumeondosha haiba ya mandhari ya eneo hilo na kuwepo kwa uwezekano mkubwa wa ajali na hata kwa wale wanaotembea kwa miguu.
- (c) Mhe. Spika, kupitia mradi wa huduma za mjini (*ZUSP*), serikali itaifanyia ukarabati eneo lile kwa kutanua kidogo eneo kwa upana wa mita tano ndani ya bahari ili kuongeza sehemu ya wanaopita kwa miguu. Hivi sasa serikali inaendelea na kazi ya kutayarishwa hadidu rejea za mjenzi atakayepatiwa kazi ya ujenzi wa eneo hilo. Kukamilika kwa ujenzi huo ni dhahiri kwamba kutarejesha tena haiba na mandhari nzuri ya eneo hilo, na mji wetu kwa ujumla zaidi ya ilivyokuwa hapo mwanzoni.

Nam. I74

Ulipaji wa Madeni ya Shirika la Umeme

Mhe. Salma Mussa Bilal – Aliuliza:-

Uhai wa Shirika la Umeme unatokana na ulipaji mzuri wa madeni kwa wateja wake zikiwemo wizara na taasisi mbali mbali za serikali. Cha kusikitisha ni kwamba takriban taasisi nyingi za serikali hazitowi kipaumbele katika ulipaji wa madeni sugu ya muda mrefu na kusababisha usumbufu mkubwa wa kiutendaji.

- (a) Mhe. Waziri utakubaliana nami kwamba kutolipwa kwa madeni ya Shirika ni kuzorotesha maendeleo ya shirika.
- (b) Je, Mhe. Waziri huoni sasa iko haja ya ama kuzilazimisha taasisi hizo kulipa deni hilo kwa kuwakata katika bajeti zao za kila mwaka, au wizara yako kubeba mzigo na kusaidia kulipa gharama hizo moja kwa moja katika shirika.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa heshima kubwa naomba kujibu swali la Mhe. Mwakilishi lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

- (a) Mhe. Spika, nakubaliana na Mhe. Mwakilishi kwamba kutolipwa kwa madeni ya Shirika la Umeme kunazorotesha sana maendeleo ya Shirika.
- (b) Mhe. Spika, jukumu kubwa la Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo ni kuhakikisha kuwa wizara na taasisi za serikali zinapatiwa fedha kwa ajili ya kutekeleza mipango yao ya mwaka, ikiwa ni pamoja na kulipa huduma mbali mbali wanazopatiwa taasisi za serikali.

Ushauri wangu kwa Shirika la Umeme ni kuzifungia mita za TUKUZA taasisi zote za serikali isipokuwa taasisi nyeti kama vile Hospitali. Hata hivyo, nitajitahidi kufuatilia madeni ya shirika, ili wizara na taasisi za serikali zilipe madeni yao ya umeme kwa ukamilifu na kwa wakati.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Ahsante Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kumuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Wizara ya Fedha imekuwa na *trend* ya kutekeleza yale mambo ambayo taasisi za kawaida hazitekelezi, Wizara ya Fedha huwa inabeba kuyatekeleza. Je, Mhe. Waziri haoni kuna haja sasa ya hizi bajeti za umeme zikabakia pale ofisi ya fedha na ikawa Wizara ya Fedha ndio inalipa.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Spika, analolitaka Mhe. Mwakilishi ni kuondoa majukumu ya wizara na taasisi za serikali kupeleka Wizara ya Fedha. Mimi nataka kusema tu kwamba, huo hautakuwa utaratibu mzuri, utaratibu mzuri ni kwamba kila taasisi na kila wizara iweze kulipa huduma wanazopatiwa kutoka taasisi nyengine. Hivi sasa nina jukumu la kulipa madeni ya umeme yanayotumiwa katika vituo vya maji na sio deni dogo. Kwa hivyo, mimi ninachoomba ni kwamba tusimamie na Mhe. Spika, wewe

utakuwa shahidi katika vifungu tulivyovipitisha tayari kuna malipo ya umeme, na kama malipo ya umeme yako ndani ya bajeti na kama taasisi hailipi basi tuendelee kuibana, ili taasisi hii iweze kuheshimu kulipia huduma wanazozitumia.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza. Kwa kuwa uhai wa Shirika la Umeme unategemea ulipaji mzuri kwa wateja wake, lakini pia uhai wa wateja unategemea huduma nzuri na bei nzuri iliyokuwa na utaratibu unaokubalika kwa wateja wake, na kwa kuwa leo Mhe. Spika, katika kipindi cha Mawio wananchi wanaokata umeme katika kituo cha Malindi wamekuwa wakilalamika juu ya utaratibu mbovu wa ulipaji wa umeme, ambapo mteja analipa shilingi elfu kumi lakini *unit* wanazozipata zinakuwa ni tofauti, na kwa kuwa serikali huwa inafanya kazi kwa utaratibu wa *collective responsibility*. Je, Mhe. Waziri ni sababu ipi inayopelekea wateja kulipa shilingi elfu kumi kwa pamoja, lakini wote wakapata *unit* zilizokuwa tofauti.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Spika, kwa kuwa swali alilolileta Mhe. Mwakilishi kwangu mimi ni jipya, namuomba basi nilifanyie utafiti ili niweze kuelewa. Kwangu mimi ninavyoamini ni kwamba kama mteja amelipa shilingi elfu kumi ni dhahiri kwamba tupate *unit* sawasawa na mteja mwengine ambaye amelipa shilingi elfu kumi, kama kuna hiyo tofauti basi ningeliomba vile vile niweze kupata muda kuisoma nini kilichojiri kuwepo na tofauti hiyo.

Lakini vile vile Mhe. Spika, nitaiomba sana wizara hii itoe elimu kwa wananchi wetu pale ambapo umeme unapouzwa *unit* moja kiasi gani ili kila mmoja aelewe, atakapokwenda basi kununua umeme ajue kwa kiwango hiki cha pesa ni kiasi gani cha umeme naweza kupata.

Mhe. Spika: Hivi wizara inayohusika inasemaje, Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati inasemaje juu ya jambo hili. Waheshimiwa Wajumbe ni vizuri tunapojibu maswali na shughuli zote tuwe makini kusikiliza. Kwa sababu mambo haya kama alivyozungumzia kuna *same set of collective responsibility*, jambo limeulizwa hapa lakini kumbe linahusu Wizara ya Ardhi. Sasa ndio nauliza Wizara ya Ardhi inasemaje huko.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, hilo swali mimi sikulipata vizuri kwa sababu kuna swali katika *order paper* Nam. 83, ambalo nimeshalijibu wiki iliyopita, sasa nilikuwa najadiliana na muulizaji hapa kwa hivyo sikulipata vizuri hili swali.

Mhe. Spika: Mhe. Mwakilishi rudia swali.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Mhe. Spika, kwa kuwa uhai wa Shirika la Umeme unategemea ulipaji mzuri kwa wateja wake, lakini pia uhai wa wateja unategemea huduma nzuri na bei nzuri iliyokuwa na utaratibu unaokubalika kwa wateja husika. Na kwa kuwa katika kipindi cha Mawio leo wananchi wengi wamelalamika wanaolipa malipo ya TUKUZA katika kituo cha Malindi, wamekuwa wanalipa bei ya shilingi elfu kumi lakini wanapata *unit* tofauti kwa kila mmoja, na kwa kuwa serikali huwa inafanya kazi kwa utaratibu ule wa *collective responsibility*, yaani kwa pamoja. Je, Mhe. Waziri ni sababu zipi zinazopelekea wateja wote walipe shilingi elfu kumi lakini wapate *unit* zilizokuwa tofauti wote.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, ni kweli jana Mhe. Salmin Awadh aliniletea swali hapa ambalo ndio hilo analoliulizia sasa hivi, na nikamuahidi kwamba leo nitalifanyia kazi na kumpa jibu rasmi juu ya suala hili. Ni kweli kwamba alitoa shilingi 30,000 akapata *unit* 157, lakini siku ya pili akatoa tena shilingi 30,000 akapata *unit* 112 ambapo ni tofauti ya *unit* 45. Hili suala nakusudia kulifanyia kazi kwenye Shirika na nitashindwa kujibu hapa nitamjibu kwa maandishi.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, nakushukuru sana kwa busara zako naomba nimuulize Mhe. Waziri swali moja la nyongeza lenye kifungu a na b. Mhe. Spika, moja kati ya tatizo ambalo linaikumba Shirika la Umeme ni madeni ambayo taasisi za serikali hawalipi licha ya Baraza lako tukufu kutenga fedha kila mwaka, na kwa kuwa Mhe. Waziri amesema kwamba kukusanya fedha hizi ni kuinyima uhuru wa taasisi husika.

- (a) Mhe. Waziri hebu atusaidie kama mdhamini wa fedha, na kama ni mtaalamu wa fedha, tufanye nini ili kuanzia bajeti hii fedha zote ambazo zimetengwa kwenye malipo ya umeme zifike Shirika la Umeme bila ya tatizo.

- (b) Kwa kuwa ushahidi umeonesha kwamba mteja mwenye kununua umeme wa shilingi elfu kumi anapata unit tofauti, na kwa kuwa muda mrefu Wazanzibari wamekuwa wakilalamika kwamba hata umeme ambao tunanunua kutoka Bara umekuwa na mazingaombwe. Mhe. Waziri haoni kwamba leo ule ushahidi umekamilika kwamba Shirika la Umeme linashindwa kazi.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Spika, naomba arudie swali la kwanza alikuwa anasema mbio mbio, aseme taratibu nimsikie.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, swali la kwanza ni kwamba Baraza la Wawakilishi limekuwa likitenga fedha kila mwaka kwa ajili ya malipo ya umeme kila idara, lakini kila mwaka madeni ya umeme yanaongezeka kwa maana kwamba taasisi za serikali hazilipi umeme. Kwa nini hutushauri vizuri ili fedha hizo ambazo zimetengwa zote zikafika Shirika la Umeme badala ya kuwaachia taasisi husika kuzipeleka. Maana yake taasisi zinaonesha kwamba hazipeleki fedha hizo Mhe. Waziri, kwa hivyo hebu kama mtaalamu na mdhamini wa fedha tufanye nini ili fedha hizi zifike kwenye Shirika la Umeme.

Swali la pili ni kwamba bei ya umeme hivi sasa shilingi elfu kumi unapata unit tofauti, na tangu zamani watu wamekuwa wakilalamika kuwa hata umeme wanaonunua Tanzania Bara umekuwa na tatizo hilo hilo, kwamba Tanzania Bara tunanunua umeme na wananchi wa Zanzibar wanafidia malipo hayo, huoni kwamba ushahidi umekamilika kuwa Shirika la Umeme limeshindwa kazi.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Spika, swali lake la kwanza tufanye nini. Ushauri wangu na nitaendelea kuutoa hapa ni ule ule, Shirika la Umeme wazifungie TUKUZA taasisi zote za serikali. Narudia tena, shirika la Umeme wazifungie TUKUZA taasisi zote za serikali waache taasisi nyeti kama Hospitali. Kufanya hivyo tu ndio Shirika litakuwa halipati hasara na madeni yake yatalipwa kwa wakati. Lakini mimi sioni kizito kwa Shirika kuwa hawawafungii umeme taasisi za serikali na bajeti tunapitisha hapa, vifungu tumepitisha. Jana Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii amesema hapa kuna vifungu tele anavyo mle vya kulipia madeni na umeme anaotumia hivi sasa sioni sababu za msingi kwa nini tunachelewa kuwafungia.

Mimi nawaambia Shirika watafute hizo mita waanze kuzifunga, na kama kuna taasisi yoyote ya serikali itakataa kufungwa umeme Makamo wa Rais tunae hapa atawaita, hilo ni agizo la serikali sio agizo la Omar Yussuf ni agizo la serikali. Hilo la kwanza.

Lakini la pili Mhe. Spika, Mhe. Waziri mwenye dhamana ya umeme ameeleza kwamba atatoa majibu kwa maandishi, na nadhani unapomjibu Mwakilishi mmoja ile inakuwa *circulated* kwa wawakilishi wote ataeleza hili, kama kuna tofauti ya *unit* kwa pesa ambazo zinatolewa na wateja sawa na ikiwa Shirika limeshindwa kutekeleza majukumu yake ataeleza.

Kwa hivyo, mimi nadhani kwamba waziri mwenye dhamana ya nishati tusubiri jibu halafu kwenye *conclusion* atatwambia, je, kufanya hivyo ni kwamba shirika limeshindwa au wanafanya hivyo kwa maana gani, tuelewe, wananchi wanapotoa shilingi elfu kumi ni kweli wanataka kuona umeme unafanana. Lakini leo huyu katoa shilingi elfu kumi analipwa *unit* mbili yule shilingi elfu kumi analipwa *unit* 100 kuna nini, hata na mimi najiuliza kuna nini. Basi Mhe. Waziri madhali ameahidi atatuletea hilo jibu tusubiri jibu la Mhe. Waziri.

Nam. 54

Mgao wa Hisa *BoT*

Mhe. Ismail Jussa Ladhu – Aliuliza:-

Wakati Bodi ya Sarafu ya Afrika Mashariki inavunjwa na kuanzishwa kwa Benki Kuu za kila nchi iliyokuwa mwanachama wa Bodi hiyo, Zanzibar ilipatiwa fungu lake la mgao ambalo lilijumuishwa na lile la Tanganyika kuwa kama mtaji wa kuanzisha Benki Kuu ya Tanzania mwaka 1966. Fungu hilo la Zanzibar lilikuwa ni sawa na asilimia 11.02 ya jumla ya hisa iliyoanzisha Benki Kuu ya Tanzania (*BoT*).

- (a) Zanzibar imepata mgao wa kiasi gani wa faida kutokana na mchango huo wa hisa kwenye mtaji wa *BoT* kuanzia 1966 hadi 2011.

- (b) Fedha hizo za mgao wa faida zimeingia katika mfuko upi kwa manufaa ya Zanzibar.
- (c) Kwa nini muundo wa *BoT* katika uongozi wa juu na uongozi wa matawi yake hauwakilishi sura ya Muungano kama ilivyokuwa msingi wake.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa heshima kubwa naomba kujibu swali la Mhe. Mwakilishi lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:

- (a) Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeanza kupokea mgao wa faida kutoka Benki Kuu ya Tanzania kuanzia mwaka 1994/95. Hata hivyo, mwaka 2000/2001, mwaka 2007/2008 na mwaka 2009/2010 Benki Kuu haikutengeneza faida, kwa maana hiyo Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar nayo haikupata mgao wa faida katika miaka hiyo. Kwa ujumla mgao wa faida iliyopata kutoka *BoT* kuanzia mwaka 1994 – 95 hadi kufikia Juni, 2012 ni shilingi 14, 136,100,782/-.
- (b) Mhe. Spika, kisheria fedha zote zinatakiwa kuingia katika Mfuko Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kwa maana hiyo fedha za mgao wa faida kutoka *BoT* nazo zimeingia katika Mfuko Mkuu wa SMZ na matumizi yamefanywa na SMZ.
- (c) Mhe. Spika, nakubaliana na Mhe. Mwakilishi kwamba muundo wa *BoT* kwa kiwango kikubwa hauwakilishi sura ya Muungano, sio ule wa juu tu, hata kwa watendaji wa chini. Hali hii imetokana na zaidi na utaratibu mzima wa uteuzi na uajiri. Hata hivyo, utaratibu wa uajiri katika Taasisi za Muungano ni miongoni mwa masuala yanayojadiliwa baina ya wizara zetu mbili za utumishi na tayari wamefikia hatua nzuri.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Nakushukuru Mhe. Spika na namshukuru Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri, naomba kuuliza swali la nyongeza lenye kifungu a na b.

- (a) Mhe. Spika, katika majibu yake Mhe. Waziri kasema kwamba Zanzibar imeanza kupata mgao unaotokana na faida kuanzia mwaka 1994/95, lakini Benki Kuu ya Tanzania iliundwa mwaka 1966, na wakati huo tayari Zanzibar ikiwa imetoa hisa yake ambayo ni asilimia 11.02 ya mtaji wote ulioanzishiwa *BoT*. Mhe. Waziri kwa nini kuanzia mwaka 1966 hadi 1994/95 Zanzibar haikupata mgao wowote.
- (b) Kwa sababu Zanzibar imetoa asilimia 11.02 ya hisa katika mtaji ulioanzishiwa *BoT*, hizo fedha alizotwambia za shilingi 14 bilioni katika kipindi cha miaka kuanzia 1994 hadi 2012 inawakilisha kiasi gani asilimia ya hisa ambazo Zanzibar imetoa.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Spika, kwanza wataalamu wa *IMF* walikuja Zanzibar na Tanzania kwa ujumla kuangalia jinsi gani mgao wa faida wa *BoT* uende kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar mwaka 1993, baada ya kuja kwao ndio tathmini hiyo ikafanywa ikaonekana kwamba na Zanzibar kuna haja, na wao kupata mgao huo wa asilimia 4.5 kwenda Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuanzia mwaka 1994/95.

Kuna taarifa tu ambazo sijazifanyia uchambuzi wa kina bado kwamba baadae Zanzibar iliamua kufanya mahesabu kwa kutumia wataalamu mbali mbali, ili kudai madeni yake mbali mbali ya nyuma. Kwa maelezo ya taarifa ambazo nimeziona kuna baadhi ya fedha Zanzibar ilipewa na ilisaini na kupokea. Sasa sina uhakika ule mchanganuo kama ulihusisha vile vile na gawio la *BoT* kuanzia 1966, lakini bado kwa sababu ripoti ni kubwa sana na ni zamani bado najaribu kuifanyia uchunguzi nikibaini basi Mhe. Mwakilishi nitaweza kukwambia kwamba na lile deni lilikuwemo na hili la kuanzia mwaka 1966 kama halikuwemo vile vile naweza nikakupa hiyo taarifa.

Swali la pili Mhe. Spika, hivi sasa moja ya kero ya Muungano ambayo bado haijapata ufumbuzi, Mhe. Ismail Jussa anapiga makofi sijui kama ameshajua au makofi anatanguliza, ambayo ni usahihi wa hisa ya Zanzibar kwenye *East African Currency Board* linafanyiwa kazi bado, na wizara zetu mbili hizi za fedha zimepewa kazi hiyo ili

tukishakupata usahihi tutakuja kutoa taarifa kwamba asilimia yetu ilikuwa ni 11 au ilikuwa ngapi. Kwa maana hiyo, hili gawio ambalo tunalipata sasa hivi Mhe. Spika, ni gawio ambalo limetokana na ripoti ya *IMF* ya asilimia 4.5 na sio asilimia 11.

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa: Nakushukuru Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Baada ya maelekezo yote ambayo ametupatia Mhe. Waziri kwa nini *BoT* haitambui Zanzibar kama ni m-bia katika suala hili la *BoT*.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Spika, *BoT* ni Benki ya Muungano, kwa maana hiyo Zanzibar ni sehemu ya Muungano, kwa maana hiyo kama tunalipwa hisa maana yake tayari wameshaku-*recognize* kwamba na wewe ni m-bia wa hiyo benki.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, nashukuru kupata nafasi hii ya kuuliza swali la mwisho la nyongeza kwa swali hili. Mhe. Spika, Mhe. Waziri alipokuwa akijibu swali hili alisema kiko kipindi nafikiri mwaka 2002, na kuendelea Zanzibar haikupata pesa kutoka Benki Kuu kwa sababu Benki Kuu haikupata faida kwa wakati huo. Na kwa sababu Mhe. Waziri kakiri kuwa ule uongozi ulioko katika *BoT* haufanani kuwa ni wa Kimuungano. Sasa nauliza Mhe. Waziri alitumia vielelezo gani mpaka akaridhika kuwa *BoT* haikupata fedha wakati huo na wao wakakubali kutopata hisa yao.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Spika, kwanza lazima tufahamu kwamba *BoT* kwa maana *The Central Bank* haifanyi biashara. Hili tufahamu Waheshimiwa Wawakilishi tafauti na *Commercial Bank* nyengine. *Central Bank* haifanyi biashara, kinachopatikana kama ni faida ni ile *exchange rate*, ule mbadiliko tu wa pesa wao wanauza pesa za kigeni katika *Commercial Bank* na wananunua sasa ile *exchange rate* ndiyo inayotoa faida katika *Central Bank*.

Kwa maana hiyo kigezo kinachotumia hapa ni kwamba kama benki inatengeneza faida kutokana na hizo *exchange rate*, na inaonekana katika hesabu kwamba sasa tumepata faida kwa hivyo faida ile ndiyo inayogaiwa Zanzibar wanapata asilimia 4.5 na nyengine inakwenda katika Serikali ya Muungano. Nimetaja hapa miaka mitatu nimetaja *specific* kwamba hapa hakukuwa na biashara, hakukuwa na faida iliyopatikana kwa hivyo hakukuwa na gawio.

Nam. 138

Ubovu wa Barabara Kiuyu

Mhe. Viwe Khamis Abdalla - Aliuliza:-

Miongoni mwa ahadi za Mhe. Rais wa Zanzibar ni kuifanyia matengenezo barabara ambayo inayotoka Kiuyu Penjewani mpaka Mjini Kiuyu. Kwa kuwa barabara hiyo inawapa usumbufu mkubwa wananchi wa Mjini Kiuyu wakati wa mvua, na hupelekea kukosa huduma muhimu ikiwemo ya wanafunzi wanaosoma Skuli ya Minungwini kushindwa kwenda skuli.

Je, Mhe. Waziri Wizara yako ina mpango gani wa kuwaondoshea kero hizo wananchi wa Mjini Kiuyu.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake namba 138 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, barabara ya Mjini Kiuyu hadi Penjewani hufanyiwa matengenezo ya kawaida kila mwaka, katika bajeti ya mwaka huu 2011/2012 inayomalizika, jumla ya *kalvati* mbili zilizengwa na pia zimetengwa fedha zisizopungua shilingi 4,106,000 kwa ajili ya kufanya matengenezo kwenye sehemu korofi ili iweze kupitika kwa muda wote katika bajeti ijayo 2012/2013 tumeingiza katika mpango wa kuikarabati kila mwaka. Hivyo barabara hiyo nayo itaingizwa katika mpango huo ili kuimarisha huduma za usafiri pamoja na watumiaji wengine wanaotumia barabara hiyo.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante Mhe. Spika, na mimi kupata fursa ya kuuliza swali dogo tu la nyongeza.

Mhe. Spika, kwa kuwa Mhe. Naibu Waziri ametoa majibu ambayo kwa kweli yanaleta matumaini kwa kiasi fulani, kwa kuwa hii barabara ya Kiuyu - Penjewani ni muhimu sana na sio kuwa haipitiki siku za mvua, hata siku za jua inakuwa ni tatizo kwa afya za wananchi kutokana na vumbi lililozidi kwenye barabara ile. Jee, Mhe. Waziri ni lini hasa atatia kifusi cha uhakika kusudi kupunguza hili vumbi hasa kwa hizi siku ambazo si za mvua.

Pili, kwa kuwa barabara ile watu wake ni wazuri kwa uzalishaji wazuri wa matunda kama vile matikiti maji, ndizi, embe na kwa mujibu wa semina ambayo tuliyopewa juzi tu katika Zanzibar Ocean View kule kuhusiana na wenzetu wa afya kuwa wanataka tutumie lishe nzuri, na kwa kuwa wanashindwa kuleta mazao yao pale Penjewani na kuyaleta Chake-Chake katika soko kuu pamoja na kuyasafirisha wakati mwengine kuyaleta hapa Unguja vitu kama ndizi, jee haoni Mhe. Naibu Spika, kuendelea kupanga siku, leo keshokutwa tutaifanyia matengenezo, haoni kama anapunguza lishe ya Wazanzibari jambo ambalo linaweza lika-reduce ile *qualitative population*.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi maswali yake ya nyongeza kwa pamoja kama hivi ifuatavyo.

Mhe. Spika, dhamira ya wizara yetu ni kuona kwamba barabara hii nayo inaweza kufanyiwa ukarabati ili iweze kupitika kwa mwaka mzima kipindi cha mvua na kipindi cha jua. Mipango yetu ni kuona mwakani bajeti yetu hii itaweza kutuchukua kwa sehemu kubwa katika kutimiza hayo malengo na azma yetu.

Naomba Mhe. Mwakilishi ajenge imani na sisi tutaifanya kazi kwa kutambua kwamba uimarikaji wa barabara kutatanua wigo, hisia, lakini pia na hisia kwa watumiaji wengi wakiwemo wananchi kwa kuweza kuimarisha lishe zao kwa kupata matunda na virutubisho vyengine muhimu, pamoja na kuongoza utanuzi wa soko kwa mazao yao.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri namuuliza Mhe. Naibu Waziri kwa kuwa barabara hiyo hivi sasa ina fusi, lakini fusi lake linaanza kuchimbuka. Ni lini wizara yake itasimamia ili kuirekebisha zaidi ili iweze kupitika.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, kwa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama hivi ifuatavyo.

Mhe. Spika, tumeeleza katika majibu mama kwamba kikawaida kila mwaka tunafanya marekebisho ya kuingiza kifusi. Lakini mpango wetu mwakani kwenye bajeti ya 2012/13 jambo hili litapewa kipaumbele na tutahakikisha kifusi hiki mwakani katika bajeti inayoanza mwezi wa sita na nane, basi tukipata fedha jambo hili litafanyika.

Mhe. Kazija Khamis Kona: Ahsante sana Mhe. Spika, naomba swali fungu (a) hili asinijibu kwa sababu ameshanitolea maelezo sana lakini naomba fungu (b) anijibu swali langu.

Nam. 83

Tatizo la Maji Safi na Ujenzi wa Kisima cha Kiashange

Mhe. Kazija Khamis Kona - Aliuliza:-

Kwa kuwa eneo la Kiashange linasemekana kuwa ni lenye maji mengi sana.

- (a) Ni sababu zipi zilizopelekea wananchi wa eneo hilo hasa wa kijiji cha Matemwe kukosa maji kwa muda mrefu sasa.
- (b) Kwa kuwa hivi sasa kuna kisima kipya ambacho kimeanza kuchimbwa katika maeneo hayo, ni lini hasa kisima hicho kitamalizika na kuanza kufanya kazi rasmi ili kuwaondolea usumbufu wananchi hao.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati, Naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 83 lenye vifungu (a) na (b) kama hivi ifuatavyo:-

- (b) Katika hatua za dharura za kulitafutia ufumbuzi tatizo hilo, Wizara yangu kupitia Mamlaka ya Maji imechukua hatua ya kuchimba kisima chengine kipya ambacho kipo katika hatua za mwisho, kukamilika kwa kisima hicho katika hatua za ufungaji wa pampu basi tunategemea wananchi wa eneo hilo watapatiwa ufumbuzi na kuondokana na tatizo hilo la maji.

Mhe. Kazija Khamis Kona: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa fursa ya kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali la nyongeza.

Kwa kuwa Jimbo la Matemwe lina Shehia 8 kama sijazisahau, na Shehia ya Kijini hata bomba la maji kule halijapeleka. Jee, Mhe. Naibu Waziri kisima hiki kipya kitasambaza mabomba kupeleka eneo la Shehia ya Kijini.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Ahsante sana Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama hivi ifuatavyo.

Wizara yangu kupitia Mamlaka ya Maji lengo ni kuhakikisha vijiji vyote vinasambaziwa huduma hiyo. Kwa hivyo tunategemea kila pale ambapo haijafika huduma hiyo basi tutaipoleka huduma hiyo na si kwa kisima hiki tu, nimuhakikishie kwamba Mhe. Mwakilishi kuna mradi ambao tumeusaini tarehe 31 mwezi wa tano, mradi wa AFBB ambao utanza shughuli zake rasmi katika kipindi hiki kifupi, na tunategemea kuendelea kwa mradi huo mpaka kumalizika kwake basi wananchi wote wa eneo hilo na Jimbo hilo na Matemwe na baadhi ya majimbo mengine watanufaika na huduma hiyo.

Mhe. Asha Bakari Makame: Ahsante sana Mhe. Spika, kwanza nichukue nafasi hii ya kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametuwezesha siku ya leo kuamka katika hali ya afya njema.

Nikushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii.

Mhe. Spika, kwa kuwa maendeleo kila sehemu yanahitaji maendeleo, na kwa kuwa wananchi ni miongoni mwa watu ambao wanakubaliana na hayo kutokana na serikali yao.

Nimuuliza Mhe. Naibu Waziri ni sababu zipi ambazo kwa kweli katika sehemu ya Mazizini kulikojengwa ofisi ya Mwanasheria Mkuu ambao wale wanaojenga ofisi wamechukua mawaya yote ya maji wameyasombasomba sasa imekuwa tatizo la maji limerudia pale pale.

Atalihakikishiaje Baraza lako tukufu kwamba akitoka hapa Mhe. Naibu Waziri anakwenda kuzungumza na Wachina wanaoleta maendeleo ya nyumba ya Waziri wa Katiba na Sheria.

Mhe. Spika: Swali lipo mbali na swali mama lakini kwa uzito na umuhimu hebu tusaidie suala hilo.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Ahsante sana Mhe. Spika, naomba Mhe. Mwakilishi kama hivi ifuatavyo.

Kama kawaida yangu ya ufuatiliaji basi ninamuhakikishia kwamba suala hilo tatalifuatilia na tatalipatia ufumbuzi.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa maji ni uhai wa mwanadamu, na kwa kuwa watu wa Matemwe ni muda mrefu hivi sasa wamekosa kupata maji, na kwa kuwa hivi sasa tumekabiliwa na mwezi mtukufu wa Ramadhani.

Jee, utawafanyia utaratibu gani wananchi hawa ili waondokane na matatizo kwa mwezi huu wa Ramadhani.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama hivi ifuatavyo.

Kwanza niseme wananchi wa Matemwe hawana ukosefu wa maji bali wana upungufu wa maji. Maji yanatoka ingawaje si asilimia mia moja lakini wanapata huduma hiyo kiasi.

Lakini ikumbukwe kwamba katika mwezi Mtukufu wa Ramadhani uliopita wizara yangu kupitia Mamlaka ya Maji ilikuwa tunasaidia vijiji ambavyo havina huduma hiyo kwa kuwapelekea magari ya maji. Wizara yangu haijachoka kuwasaidia wananchi juu ya hilo hususan katika mwezi Mtukufu wa Ramadhani.

Na. 107

Uharibifu wa Mazalia ya Samaki

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi - Aliuliza:-

Inasemekana wapo baadhi ya wavuvi huingia katika Shehia kuvua bila Sheha wa Shehia kuwa na taarifa, na huvua mpaka samaki wadogo wadogo ambapo suala hili limejitokeza kisiwani Pemba katika sehemu za Kengeja na baadhi ya vijiji vyengine ambapo husababisha viumbe vya bahari kutoweka.

- (a) Je, Mhe. Waziri hali hii unaelewa.
- (b) Kama unaelewa ni udhibiti gani ulioandaliwa dhidi ya wavuvi hawa ili kuondosha tatizo la uharibifu huu wa mazalia ya samaki na viumbe vya baharini.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi - Alijibu:-

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake namba 107 lenye vifungu (a) na (b) kwa pamoja kwa kumueleza kuwa suala hili linaeleweka.

Aidha, napenda kulijulisha Baraza lako tukufu kuwa taaluma ya uvuvi unaofaa inatolewa kwa wavuvi wa vijiji vyote Unguja na Pemba na kupitia kamati za uvuvi vijijini pamoja na ofisi za Wilaya kufanya doria na kuwakabidhi wale wote wanaofanya uvuvi wa uharibifu wa mazingira baharini, hususan kwenye mazalio ya samaki na viumbe vya baharini.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, baada ya majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kumuuliza kama hivi ifuatavyo.

Katika kipindi cha miezi sita nyuma Waziri aliyepita wa uvuvi alifanya ziara takriban Shehia zote kuonana na wavuvi hasa wafugaji samaki, na aliweka ahadi nyingi kwa maendeleo ya sekta ya uvuvi.

Jee, Mhe. Waziri kwa kuwa waziri alianza vizuri na kwa kuwa juhudi hizo zinahitajika kuendelezwa. Ni lini utafanya ziara katika Shehia zile ambazo mwenzako alipita ili kwenda kuona changamoto ambazo mwenzako ameziacha na maendeleo aliyofikia ili kuendelea sekta hii ya uvuvi visiwani mwetu.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Spika, ninashukuru naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama hivi ifuatavyo.

Ni kweli kwa kweli hatua ni kubwa iliyofikiwa na hasa baada ya wavuvi wenyewe kushajihika na kupata taaluma ya kutosha juu ya uvuvi ambao unakubalika. Lakini ni hivi karibuni tu nimefanya ziara Mkoa wa Kusini wa Pemba na tukawatembelea baadhi ya wavuvi, tukatembelea vile vile kamati ya PECA, yaani hifadhi ya Mkondo wa Pemba.

Kwa kweli wamenufaika sana na wameshajihika, lakini bado bahati mbaya sijamaliza Mkoa wa Kaskazini Pemba, na ninategemea baada ya bajeti tu kuanza ziara hiyo ili nao vile vile kujua changamoto zilizopo ili tuweze kushirikiana nao twende sambamba ili tufikie lengo.

Kwa hivyo Mhe. Mjumbe usiwe na wasi wasi na suala hilo.

Mhe. Ali Abdalla Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa fursa ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba nimuulize swali kama hivi ifuatavyo.

Katika diko la Kama Shehia ya Kama wananchi wengi walikuwa wanavua kwa kutumia uzio wa njukuti, lakini hivi sasa uzio huo umeambiwa ni marufuku na maofisa wameupiga moto na wananchi wanapata shida sana kujikimu kimaisha.

Jee, wizara itawasaidia nini wananchi hao wa jiko la Kama pamoja na Nyanjale Kiombamvua.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama hivi ifuatavyo.

Ni kweli kwamba uvuvi huo kidogo umekuwa na matatizo, na tumejaribu kuuzuia kwa sababu ile ile ya kuhifadhi mazingira yetu. Lakini pamoja na hiyo, kwanza tunawapa elimu na kuwashajihisha kutumia uvuvi mbadala na ndio lengo kubwa la uvuvi huu mbadala, maana yake ni kuwaondoa katika ule uvuvi ambao wameuzoea ili waanze uvuvi wa juu huku ambao kwa kweli una tija kubwa zaidi.

Kwanza ni uvuvi wa uhakika na una tija, na tumetembelea mwingi humo kwa kweli hivi sasa, wananchi kwa kweli wamefurahi na wanasema huu ni uvuvi wa uhakika kuliko kwenda baharini ambapo huna uhakika.

Ule unafuga siku unataka kwenda kuvua unavua tu, unajua tu unataka samaki wangapi kumi, thalathini na tumeona hayo, mwingi hivi sasa kama Pujini kule kwa kweli wameacha kazi Dar es Salaam kwenye maduka wanasema huu ndio uvuvi tunaouhitaji.

Kwa hivyo kwa kweli tumo katika hatua hizo za kuwashajihisha wavuvi wetu ili waje katika kujenga mabwawa ambao ni uvuvi wa uhakika. Wamesema hawana matatizo nao kubwa tuwape vifaa ambalo hilo ni moja tunasubiri baada ya bajeti, tupitische bajeti ili tuwasaidie wavuvi hawa wapate kama boti au kuwapa vifaa vya kuchimba mabwawa ya kufuga samaki, kaa pamoja na majongoo. Ahsante.

Mhe. Hassan Hamad Omar: Mhe. Spika, ahsante sana pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kumuuliza swali moja la nyongeza.

Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi imekusudia kuvua uvuvi wa bahari kuu. Jee kwa sababu Zanzibar ni kisiwa na kina wavuvi wengi, ni wavuvi wangapi watakaoweza kufaidika na uvuvi wa bahari kuu.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Spika, siwezi kukupa takwimu sahihi ni wavuvi wangapi lakini kwa kuanzia wapo wavuvi ambao tayari wameanza kuvua. Kwa sababu uvuvi wa bahari kuu haina maana kwamba lazima uwe na meli kubwa, hapana.

Ni chombo ambacho kinachoweza kufika pale si lazima iwe meli kubwa ni boti ya saizi tu, muhimu ni kuwa na taaluma na kuwa na vile vifaa.

Wapo watu ambao wameshakwenda na kwa kweli wamesema kuna tija kubwa sana, kwa sababu kule kuna samaki wengi sana ambao kwa kweli hatuna la kuwafanya. Tatizo kubwa ndio hatuna vifaa lakini hao wachache ambao wamepata hivyo vifaa, tayari wameshaleta taarifa kwamba kwa kweli kuna tija kubwa.

Bado juhudi zinaendelea kutafuta misaada mbali ya kuwashajihisha wawekezaji waje, lakini vile vile tunatafuta misaada ya kupata boti kwa ajili ya kuwapa wavuvi wetu waliomo katika vijiji.

Kwanza tutaanza na boti mbili ambazo kwanza zitakuwa ni kama darasa kuanza kuwapa taaluma kwa Unguja na Pemba, halafu baadae ndio tunawapa vifaa ili waende bahari kuu. Kwa hivyo Mhe. Mwakilishi wa Kojani hili suala na wewe unalielewa hilo kwamba lina tija, tuwe na subra, tupitische bajeti yetu ili tupate hizo boti kwa kuwapa watu wa Kojani nao waende bahari kuu.

HOJA ZA SERIKALI

Wizara ya Afya

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kwa kuanza kidogo kuwafahamisha Wajumbe kwamba kwenye kile kitabu tulichowapa kuna karatasi tumeongeza, inajieleza wenyewe ilikuwa haikutoka vizuri katika *printing*, kwa hivyo kwa yule atakayekuwa na macho mabovu kama mimi aitumie hii. Mhe. Spika, naomba sasa kutoa hoja kuwa Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya matumizi liweze kupokea, kujadili, kuchangia na baada ya hapo liidhinishe makadirio ya mapato na matumizi kwa kazi za kawaida, mishahara, posho na kazi za maendeleo kwa Wizara ya Afya kwa mwaka wa fedha 2012/2013.

Mhe. Spika, kabla ya yote naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu Muumba wa vilivyo angani, baharini na nchi kavu kwa kutujaalia afya njema iliyotuwezesha kukutana kwa mara ya pili katika kikao kama hichi cha Bajeti tokea kuundwa kwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa chini ya Uongozi wa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dr. Ali Moh'd Shein.

Mhe. Spika, vile vile sina budi kumshukuru Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Makamo wa kwanza na Makamo wa pili wa Rais kwa uongozi wao wa pamoja, wenye busara na hekima, uliowezesha nchi kuendelea kuwa na amani, utulivu na kuiwezesha Serikali ya Mapinduzi kutekeleza majukumu yake ya kuwaletea wananchi maendeleo vizuri na kwa mafanikio. Mafanikio hayo yameimarika zaidi kutokana na ufuatiliaji wa kazi za wizara za Serikali chini ya utaratibu aliouanzisha Rais wa kukutana na Wizara moja moja kila baada ya miezi mitatu.

Mhe. Spika, naomba kukushukuru wewe pamoja na wafanyakazi wa Baraza lako kwa msaada tunaendelea kuupata na kutuwezesha leo hii kufikisha hotuba hii mbele ya Baraza. Shukrani za pekee ziende kwa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii kwa busaza zao, na ushauri wenye hekima katika usimamiaji wa shughuli za Wizara ya Afya.

Mhe. Spika, baada ya shukrani hizo naomba sasa uniruhusu nianze kueleza utekelezaji wa kazi za wizara kwa mwaka 2011/12 na matayarisho ya wizara ya utekelezaji ya mwaka wa 2012/13. Hotuba hii naianza kwa kueleza shughuli za idara za kinga tiba na Hospitali ya Mnazi Mmoja kama ndio idara mama (*Core functions*) zinazobeba majukumu makubwa ya kazi zetu.

Mhe. Spika, kabla sijaeleza utekelezaji wa kila idara naomba kutoa muhtasari wa mapato na matumizi ya Wizara ya Afya kwa mwaka 2011/2012

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2011/2012, Wizara iliidhinishiwa jumla ya Tsh. 14, 368, 710,000.00 kwa ajili ya kazi za kawaida, kati ya hizo 12, 268, 710,000.00 kwa ajili ya mishahara na posho, na Tsh. 2, 100, 000,000.00 kwa matumizi mengineyo (OC). Hadi kufikia 31 Machi, 2012, jumla ya Tsh. 10, 083, 328,857.00 zilikwishaingizwa, kati ya hizo Tsh. 8, 797, 318,561.00 kwa ajili ya mishahara na posho sawa na asilimia 72 ya bajeti yake, na Tsh. 1, 286, 010,296.00 kwa matumizi mengineyo (OC), ambazo ni sawa na asilimia 61 ya bajeti yake.

Mhe. Spika, kwa upande wa fedha za Miradi ya Maendeleo, Wizara ilipangiwa jumla ya Tsh. 2, 500, 000,000.00, hadi kufikia 31 Machi 2012, jumla ya Tsh. 2, 026, 745,000.00 zilikwishaingizwa, ambazo ni sawa na asilimia 81 ya bajeti. Kwa ufafanuzi zaidi angalia kiambatisho A, B na C.

Utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Afya kwa mwaka 2011/2012 na Muelekeo wa 2012/2013

Mhe. Spika, Wizara yangu kwa kipindi cha 2011/2012 imepata mafanikio mazuri katika usimamizi na utoaji wa huduma za afya kwa wananchi. Mafanikio haya yamepatikana kupitia miradi, idara na vitengo mbali mbali vinavyounda na Wizara ya Afya.

IDARA YA KINGA NA ELIMU YA AFYA

Mhe. Spika, Idara ya Kinga na Elimu ya Afya ina majukumu ya kusimamia na kufuatilia umahiri wa utolewaji wa huduma za afya za msingi mijini na vijijini. Vile vile, Idara hii ina dhamana ya kubuni mbinu za kuinga na kukabiliana na maradhi mbali mbali yakiwemo maradhi ya miripuko, maradhi ya kuambukiza na yasiyoambukiza.

Pia idara ina jukumu la kusimamia utolewaji wa elimu ya afya kwa jamii, kwa lengo la kuzikinga na kuzistawisha siha za Wazanzibari dhidi ya maradhi.

Mhe. Spika, Idara hii husimamia na kutoa huduma kwa wananchi kwa kupitia miradi na vitengo vifuatavyo; ambavyo ni Programu ya Kudhibiti Malaria, Programu shirikishi ya Afya ya Uzazi na Mtoto, Programu Shirikishi ya UKIMWI, Kifua Kikuu na Ukoma, Kitengo cha Elimu ya Afya, Kitengo cha Lishe, Kitengo cha Afya Bandarini, Kitengo cha Huduma za macho, Kitengo cha Maradhi yasiyopewa kipaumbele, Kitengo cha Afya na usalama wa wafanyakazi, Kitengo cha Kufuatilia mwenendo wa maradhi pamoja na miripuko, Kitengo cha Afya ya Mazingira na Afisi za Timu za Afya Unguja na Pemba.

Programu ya kudhibiti maradhi ya Malaria

Mhe. Spika, Programu ya kudhibiti maradhi ya malaria ina majukumu ya kuhakikisha kuwa wananchi wanajikinga na maambukizi ya malaria na kwa wale waliopata maradhi haya wanapata tiba sahihi. Miongoni mwa mikakati inayotumika ni uhamasishaji wa matumizi sahihi ya vyandarua, tiba sahihi ya wagonjwa, kuimarisha utolewaji sahihi wa elimu ya afya kwa jamii kuhusu kinga dhidi ya ugonjwa huu, pamoja na ufuatiliaji wa wagonjwa katika ngazi ya Shehia.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2011/2012, katika kuhakikisha utolewaji wa tiba sahihi ya malaria kwa wagonjwa, programu imeweza kutoa mafunzo kwa watoa huduma (matabibu) 423 tu juu ya kufuata kiukamilifu miongozo ya kutibu wagonjwa wa malaria. Mafunzo hayo yaliwashirikisha watendaji kutoka sekta za serikali, sekta binafsi, vikosi vya ulinzi na vituo vya afya vya taasisi za kidini (*Faith based Organisations*). Vile vile, jamii ilihamasishwa na kuelimishwa juu ya utumiaji sahihi wa vyandarua kupitia viongozi wa ngazi mbali mbali wakiwemo wakuu wa wilaya, madiwani, masheha, mashekhe na wasanii maarufu akiwemu Bi. Kidude walishirikishwa katika Kampeni ya Maliza Malaria Zanzibar. Halikadhalika vyombo vya habari vilishirikishwa kikamilifu katika zoezi hili.

Mhe. Spika, jumla ya vyandarua 660,000 vilitolewa bure kwa wananchi wa Unguja na Pemba ili kupunguza maambukizi ya malaria. Wastani wa chandarua 1 hadi 3 viligaiwa kwa kila kaya. Zoezi hili limefanikiwa kwa wastani wa asilimia 85 ya lengo la kutoa vyandarua.

Mhe. Spika, hadi kufikia Machi 2012 jumla ya watu 64,393 walichunguzwa damu kwa njia ya darubini Unguja na Pemba, kati yao 562 (0.87%) waligunduliwa kuwa na vimelea vya malaria. Watoto chini ya umri wa miaka mitano waliochunguzwa walikuwa 30,708, kati ya hao 166 (0.54%) walibainika kuwa na vimelea vya malaria na kutibiwa. Halikadhalika, jumla ya watu 37,003 walifanyiwa uchunguzi kwa vituo visivyo na darubini kwa kutumia njia ya haraka ya kuchunguza Malaria (*Rapid Diagnostic Test - RDT*) katika vituo vya Unguja na Pemba, kati ya hao wagonjwa 254 (0.7%) waligundulika kuwa na vimelea vya malaria.

Mhe. Spika, katika kuimarisha ufuatiliaji wa mienendo na mifumo ya utokomezaji maradhi ya malaria nchini, programu iliimarisha mfumo wa kukusanya taarifa kwa kutumia simu za mkononi kutoka vituo 90 mpaka vituo 142 vya Serikali na vituo 3 vya binafsi. Aidha, programu imeanzisha mfumo wa ufuatiliaji wa wagonjwa majumbani ambao wamebainika kuwa na vimelea vya malaria katika sehemu wanazoishi.

Mhe. Spika, ufanisi wa kutokomeza malaria unaambatana na ufuatiliaji wa mwenendo wa mbu waenezao ugonjwa huo. Kazi hii iliendelea katika maeneo teuzi (*sentinel sites*) Unguja na Pemba, maeneo yenyewe ni Mwera, Chaani, Bumbwini, Malindi, Bopwe, Vitongoji, Uwandani, na Tumbe. Vile vile, wizara iliendeleza kazi ya kuua viluilui kwa kutumia gari maalum ijulikanayo kama “*Buggy*” ambayo ina uwezo mkubwa wa kupita sehemu zenye tope ambazo ni vigumu kuzifikia bila ya kutumia kifaa hicho.

Mhe. Spika, ni jambo la kufurahisha kuwaeleza Wajumbe la Baraza hili na Wananchi kwa jumla kwamba ugonjwa wa malaria Zanzibar unaendelea kudhibitiwa na kubaki chini ya asilimia moja ya wagonjwa.

Mhe. Spika, ili kufikia maamuzi yatakayosaidia kuendeleza mbele kampeni ya Maliza Malaria Zanzibar programu imekusudia kutekeleza kazi kuu zifuatazo kwa mwaka 2012/2013:-

- a) Kuendelea kuchunguza uimara wa dawa za safu ya kwanza ya kutibu malaria (dawa za mchanganyiko)

- b) Kuendelea na uchunguzi wa damu kwa vimelea vya malaria
- c) Ufuatiliaji wa mwenendo wa maradhi “*malaria surveillance*”
- d) Ufuatiliaji wa mwenendo wa mbu “*Entomological surveillance*”
- e) Kuimarisha mfumo wa kukusanya taarifa kwa kutumia simu za mkononi kutoka vituo 3 hadi kufikia 35 vya binafsi

Kitengo cha Elimu ya Afya (*Health Promotion Unit*)

Mhe. Spika, Kitengo cha Elimu ya Afya kina wajibu mkubwa wa kuelimisha, kuhamasisha na kutoa ushauri kwa jamii kuhusu afya na kinga ya maradhi kwa kutumia njia mbali mbali za kubadilisha tabia hatarishi, ili kuweza kufikia lengo la afya bora kwa kila mwananchi.

Mhe. Spika, katika kufanikisha utoaji wa elimu kitengo kilitembelea jumla ya skuli 50 za Maandalizi, Msingi na kati, na kutoa taaluma kwa wanafunzi na walimu juu ya maradhi mbali mbali yanayoathiri jamii ikiwemo kujikinga na maradhi ya Surua, maradhi ya kuharisha yakiwemo Kipindupindu, kuchunguzwa macho, masikio, koo na afya ya kinywa. Aidha kwa kushirikiana na Kitengo shirikishi cha Ukimwi, Kifua kikuu na Ukoma Elimu ya afya ilitolewa katika skuli za Nyerere, Mwembeladu na Shaurimoyo.

Mhe. Spika, katika kuelimisha jamii juu ya kujikinga na maradhi mbali mbali, jumla ya vipindi 53 vya redio na vipindi 16 vya Televisheni vilirushwa hewani kupitia vyombo vya serikali na watu binafsi. Halikadhalika, jumla ya wanavikundi vya mazoezi 74, (wanawake 39 na wanaume 35) walipimwa afya kuhusu lishe na kupewa ushauri kuhusiana na lishe bora.

Mhe. Spika, katika kufanikisha malengo yake kwa mwaka 2012/2013 kitengo kimepanga kutekeleza kazi kuu zifuatazo: -

- a) Kuandaa na kutangaza hewani vipindi 60 vya redio na vipindi 52 vya TV vyenye mada mbali mbali
- b) Kuandaa muongozo wa utekelezaji mpango wa afya maskulini pamoja na kutoa elimu ya afya na ushauri kwa wanafunzi, walimu, na vikundi vya mazoezi
- c) Kuendelea kutoa ushirikiano wa kitaalamu kwa miradi, vitengo na wadau wanaotoa taaluma ya Elimu ya Afya katika jamii
- d) Kuanzisha kituo cha redio, kitakachojulikana kwa jina la “*Afya FM radio*” kwa azma ya kuwaelimisha jamii hususan vijana katika kupambana na tabia hatarishi za utumiaji wa dawa za kulevya, mimba za utotoni, Ukimwi n.k. na vishawishi vyengine vinavyoathiri vijana kwa azma ya kupunguza shindikizo rika “*peer pressure*” hapa Zanzibar. Redio hii pia itashajiisha jamii juu ya utumiaji bora wa huduma za afya na kutoa tathmini juu ya huduma hizi

Kitengo cha Lishe

Mhe. Spika, Kitengo cha Lishe kina majukumu ya kupanga, kutekeleza, kusimamia, kutathmini na kufuatilia shughuli za lishe nchini. Kitengo kinatoa mafunzo na ufuatiliaji matibabu ya utapia mlo mkali kwa watoto, ukosefu wa madini joto pamoja na kupunguza tabia hatarishi za kula vyakula vinavyochangia kuongezeka kwa maradhi sugu (*Chronic diseases*).

Mhe. Spika, katika kupambana na utapia mlo kitengo kiliweza kukagua na kutoa ushauri wa kitaalamu kwa watendaji wa vituo 144, pia jumla ya wafanyakazi 150 walipatiwa mafunzo kuhusu matibabu ya watoto wenye utapia mlo na jinsi ya kuwapatia huduma sahihi watoto wenye utapia mlo mkali (*Severe Malnutrition*). Aidha mikutano baina ya wafanyakazi wa vituo vya afya na wa ngazi ya jamii (*Community Owned Resource Persons - CORPs*) juu ya utekelezaji na changamoto za matibabu ya utapia mlo imefanyika katika Shehia 331.

Mhe. Spika, jamii ya wazanzibari imekuwa ikisumbuliwa na ugonjwa wa tenzi shingo (*Goitre*), ugonjwa ambao unasababishwa na upungufu wa madini joto (*Iodine*). Wizara imechukua juhudi mbali mbali kukabiliana na hali hiyo; Mpango kazi wa miaka 3 (*plan of work*) juu ya utekelezaji wa kuimarisha utiaji na utumiaji chumvi yenye madini joto umetayarishwa. Vile vile watendaji 200 kutoka wilaya za Unguja na Pemba walihamasishwa juu ya kuwepo kwa kanuni ya kuzuia uzaji na usambazaji wa chumvi isiyo na madini joto, wakati huo huo vifaa vya

maabara na vitendea kazi vilinunuliwa. Halikadhalika pampu 200 za kuwekea madini joto kwenye chumvi zimenunuliwa na kusambazwa katika vikundi vya uzalishaji chumvi vya Unguja na Pemba.

Mhe. Spika, Aidha tungependa kuwaeleza wananchi kanuni inayolazimisha wafanyabiashara na wazalishaji wa chumvi kuweka madini joto imeshaanza kutumika, na hivyo mfanyabiashara au mzalishaji wa chumvi yeyote atakayeua au kusambaza chumbi iliyokua haina madini joto, atakua na hatia kwa mujibu wa kanuni hiyo.

Mhe. Spika, katika kufanikisha malengo yake kwa mwaka 2012/2013, kitengo kimepanga kutekeleza kazi kuu zifuatazo:-

- a) Kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa matibabu ya utapia mlo mkali (*Severe Acute Malnutrition*) na matatizo ya madini joto katika hospitali, vituo vya afya na katika ngazi ya jamii kwa kushirikiana na wadau mbali mbali
- b) Utayarishaji wa mpango mkakati wa lishe wa miaka 5 (*Nutrition Strategic plan*)
- c) Kuendesha mafunzo mbali mbali kwa wafanyakazi wa afya na jamii
- d) Kutoa matone ya vitamin A na dawa za minyoo kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano

Kitengo cha Afya Bandarini

Mhe. Spika, kitengo cha afya bandarini kina jukumu la kuzuia na kuchukua tahadhari juu ya uingizwaji wa maradhi ya kuambukiza kutoka nje ya Zanzibar. Ili kuhakikisha azma hiyo inafikiwa, kitengo hulazimika kufanya ukaguzi wa vyombo vinavyoingia kutoka nje ya Zanzibar na kusimamia upulizaji na ufukizaji wa dawa kwa ajili ya kuua wadudu wanaosambaza maradhi. Aidha, kutoa ushauri na kusimamia usafi wa mazingira katika eneo la bandarini na uwanja wa ndege na kutoa elimu ya afya katika sehemu za kazi pamoja na kukagua wasafiri wanoingia nchini kutoka nje ya Tanzania.

Mhe. Spika, katika mwaka 2011/2012, Kitengo kimefanikiwa kukagua jumla ya vyombo 2731. Kati ya hivyo vyombo 12 vilifukizwa (*fumigation*) kutokana na kuwepo kwa mende na panya ndani ya vyombo hivyo, vyombo 25 vimefanyiwa usafi (*disinfection/spray/traps*).

Mhe. Spika, jumla ya abiria 159,605 walikaguliwa (bandarini na uwanja wa ndege) kati ya hao 742 (0.46%) waligunduliwa kutokuwa na kadi za chanjo ya homa ya manjano. Miongoni mwa waliogundulika kutokuwa na kadi za chanjo watu 615 walibainika wametoka katika maeneo ambayo si hatarishi, watu 69 hawakuchanjwa kutokana na sababu za kiafya, na watu 58 walichanjwa mara tu walipowasili hapa Zanzibar.

Mhe. Spika, kwa upande wa chanjo za wasafiri, kitengo kilifanikiwa kuwapatia chanjo jumla ya wasafiri 818 ambao walikuwa wanataka kusafiri nje ya nchi, kati ya hao 468 walipatiwa chanjo ya homa ya manjano na 350 chanjo ya homa ya uti wa mgongo.

Mhe. Spika, kazi ya ukaguzi wa mitumba inayotoka nje ya nchi ilifanyika ambapo jumla ya kontena 65 zilizoingizwa nchini zilikaguliwa, kontena 52 zilikuwa za nguo, 9 za viatu na 4 za mikoba. Matokeo ya ukaguzi huo yalipelekea kontena 7 kurejeshwa kutokana na kukosa sifa, mabunda 51 ya nguo, magunia 19 ya mikoba na magunia 115 ya viatu yaliangamizwa kutokana na kutokidhi sifa za matumizi.

Mhe. Spika, Jumla ya wagonjwa 96 na maiti 93 waliopitishwa Bandarini na Uwanja wa Ndege walifanyiwa ukaguzi. Katika ukaguzi huo hakuna mgonjwa wala maiti aliyegunduliwa kuwa na dalili zozote zinazoashiria kuwa na maradhi ya kuambukiza.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2012/2013 kitengo kimepanga kutekeleza kazi kuu zifuatazo:-

- a) Kufanya mafunzo kwa wafanyakazi wa kitengo katika kada za ukaguzi wa ndege na meli kama inavyoelekezwa na shirika la afya duniani (*WHO*), na sheria ya afya ya kimataifa ya mwaka 2005 (*International health regulation 2005*)
- b) Kutayarisha utaratibu wa kutengeneza muongozo kazi wa utoaji huduma za afya bandarini

Programu ya Huduma za Macho (*Comprehensive Eye Care*)

Mhe. Spika, lengo kuu la programu ya huduma za msingi za macho (*Comprehensive Eye care Services*) ni kupunguza na baadae kutokomeza kabisa upofu unaoweza kuepukika au usio wa lazima.

Mhe. Spika, katika kuendeleza huduma za uchunguzi na utibabu wa macho vijijini, kitengo kiliendelea kutoa huduma katika vituo vya Afya vya Kidoti, Nungwi, Kivunge, Konde, Chwale, Ole, Finya, Vitongoji, Pujini, Tundauwa, Kisiwapanza, Bogoa na Kengeja. Ufafanuzi zaidi unapatikana katika Kiambatanisho namba 1. Aidha, jumla ya skuli 12 zilitembelewa na wanafunzi 2,452 walichunguzwa, kati ya hao 1,956 waligundulika kuwa na matatizo na kupatiwa matibabu. Halkadhalika, jitihada zilifanyika za kuongeza idadi ya wagonjwa wanaopata huduma za uchunguzi na upasuaji kwa njia ya huduma masafa (*Outreach Screening and Surgical Visits*), jumla ya wagonjwa 697 walichunguzwa.

Mhe. Spika, katika kipindi hiki mafunzo mbali mbali kwa wafanyakazi wa vituoni yalitolewa, yakiwemo uchunguzi wa watoto wachanga "*Neonatal eye screening trial*" (*NEST*), na uchunguzi wa vitovu na macho kwa watoto wachanga (*Pioneering Ophthalmia Neonatorum study*). Aidha mfanyakazi mmoja kutoka Pemba alihudhuria masomo yanayohusu huduma za uoni hafifu (*Low Vision*) nchini Sweden kwa kupitia msaada wa *Rottary Club* kwa muda wa wiki tatu.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2012/2013 programu imejipangia kutekeleza kazi kuu zifuatazo:-

- a) Kuimarisha afya za wanafunzi wa skuli za msingi na kati pamoja na huduma za macho vijijini, kwa kuwafanyia uchunguzi wa macho wananchi katika vituo vya afya vijijini
- b) Kushirikiana na madaktari bingwa wa Muhimbili katika kuwapatia huduma za upasuaji watoto wadogo
- c) Kufuatilia utendaji na mwenendo wa shughuli zinazohusu upimaji na utoaji wa miwani

Programu ya maradhi yasiyopewa kipaumbele (Kichocho, Minyoo, Mabusha na Matende)

Mhe. Spika, ni dhamira ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, kupitia Wizara ya Afya, chini ya uratibu wa Programu hii, kuwaondolea wananchi matatizo yote yatokanayo na maradhi ya Kichocho, Minyoo, Mabusha na Matende. Katika kipindi cha 2011 – 2012 jumla ya Wananchi 1,747 walifanyiwa uchunguzi, kati ya hao watu 114 walichunguzwa vimelea vya Matende, na watu 1,633 walichunguzwa vimelea vya kichocho. Watu 1,485 (Wanaume 1,283 na Wanawake 202) walionekana na matatizo ya Kichocho na hakuna aliegunduliwa na Matende.

Mhe. Spika, katika mpango wa utekelezaji wa mradi wa kutokomeza Maambukizi ya Kichocho Zanzibar (*Zanzibar Elimination of Schistosomiasis Transmission*), programu imeona haja ya kufanya utafiti ili kubaini maeneo yanayoathirika na ugonjwa huo, ambapo utafiti wa maradhi ya kichocho ulifanyika katika shehia 45 za Unguja na shehia 45 kwa Pemba kwa watu wenye umri wa miaka 20 hadi 55. Shehia hizo ziliteuliwa kutokana na vigezo maalumu ikiwa ni pamoja na mkusanyiko wa maji, mito, maziwa na mabwawa, vile vile utafiti kama huu kwa watoto wadogo ulifanyika katika skuli 45 za Unguja na skuli 45 za Pemba. Shehia husika ni zile ambazo zilitumika katika kuangalia hali ya kichocho kwa wenye umri mkubwa. Matokeo ya tafiti hizo yanaonesha kwamba asilimia 4 ya waliochunguzwa, waligunduliwa kuwa na maradhi ya kichocho. Ufafanuzi zaidi unaonekana katika kiambatanisho namba 2.

Mhe. Spika, kwa upande wa maradhi ya mabusha, Programu imefanikiwa kupunguza kwa kiasi kikubwa matatizo yatokanayo na Mabusha (Ngiri Maji), ambapo jumla wagonjwa 81 wamefanyiwa upasuaji wa maradhi hayo katika hospitali mbali mbali katika mwaka wa fedha uliomalizika.

Mhe. Spika, kwa nia ile ile ya kutokomeza maradhi ya kichocho Zanzibar, ukaguzi wa Mito, Maziwa na Mabwawa umefanyika kwa lengo la kuangalia makonokono wenye uwezo wa kusambaza maradhi ya kichocho katika sehemu mbali mbali za Unguja na Pemba. Aina mbali mbali za makonokono yaligunduliwa zikiwemo "*Cleopatra, Bulinus globosus, Bulinus nasutus, Pillar, Thiara, Forskali*" lakini aina ya *Bulinus globosus* ndio ambao walionekana kuwa na vimelea vya ugonjwa huo. Hatua hii ni muhimu sana katika kutafuta dawa sahihi ya kupambana na makonokono hayo.

Mhe. Spika, Ukamataji wa mbu wanaosababisha matende unaendelea na uchunguzi wa damu kwa maradhi ya matende umefanyika kwa watu 300 kutoka shehia za Kilimani, Makadara na Kwahani. Matokeo ya uchunguzi yalionesha hakuna mtu mwenye vimelea vya maradhi hayo. Aidha, uchunguzi wa maambukizo mapya ya ugonjwa wa matende kwa watoto wadogo ambao walizaliwa baada ya kipindi cha utoaji wa dawa dhidi ya matende kilichofanyika kutoka 2001-2006 ulitekelezwa kwa mashirikiano na “*Centre for Neglected Tropical Diseases*” ya Chuo Kikuu cha Liverpool cha Uingereza. Katika uchunguzi huu jumla ya skuli 60 (30 Unguja na 30 Pemba) zilihusika. Wanafunzi 1,800 walishirikishwa katika zoezi hili, ambapo wanafunzi 90 (5%) waligundulika na vimelea vya matende.

Mhe. Spika, ili kuongeza uelewa wa jamii juu ya maambukizi ya kichocho, elimu ya Afya iliendelea kutolewa katika Shehia 15 Unguja na Shehia 15 Pemba zenye mkusanyiko wa maji, mito, maziwa na mabwawa. Pamoja na mafunzo hayo washiriki wamepata bahati ya kutembelea maeneo yenye matatizo ya kichocho na kuweza kutoa maoni yao ili kuondosha kabisa maambukizo ya kichocho.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2012/2013 kitengo kimejipangia kutekeleza kazi kuu zifuatazo:-

- a) Kuendeleza kazi za utafiti kwa ajili ya kuimarisha mbinu za mapambano dhidi ya maradhi yasiyopewa kipaumbele (*neglected tropical diseases - ntds*)
- b) Kushirikiana na taasisi mbali mbali za ndani na nje ya nchi katika kufanikisha upatikanaji wa dawa na huduma za kupambana na maradhi ya kichocho, minyoo na matende
- c) Kitengo kitaendelea kutoa elimu na kufuatilia mafanikio ya kazi za utoaji dawa dhidi ya kichocho na minyoo maskulini

Kitengo cha Afya na Usalama wa Wafanyakazi. (*Occupational Health*)

Mhe. Spika, Kitengo cha Afya na Usalama wa wafanyakazi kina malengo ya kuangalia afya na Usalama wa wafanyakazi wakiwa kazini, kwa madhumuni ya kupunguza athari na madhara yatokanayo na kazi na mazingira yake.

Mhe. Spika, ili kuhakikisha mazingira bora ya wafanyakazi na maeneo wanayoyafanyia kazi. Kitengo kimeendelea kufanya ukaguzi katika sehemu mbali mbali za kazi zikiwemo Hoteli, Vilabu vya Vileo (Bar), Mikahawa na nyumba za kulala wageni (16), katika ukaguzi huo kitengo kilitoa maelekezo ya kuimarisha usafi, upimaji wa afya za wafanyakazi na jinsi ya kujikinga na maafa.

Mhe. Spika, kitengo kimeendelea kutoa huduma za uchunguzi wa afya za wafanyakazi na kutoa ushauri kwa waliogundulika na matatizo, jumla ya wafanyakazi 3,154 walichunguzwa afya zao kutoka taasisi za kiserikali na zisizo za kiserikali, ufafanuzi unapatikana kiambatanisho namba 3. Baadhi ya Wafanyakazi waliochunguzwa waligunduliwa na matatizo tofauti, yakiwemo UKIMWI 13, Shindikizo la damu 54, Homa ya ini B na C 21 na mengineo.

Mhe. Spika, kwa mwaka 2012/13 kitengo kimejipangia kazi kuu zifuatazo:-

- a) Kuendeleza ukaguzi wa mazingira sehemu za kazi
- b) Kusimamia uchunguzi wa afya za wafanyakazi
- c) Kuimarisha huduma za kitengo cha afya na usalama wa wafanyakazi kazini Pemba

Kitengo cha kufuatilia mwenendo wa maradhi (*Epidemiolojia*)

Mhe. Spika, Kitengo cha kufuatilia mwenendo wa maradhi (*epidemiolojia*), kina jukumu la kuratibu, kufuatilia mienendo ya maradhi, kutafuta vyanzo na vichocheo vya maradhi pamoja na kuchukua hatua za kukabiliana na maradhi pamoja na majanga mengine.

Mhe. Spika, katika kuimarisha upatikanaji wa taarifa sahihi na kwa wakati za magonjwa na miripuko, kitengo kimewapatia mafunzo ya msingi ya Mfumo wa taarifa za Kijiografia (*Geographic Information System - GIS*) kwa wafanyakazi 46 wa wizara ya afya (Unguja na Pemba), Lengo la mafunzo hayo ni kuwajengea uwezo watendaji hao ili waweze kuripoti hali ya maradhi yanayotokea kupitia mfumo huu.

Mhe. Spika, kitengo kimekuwa na utaratibu wa kupokea takwimu za mwenendo wa maradhi kwa kila wiki. Pale inapotekea takwimu za mwenendo huo katika eneo au shehia fulani zikawa si za kawaida, ndipo ufuatiliaji huanza kwa kwenda sehemu husika. Moja kati ya mbinu za kuchunguza chanzo cha maradhi ni kufanya ukaguzi wa maji katika vyanzo tofauti. Kuanzia Julai 2011 – Machi 2012 Sampuli 8 za maji kutoka kwenye visima, maji ya majumbani na kwenye mahodhi zilichukuliwa na kupelekwa maabara kwa uchunguzi zaidi. Matokeo yalionesha kwamba sampuli 3 kati ya hizo zilionekana kuwa na vimelea vya maradhi. Miongoni mwa hatua zilizochukuwa ni kuweka dawa ya (*Chlorine*) kwenye vianzio vya maji, kutoa elimu ya afya kwa jamii.

Mhe. Spika, kwa mnasaba huo, kitengo kilishiriki kikamilifu kufuatilia mripuko wa maradhi ya surua nchini hususan katika Wilaya za Mjini, Magharibi na Mkoani, kitengo kwa kushirikiana na kitengo cha Chanjo na timu za afya za wilaya kilifanya uchunguzi wa chanzo cha maradhi hayo, na baadae kuamua kuchanja watoto wote wenye umri wa miezi sita hadi miaka mitano.

Mhe. Spika, kufuatia kwa ongezeko la ajali za barabarani kitengo kilifanya utafiti mdogo (*operational research*) kwa Mkoa wa Mjini Magharibi ambao ulilenga miaka miwili nyuma (2009-2010), na matokeo ya utafiti huo ulionesha kuwa jumla ya ajali zilizotokea kwa mwaka 2009 ni 583 na 2010 ni 692, waliojeruhiwa kwa mwaka 2009 wanawake 498 (74%) na wanaume 114 (26%). 2010 waliojeruhiwa wanaume 692 (85%) na wanawake 179 (15%). Vifo vilivyotokea kwa mwaka 2009 ni 55 (9%) na 2010 ni 54 (8%).

Mhe. Spika, kitengo cha *epidemiolojia* cha Wizara ya Afya kina mashirikiano mazuri na kitengo cha *epidemiolojia* ya mifugo katika kufuatilia taarifa za kutafunwa na mbwa pamoja na wanyama wengine, na kila wiki kitengo kinapokea taarifa za ugonjwa huo na hatua za lazima na za haraka zinachukuliwa.

Mhe. Spika, Katika mwaka wa fedha 2012-2013, Kitengo cha *Epidemiolojia* kitaendelea kufuatilia mienendo ya maradhi na kuishauri wizara katika kuandaa sera, mikakati na miongozo ya kukabiliana na maradhi ya miripuko na yaibukayo. Vile vile kitengo kina mpango wa kufanya tafiti mbali mbali za maradhi ya kuambukiza na yasio ya kuambukiza, na tafiti za wadudu wanaoeneza magonjwa hayo.

Kitengo cha Afya ya Mazingira

Mhe. Spika, Kitengo cha Afya ya Mazingira kinafanya kazi za kuimarisha, kustawisha na kulinda afya ya jamii kutokana na majanga yanayohusiana na mazingira kwa kutayarisha sheria, kanuni, miongozo na taratibu. Halikadhalika kitengo kinapanga taratibu za kutoa taaluma, mbinu, mikakati na kushajiisha jamii kuchukua hatua za kuimarisha usafi wa mazingira ili yasiwe chanzo cha maradhi na majanga.

Mhe. Spika, Mafunzo ya Mbinu Shirikishi jamii ya maji na usafi wa mazingira (*PHAST*) yalifanyika, lengo ni kuwawezesha wanajamii wa ngazi na rika tofauti kufahamu umuhimu na njia rahisi za kutumia maji salama na usafi wa mazingira, ili kuimarisha afya ya jamii. Njia hii inajumuisha mazoezi ya vitendo na utumiaji picha za kuchora kufikisha ujumbe. Kitengo kilifanya mafunzo kwa watu 40 kwa kila shehia za Wilaya ya Magharibi ikiwa ni sehemu ya kukamilisha wilaya za Unguja. Washiriki hao wanatumika kama wawezeshaji katika shehia zao katika mikakati ya kuinua na kuimarisha hali ya usalama wa maji na usafi wa mazingira.

Mhe. Spika, katika kukabiliana na majanga ya kimazingira nchini, kitengo kwa msaada wa *UNICEF* kimefanikiwa kununua mahema, viatu, mabwela suti, aproni, mabomba ya kufukizia dawa, *gloves* na maski na kusambazwa katika wilaya zote za Unguja na Pemba.

Mhe. Spika, Kwa mwaka 2012-2013, kitengo kimepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

- a) Kuhamasisha na kuiwezesha jamii kuchukua hatua za kuimarisha usafi wa mazingira kwa ajili ya kujikinga na maradhi
- b) Kujenga uwezo wafanyakazi wa afya juu ya kufanya uchambuzi yakinifu wa afya ya mazingira (*Environmental Health Impact Assessment*)
- c) Kusimamia ukamilishaji wa sheria ya maafisa afya ya mazingira na ya afya ya jamii
- d) Kuandaa tathimini ya ushughulikiaji wa taka za hospitali na kuandaa mpango madhubuti wa kuziteketeza taka hizo

Ofisi za Timu za Afya Unguja na Pemba

Mhe. Spika, majukumu ya Ofisi za Timu za Afya za Unguja na Pemba ni kusimamia utoaji wa huduma za afya katika ngazi za wilaya na vijiji. Pia ni kiungo muhimu kati ya Wizara ya afya, Wizara na Taasisi nyengine za Serikali na zisizo za Serikali za ndani na nje ya Zanzibar zinazoshughulikia kazi za utoaji wa huduma za afya katika wilaya na vijiji. Aidha, ofisi hizi zinasimamia na kuratibu kazi za timu za afya za Wilaya, hospitali za vijiji na vituo vya afya.

Mhe. Spika, ili kutekeleza malengo ya Idara kwa mwaka 2012/2013 idara inaomba kuidhinishiwa matumizi ya Tsh. 132,000,000.00 kwa kazi za kawaida Unguja na Tsh. 99,000,000.00 kwa Pemba.

IDARA YA TIBA

Mhe. Spika, Idara ya Tiba inajumuisha hospitali 4 za vijiji zikiwemo Makunduchi na Kivunge kwa Unguja, Micheweni na Vitongoji kwa Pemba; Hospitali 3 za Wilaya ambazo ni Hospitali ya Abdalla Mzee, Wete na Chake Chake Pemba. Pia idara inasimamia Mpango wa Damu Salama, Usafirishaji wa Wagonjwa nje ya nchi, Mradi wa Afya ya Akili na Mradi wa Chuo cha Madaktari Zanzibar.

Hospitali za Wilaya

Mhe. Spika, huduma katika hospitali za Wilaya na Vijiji zimeendelea kuimarika katika mwaka wa fedha 2011/2012. Huduma za wagonjwa wa nje (*out patient*), huduma za kulazwa wagonjwa na huduma mbali mbali za uchunguzi wa maradhi ziliendelea kutolewa kwa ufanisi katika hospitali hizo.

Hospitali ya Chake Chake

Mhe. Spika, katika kipindi cha mwaka 2011/2012 wizara imefanikiwa kuongeza vifaa vya uchunguzi wa maradhi kama vile mashine ya *Ultra-Sound* na mashine ya kupimia moyo (*ECG machine*). Aidha, kwa msaada wa ICAP Hospitali imefanikiwa kujenga maabara ya kisasa itakayosaidia kuleta ufanisi wa kazi za maabara kwa hospitali hiyo. Mbali na huduma za kawaida, maabara hiyo pia itatoa huduma za uchunguzi na matibabu ya ukimwi (*Care and treatment centre – CTC*) kwa wananchi wa Chake Chake.

Mhe. Spika, Kwa kipindi cha Julai 2011 hadi machi 2012 idadi ya wagonjwa wa ndani waliopokelewa walikuwa ni 4,391 na waliofariki ni 118 Sawa na asilimia (3) ya wagonjwa waliolazwa. Wagonjwa wa nje walikuwa ni 18,009. Kiambatanisho namba 4 kinafafanua zaidi.

Hospitali ya Abdalla Mzee

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2011/2012 hospitali ya Abdalla Mzee iliopo mkoani Pemba imefanikiwa kufanya ukarabati mkubwa wa tanuri la kuchomea taka za hospitali (*Incinerator*).

Mhe. Spika, Kwa kipindi cha Julai 2011 hadi machi 2012 idadi ya wagonjwa wa ndani waliopokelewa walikuwa ni 2,434 na waliofariki ni 50 Sawa na asilimia (2) ya wagonjwa waliolazwa. Wagonjwa wa nje walikuwa ni 10,643. Kiambatanisho namba 4 kinafafanua zaidi.

Mhe. Spika, napenda kuliirifu Baraza lako Tukufu kwamba Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China imekubali kuifanyia matengenezo makubwa hospitali hii, ikiwemo kuongeza majengo ya kutolea huduma hususan wodi ya wazazi na watoto wachanga. Hivi sasa wizara inasubiri ujio wa wataalamu kutoka China kuja kutembelea hospitali hiyo na kufanya tathmini kamili ya gharama na maeneo yanayohitaji kujengwa na kutengenezwa.

Hospitali ya Wete

Mhe. Spika, Katika kipindi cha Julai 2011 hadi Machi 2012, hospitali hii imefanikiwa kufanya matengenezo kwa baadhi ya majengo ya hospitali, ikiwa ni pamoja na kuweka *tiles* vyooni na kupaka rangi, utiaji wa mafeni katika Wodi ya Watoto na Wanaume pamoja na kulifanyia matengenezo gari la kubebea wagonjwa. Pia hospitali imefanikiwa kuchimba kisima cha makalbi na mipira kwa ajili ya kusambaza maji katika badhi ya maeneo ya

hospitali. Aidha, hospitali imepata msaada wa jokovu na matangi mawili ya maji (*sim tank*) zenye ujazo wa lita 2000 kila moja kutoka kwa Jumuiya ya Maendeleo ya Jimbo la Wete.

Mhe. Spika, kwa msaada wa ICAP hospitali imefanikiwa kujenga jengo la huduma za maabara itakayosaidia kuleta ufanisi wa kazi za maabara kwa hospitali hiyo, mbali na huduma hizo, jengo hilo pia litatumika kutoa huduma za kuwashughulikia na kuwatibu wagonjwa wa UKIMWI (*CTC*).

Mhe. Spika, kwa kipindi cha Julai 2011 hadi machi 2012 idadi ya wagonjwa wa ndani waliopokelewa walikuwa ni 3,156 na waliofariki ni 58 sawa na asilimia (2) ya wagonjwa waliolazwa. Wagonjwa wa nje walikuwa ni 25,306. Kiambatanisho namba 4 kinafafanua zaidi.

Hospitali za Vijiji (*COTTAGE HOSPITALS*)

Hospitali ya Makunduchi

Mhe. Spika, azma ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ni kuipandisha hadhi hospitali hii kuwa hospitali ya Wilaya. Katika kufanikisha lengo hili hospitali kwa kushirikiana na Shirika lisilo la kiserikali la Uingereza (*Health Improvement Project Zanzibar – HIPZ*) limefanikiwa kuzifanyia matengenezo nyumba 12 za wafanyakazi, kati ya hizo 9 tayari matengenezo yake yamemalizika, matengenezo hayo yamegharimu jumla ya Tsh. 51,586,600 mpaka kumalizika kwake. Aidha, hospitali imepatiwa mtambo maalum wa kuzalisha hewa ya *Oxygen (Oxygen Concentrator)*, mashine za uchunguzi (*Haematology and Chemistry*) pamoja na kuwapatia mafunzo wafanyakazi juu ya kutumia vifaa hivyo.

Mhe. Spika, jitihada nyengine zilizofanyika ni kumuendeleza kielimu mfanyakazi mmoja wa hospitali hii kwa mafunzo ya muda mrefu juu ya fani ya nuskaputi (*Anaesthesia*).

Mhe. Spika, Kwa kipindi cha Julai 2011 hadi Machi 2012 jumla ya wagonjwa 1,388 walilazwa hospitalini hapo ambapo kati yao 16 walifariki, hii ni sawa na asilimia (1%) ya wagonjwa waliolazwa. Aidha, jumla ya wagonjwa 13,670 wa nje walihudumiwa. Ufafanuzi zaidi unapatikana katika kiambatanisho namba 4.

Hospitali ya Kivunge

Mhe. Spika, kama ilivyo katika wilaya nyengine hospitali hii ina mchango mkubwa sana katika kuwapatia huduma za afya wananchi wa Mkoa wa Kaskazini Unguja. Kwa mwaka 2011/2012 jumla ya wagonjwa wa ndani 2,379 walihudumiwa kati yao 17 sawa na asilimia (1%) walifariki. Aidha, wagonjwa wa nje 45,637 walipatiwa huduma za nje katika hospitali hiyo. Kiambatanisho namba 4 kinafafanua zaidi.

Mhe. Spika, mafanikio mengine yaliyopatikana katika hospitali hii ni kukamilika kwa ujenzi wa tanuri maalum na la kisasa la kuchomea takataka za hospitali (*Incinerator*). Kukamilika kwa tanuri hilo kumeongeza hali ya usafi wa mazingira ya hospitali, hivyo kupunguza uwezekano wa usambazaji wa maradhi ya kuambukiza. (*Makofi*)

Mhe. Spika, miongoni mwa huduma muhimu wanazostahiki mama wajawazito, ni huduma sahihi kwa walioharibikiwa na ujauzito. Hospitali hii imekamilisha matengenezo makubwa ya chumba cha kutolea huduma za akina mama walioharibikiwa na mimba.

Mhe. Spika, kwa lengo la kuimarisha utoaji wa huduma katika hospitali hii, Wizara imetilia saina mkataba na Shirika lisilo la kiserikali *HIPZ* kuiendesha hospitali hii kwa mashirikiano. Kwa sasa Meneja wa Hospitali ameshaajiriwa na Serikali kupitia ufadhili wa shirika hili. Tuna imani kwamba uzoefu uliopatikana katika Hospitali ya Makunduchi utasaidia sana kuongeza ubora wa huduma za afya katika hospitali hii. (*Makofi*)

Hospitali ya Micheweni:

Mhe. Spika, hospitali hii ina uwezo wa kulaza wagonjwa 50. Katika kipindi cha Julai 2011 hadi Machi 2012, Hospitali ya Micheweni imefanikiwa kufanya matengenezo ya nyumba mbili za wafanyakazi, Chumba cha *Ultra-Sound* na wodi ya wanawake pamoja na jengo la maabara. Aidha, kwa mashirikiano na Timu za Afya ya Wilaya ya Micheweni (*DHMT*) hospitali imeweza kukodi na kuifanyia matengenezo nyumba moja kwa ajili ya wafanyakazi.

Mhe. Spika, katika kuimarisha upatikanaji huduma bora, hospitali imefanikiwa kupata vifaa mbali mbali ikiwemo Friji, Mashine ya kuhifadhia Damu, mashine ya kufanyia vipimo vya *Biochemistry* na *Haematology, Delivery Kits* na *Fetus heart Doppler*. Vifaa na zana hizi ni ufadhili kutoka Shirika la Jhpiego na ICAP Tanzania.

Mhe. Spika, moja kati ya mafanikio makubwa kwa hospitali hii ni kupatikana kwa daktari wa kigeni mzoefu wa maradhi ya akinamama, ambae kwa kushirikiana na madaktari wengine wa kizalendo waliopo hospitalini hapo wameweza kutoa huduma bora kwa wananchi. Ni azma ya wizara kuanza kutoa huduma za upasuaji kwa akina mama wajawazito pale vifaa vya upasuaji vitakapopatikana.

Mhe. Spika, kwa kipindi cha Julai 2011 hadi machi 2012 idadi ya wagonjwa wa ndani waliopokelewa walikuwa ni 2,092 na waliofariki ni 60 sawa na asilimia 3 ya wagonjwa waliolazwa. Wagonjwa wa nje walikuwa ni 14,967. Kiambatanisho namba 4 kinafafanua zaidi.

Hospitali ya Vitongoji:

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2011/2012 Hospitali ya Vitongoji imefanikiwa kutoa mafunzo kwa wafanyakazi wote wa Hospitali yanayohusiana na *Post Exposure Prophylaxis (PEP)*. Matengenezo madogo madogo kwenye wodi, vyoo, karo, nyumba za wafanyakazi na ghala ya madawa yamefanyika.

Mhe. Spika, katika kipindi cha Julai 2011 hadi machi 2012 idadi ya wagonjwa wa ndani waliopokelewa walikuwa ni 817 na waliofariki ni 7 sawa na asilimia 1 ya wagonjwa waliolazwa. Wagonjwa wa nje walikuwa ni 11,635. Kiambatanisho namba 4 kinafafanua zaidi.

Huduma za Uzazi katika Hospitali za Idara ya Tiba:

Mhe. Spika, katika kutekeleza mkakati wa kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi, huduma za kujifungua zinaendelea kuimarishwa katika hospitali hizi. Hadi kufikia mwezi wa Machi 2012 jumla ya wajawazito 8,090 walilazwa katika Hospitali za Idara ya Tiba Unguja na Pemba. Kati yao wajawazito 6,075 walijifungua kwa njia ya kawaida na 395 sawa na asilimia 5 walijifungua kwa njia ya upasuaji na akinamama 18 walifariki dunia. Jumla ya watoto 6,528 walizaliwa katika kipindi hicho. Kwa maelezo zaidi angalia kiambatanisho namba 5.

Mhe. Spika, suala la uzazi pia limekua likitoa mjadala mkali humu ndani ya Baraza lako hasa pale panapotajwa suala la wazazi kutakiwa kuchangia wanapopatiwa huduma hizo, na kusababisha mjadala huo kurudiwa mara kwa mara. (*Makofi*)

Mhe. Spika, ninachukua fursa hii adhimu, kumpongeza Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa tamko kubwa na zito la kufuta michango ya fedha kwa kinamama wanaojifungua hapa Zanzibar. Tamko hili lililotolewa Tarehe 09/05/2012 lina azma kuu ya kuwapunguzia makali kinamama wajawazito na tabaan tamko hili lina lengo la kupunguza vifo vya kinamama na watoto. Tamko hili linakwenda sanjari na malengo ya Millenia pamoja na mpango wa kukuza uchumi hapa Zanzibar (MKUZA). (*Makofi*)

Mhe. Spika, azma hii ya Kiongozi Mkuu wa Serikali ya kuhakikisha kuwa huduma zote za kujifungua zikiwemo zile za upasuaji zitakua bila ya malipo, yaani bure limepokelewa kwa moyo mkunjufu na Wizara ya Afya. Kwa kutekeleza agizo hili, wizara imeandaa mipango thabiti ya kuhakikisha kua Serikali inabeba mzigo wote wa kinamama kujifungua bure na kwa hali ya usalama katika vituo vyetu maalum vya afya, Hospitali za Vijiji (*Cottage Hospital*), hospitali za wilaya na hata hospitali kuu ya Mnazi Mmoja. (*Makofi*)

Mhe. Spika, kwa niaba ya Serikali napenda kurudia tena, kujifungua sasa ni bila ya malipo kwenye Hospitali za Serikali. Kwa mnasaba huo, ninachukua nafasi hii kuwashajiisha kinamama wajawazito waende kwenye Kliniki kupima na pia wajifungulie kwenye hospitali au kwenye vituo vya afya vinavyotoa huduma hii. (*Makofi*)

Halikadhalika, ninachukua fursa hii kutoa indhari kwa wananchi wote wale ambao watakaokabilia na changamoto za watendaji wetu kwa aina yoyote ile isiyopendeza, basi wasione ugumu kutuletea taarifa rasmi bila woga. Taarifa hizi ni vyema zikawasilishwa kwa utawala wa kituo cha afya au hospitali husika. Ikumbukwe kua mashirikiano tutayoyapata kutoka kwa wananchi ndio mafanikio ya agizo hili la kitaifa. (*Makofi*)

Huduma katika Kliniki Maalum:

Mhe. Spika, mbali na kuwepo kwa huduma za matibabu ya maradhi ya kawaida pia zipo kliniki zinazotowa huduma za matibabu ya maradhi maalumu, katika hospitali za Wilaya na Vijiji. Maradhi yanayoshughulikiwa katika kliniki hizi ni pamoja na shindikizo la damu, kisukari, macho, pua, masikio, koo, kifua kikuu, viungo, magonjwa ya wanawake, maradhi ya uasharati na ngozi. Kwa kipindi cha Julai 2011 hadi machi 2012 jumla ya wagonjwa 95,363 walipatiwa huduma katika kliniki hizo. Kiambatanisho namba 6 kinatoa ufafanuzi zaidi.

Mhe. Spika, katika juhudi za kukabiliana na magonjwa yasio ya kuambukiza, wizara imeboresha huduma za kudhibiti magonjwa hayo. Aidha, kitengo kimepata ufadhili wa miaka mitatu na nusu kutoka Mfuko wa Kisukari Duniani (*World Diabetes Foundation*).

Miongoni mwa kazi zitakazofanywa chini ya ufadhili huo ni pamoja na kufundisha wafanyakazi katika ngazi za afya ya msingi, kuhamasisha jamii, kufanya tafiti mbali mbali zinazohusiana na magonjwa yasio ya kuambukiza, kuvipatia vifaa vituo vya afya na kutengeneza miongozo ya matibabu. Ufadhili huo utagharimu jumla ya Dola za Kimarekani laki tano (500,000).

Matibabu nje ya Zanzibar:

Mhe. Spika, miongoni mwa majukumu ya Idara ya Tiba ni kusimamia matayarisho ya usafirishaji wa wagonjwa nje ya Zanzibar baada ya kushindikana kutibiwa katika hospitali zetu. Katika kipindi cha July 2011 – March 2012, vikao vya kuwahakiki wagonjwa (*Medical Board*) vilifanyika na jumla ya wagonjwa 1,086 walihakikiwa.

Kati yao wagonjwa 452 matibabu yao yalihatiji kupelekwa nje ya Zanzibar. Hadi kufikia Machi 2012 wagonjwa 157 tu ndio waliofanikiwa kupatiwa matibabu nje ya Zanzibar, kati yao watu wazima ni 95 na watoto 62. Watoto wote hao walisafirishwa kwa ajili ya kupatiwa matibabu ya moyo, watoto 7 walipelekwa Israel na watoto 55 walipelekwa India.

Mhe. Spika, ni vyema Wajumbe wa Baraza lako Tukufu wajuwe kwamba kupeleka wagonjwa kutibiwa nje ya Zanzibar kunaigharimu serikali fedha nyingi mno za kigeni. Kwa mwaka wa 2010/11 ni shilingi 906,295,038.00/= zilitumika kwa kazi hiyo na mwaka huu hadi Machi shilingi 616,091,417.00/= zaidi ya gharama hizo za Serikali ya Zanzibar, Serikali ya Oman imesaidia matibabu ya watoto 62 kupelekwa huko India na watoto 7 wamesaidiwa na serikali ya Israel.

Mhe. Spika, kwa niaba ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, napenda kutoa shukrani za dhiti kwa serikali ya Oman kwa ufadhili wa matibabu wa watoto waliopelekwa India na Serikali ya Israel kwa wale waliopelekwa Israel, kwani bila ya msaada huo hali za watoto wetu zingekuwa hatarini. Vile vile napenda kutoa shukrani zangu za dhiti kwa *Lions Club*, Serikali ya India pamoja na Spain katika msaada wao. (*Makofi*)

Mpango wa Damu Salama:

Mhe. Spika, Mpango wa Damu Salama una jukumu la kuhamasisha wananchi juu ya uchangiaji damu kwa hiari. Mpango huu unaendeshwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar pamoja na ufadhili wa Serikali ya Marekani kupitia mfuko wa dharura wa Rais wa Marekani (*PEPFAR*) na (*Center for Disease Control*). Lengo la mpango huu ni kuhakikisha upatikanaji wa damu salama na ya kutosha kutoka kwa wachangiaji wa hiari, ambayo itapatikana kwa urahisi pale inapohitajika.

Mhe. Spika, kwa kipindi cha mwaka 2011/2012 Mpango wa Damu Salama ulijipangia kukusanya jumla ya uniti 5,250. Hadi kufikia Machi, jumla ya uniti 6,627 za damu kutoka kwa wachangiaji wa hiari zilikusanywa na kuvuka lengo lililokusudiwa kwa uniti 1,377 sawa na asilimia 26.23, hongera sote. Damu hiyo hufanyiwa uchunguzi wa magonjwa ya *HIV*, *Syphilis* na *Hepatitis B and C* kabla ya kusambazwa katika hospitali mbalimbali za Unguja na Pemba kwa matumizi.

Mhe. Spika, mafanikio ya ukusanyaji wa uniti hizo yalitokana na juhudi za wafanyakazi husika kutoa elimu ya uhamasishaji katika sehemu mbali mbali kama vile maskuli, vyuoni, katika mikusanyiko ya kidini, vilabu vya mipira na sanaa na vikosi vya ulinzi. Elimu iliyotolewa ni juu ya umuhimu wa damu na uhamasishaji juu ya uchangiaji wa damu kwa hiari.

Mhe. Spika, utaratibu huu unasaidia upatikanaji wa damu ya kutosha na kuongeza idadi ya wachangiaji wa kudumu, ambapo baadhi ya vikundi vya jamii viliunda vilabu vya uchangiaji damu, “*Donor Clubs*” na hadi sasa kuna vilabu vipatavyo 50. Naomba niwashukuru kwa dhati kabisa wananchi wote waliojitolea kutoa damu ili kuokoa maisha ya wagonjwa.

Mhe. Spika, Mpango wa Damu Salama kupitia ufadhili wa *American Association of Blood Bank (AABB)* umetowa mafunzo (*mentorship*) kwa wafanyakazi juu ya uchunguzi wa damu na utengenezaji wa mazao ya damu. Aidha, wafanyakazi wa kitengo walipatiwa mafunzo ndani na nje ya nchi yakiwemo mafunzo juu ya huduma kwa wateja na wachangiaji damu.

Vile vile mpango umepata mtaalamu kutoka Kituo cha *Heukland University Blood Bank* cha Norway kwa muda wa mwaka mmoja, na mfunzi mmoja kutoka kituo cha mpango wa damu salama yuko mafunzoni nchini Norway katika kituo hicho.

Mhe. Spika, Mpango wa damu salama una mfumo ulioimarika wa takwimu kuanzia ukusanyaji, upimaji na usambazi damu ulio katika *computer “Blood Established Computerised Systems “BECS”*, ambao unaimarisha uwekaji na upatikanaji wa taarifa za damu kiurahisi. Pia umeongeza ufanisi na ubora wa mazao ya damu yanayotengenezwa kituoni. Vile vile Kitengo kimefanikiwa kutumia *M-Health* katika kutuma ujumbe mfupi wa maneno (*SMS*) kwa wachangiaji damu kwa kuwashukuru na kuwakumbusha tarehe zao za uchangiaji.

Mhe. Spika, Mpango wa Damu Salama kwa mwaka wa fedha 2012/2013 umejipangia kazi zifuatazo:-

- a) Kuhamasisha zaidi jamii na kukusanya unit 7,500 za damu kwa mwaka.
- b) Kuendeleza Kamati ya Damu Salama ya Taifa, ili kusimamia utumiaji mzuri wa damu.
- c) Kuimarisha uchangiaji damu kwa hiari na huduma za Damu Salama kwa upande wa Pemba.
- d) Kuziimarisha kluba za wachangiaji damu “*Donor Clubs*”.
- e) Kuondosha kabisa uchangishaji damu wa lazima kutoka kwa ndugu wa mgonjwa “*Replacement Donations*”.

Mhe. Spika, ili kutekeleza malengo ya Idara kwa mwaka 2012/2013 idara inaomba kuidhinishiwa matumizi ya shilingi 435,000,000.00/= kwa kazi za kawaida Unguja na shilingi 213,000,000.00/= kwa Pemba.

Idara ya Hospitali ya Mnazi Mmoja:

Mhe. Spika, Idara ya Hospitali ya Mnazi Mmoja ina jukumu la kusimamia uendeshaji wa Hospitali ya Mnazi Mmoja, Hospitali ya Wazazi Mwembeladu na Hospitali ya Wagonjwa wa Akili Kidongo Chekundu.

Hospitali ya Mnazi Mmoja:

Mhe. Spika, Hospitali ya Mnazi Mmoja yenye wastani wa vitanda 400 ina jumla ya wafanyakazi 746, ambao kati yao 27 ni madaktari bingwa (14 wageni na 13 wazalendo), 14 ni madaktari na 52 ni wasaidizi madaktari. Wauguzi waliopo hospitalini hapo ni 310, wataalamu wafani nyengine za afya kama vile maabara, X-Ray n.k ni 141 na waliobaki ni wahudumu pamoja na wataalamu wa fani nyengine.

Aidha utolewaji wa huduma katika hospitali hii umekuwa ukisaidiwa sana na timu za madaktari kutoka Jamhuri ya Watu wa China, Misri, Uholanzi na Cuba.

Mhe. Spika, katika kuendeleza juhudi za Wizara za kuifanya hospitali hii kuwa Hospitali ya Rufaa, Mpango Mkakati (*Strategic Plan*) wa miaka kumi umekamilishwa. Hatua za utekelezaji za mpango huo zimeanza, moja kati ya malengo ya mkakati huo ni kuanzisha Kitengo Maalum cha Utafiti chenye lengo la kufanya utafiti (*Operational Research*) pamoja na kutoa elimu kwa wafanyakazi juu ya njia mpya zilizogunduliwa za kukabaliana na maradhi mbali mbali.

Mhe. Spika, mashirikiano na hospitali nyengine za kimataifa ni mkakati unaotumiwa na Wizara katika kuimarisha huduma za hospitali hii. Kama nilivyoeleza katika Baraza lako Tukufu katika hotuba yangu ya mwaka wa fedha 2011/2012 kuwa hospitali hii imetiliana mkataba na Hospitali ya Chuo Kikuu cha Haukeland cha nchini Norway.

Napenda kulijuilisha Baraza kuwa mkataba huo umeanza kutekelezwa kwa wafanyakazi wetu watatu kwenda katika hospitali hiyo sambamba na wafanyakazi wao wawili kuja kufanya kazi hapa Zanzibar. Aidha, ujenzi wa nyumba ya madaktari hao umeanza kujengwa katika eneo la Chuo cha Taaluma za Sayansi za Afya Zanzibar, ambao unategemea kukamilika mwezi wa Oktoba mwaka 2012. (*Makofi*)

Mhe. Spika, uchunguzi wa maradhi ni sehemu muhimu katika kufanikisha matibabu ya mgonjwa. Kwa kuliona hilo, Wizara kwa kushirikiana na Shirika la *International Centre for AIDS Care and Treatment Programs (ICAP)* limelifanyia matengenezo makubwa jengo la huduma za maabara. Matengenezo hayo yaliyogharimu shilingi milioni 300 yameenda sambamba na uwekaji wa vifaa vya kisasa katika idara mbali mbali za maabara.

Mhe. Spika, huduma za meno hospitalini hapo zimeimarika sana baada ya kupokea viti 5 vya kisasa vya kutolea huduma hiyo pamoja na mashine ya *Digital ya X-Ray* ya meno. Aidha kufungwa kwa mtandao wa kompyuta wa kuhifadha kumbukumbu za wagonjwa utawezesha kupatikana takwimu sahihi za wagonjwa wa meno. Vifaa hivyo vyenye thamani ya shilingi 320,000,000/= vimegharamiwa na Shirika la "*Miracle Cornes of The World (MCW)*".

Mhe. Spika, kama nilivyoahidi katika Baraza lako Tukufu kwenye majumuisho ya hotuba yangu ya mwaka wa fedha 2011/2012 kuwa, Wizara yangu itaifanyia matengenezo makubwa Wodi ya Wagonjwa Mahututi (*ICU*), ahadi hiyo imetekelezwa kwa uwekaji wa vifaa vifuatavyo:-

- a) *Monitors* (6) kwa ajili ya kuangalia viashiria muhimu vya mgonjwa (*vital signs*).
- b) Mashine mbili za kumsaidia mgonjwa kupumua (*ventilators*).
- c) Mashine ya kuangalia madini ndani ya mwili (*electrolytes analyser*).
- d) Mashine ya kuangalia damu (*blood gas analyser*).
- e) *Drip* maalum (*infusion pumps*) 8.
- f) Mashine ya kupimia moyo ya kisasa (*ECG*) 1.

Mhe. Spika, sambamba na uwekaji wa vifaa hivyo hospitali iko katika hatua za mwisho za uwekaji mtandao wa hewa safi (*Piped Oxygen Air and Vacuum*) kwenye wodi ya *ICU*, wodi ya Wazazi, Chumba cha wagonjwa wa dharura na Chumba cha Upasuaji. Kazi hii inafanywa na kampuni ya *Tanzania Oxygen Limited* na inategemea kukamilika mwezi wa Agosti 2012. (*Makofi*)

Mhe. Spika, kukamilika kwa matengenezo hayo yaliyogharimu shilingi zisizopungua milion 500/= kutoka Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kumesaidia sana kuimarisha huduma katika hospitali hiyo. (*Makofi*)

Mhe. Spika, mafanikio ya kazi hii yametokana na mchango mkubwa wa Baraza lako Tukufu pale lilipoweka msisitizo kwa wizara na Serikali kwamba *ICU* hii ni muhimu na lazima ijengwe bila kusubiri misaada kutoka nje. Wizara inatoa shukrani za dhati kwako wewe Mhe. Spika pamoja na msimamo mwema wa Wajumbe wa Baraza lako. (*Makofi*)

Mhe. Spika, kwa lengo la kuimarisha afya za watoto wachanga, wizara kwa kushirikiana na *Haukeland University* imefanikiwa kuweka vifaa vya kisasa kwenye wodi ya watoto wachanga wenye umri chini ya mwezi mmoja (*Neonatal Ward*). Vifaa vyenyewe ni *Oxygen Concentrator* 5, *Oxymetry* 4, *Phototherapy Machine* 5, *Incubator* 3 na *Ambubag* 5. Ni imani yetu kuwa upatikanaji wa vifaa hivyo utasaidia sana kupunguza vifo vya watoto wachanga.

Mhe. Spika, kambi za madaktari kutoka Spain, Norway, India na Uturuki zimeendelea kufanyika katika Hospitali ya Mnazi Mmoja, ambapo kuanzia Julai 2011 hadi Machi 2012 jumla ya wagonjwa 822 walichunguzwa, kati yao 199 walifanyiwa upasuaji ikiwemo wa kichwa, uti wa mgongo, *Hypospadi*, *Urethral fistula*, *Post burn Contracture*. Kuja kwa madaktari hao kumeokoa matumizi ya fedha za kigeni dola za Marekani 1,596,000 (shilingi 2.6 billion), ambazo ama zingetolewa na wananchi au Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. (*Makofi*)

Mhe. Spika, kazi za utoaji wa huduma za matibabu zilifanyika kwa ufanisi, ambapo wagonjwa 84,161 walitibiwa na kati yao wagonjwa 906 walifariki dunia, Kiambatisho namba 7 kinaonyesha idadi ya wagonjwa wa nje, waliolazwa na waliofariki kuanzia mwezi wa July 2011 hadi Machi 2012.

Aidha, kiambatisho namba 8 kinaonyesha idadi ya wajawazito waliolazwa, waliojifungua kwa njia ya kawaida, kwa upasuaji na vifo vya akinamama vilivyosababishwa na uzazi. Halkadhalika idadi ya wagonjwa waliohudumiwa katika kliniki maalum za hospitali hiyo inapatikana katika Kiambatanisho namba 9.

Mhe. Spika, huduma za macho zimepata msukumo mkubwa baada ya kupata vifaa vya kisasa pamoja na daktari bingwa kutoka Jamhuri wa Watu wa China. Katika kipindi cha Julai 2011 hadi Machi 2012 jumla ya wangojwa 44,868 wametibiwa (wanawake 24,927, wanaume ni 12,464 na watoto 7,477).

Jumla ya wagonjwa 598 walifanyiwa upasuaji mkubwa na 773 walifanyiwa upasuaji mdogo. Kwa ujumla shughuli za upimaji wa miwani kwa kutumia vifaa vya kisasa ziliendelea vizuri na jumla wagonjwa 12,320 walipimwa na kati yao 7,155 walipatiwa miwani ya kusomea (wanawake 3,210 na wanaume 3,945).

Mhe. Spika, pamoja na mafanikio hayo ya Hospitali ya Mnazi Mmoja, kuna changamoto nyingi tunazozikabili, ili kuongeza ubora wa huduma za hospitali hiyo ambayo ndiyo tegemeo kubwa la wanyonge. Kiambatisho namba 10 kinaonyesha hali halisi na mahitaji ya wafanyakazi katika hospitali ya Mnazi Mmoja.

Mhe. Spika, uwezo wa serikali kuajiri bado haujatosheleza mahitaji haya na kwa hivyo juhudi za makusudi zinahitajika. Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora, imetuahidi kwamba itakuwa tayari kuajiri madkatari wowote kama wapo kulingana na mahitaji yetu. Notoa wito kwamba wale wazanzibari walioko nje ya Zanzibar warudi kushirikaina na wenzao katika kujenga taifa lao. Maslahi ya kada ya madakatari yanaboreshwa na yataendelea kuboreshwa, ili kutoa heshima kamili ya utaalamu wao. *(Makofi)*

Mhe. Spika, moja kati ya tatizo sugu la hospitali hii ni msongamano mkubwa kwa jamaa wa wagonjwa wanaokuja kuwatizama au kuwasaidia kuwapa huduma wagonjwa wao. Moja ya sababu ya msongamano huo ni upungufu wa wauguzi kuweza kukidhi wingi wa huduma za wagonjwa kwa wakati. Lakini, hiyo haitowi uhuru kwa jamaa wa wagonjwa kukaa ndani ya wodi masaa yote. *(Makofi)*

Kwa kupitia baraza hili naomba mashirikiano ya wananchi wanaokuja kuwatizama wagonjwa wawe wasikivu pale wanapooombwa na wauguzi wetu au daktari kuondoka saa za kutizama wagonjwa zinapokwisha au wauguzi wanapotaka kuwahudumia wagonjwa ndani ya wodi.

Hospitali ya Wazazi Mwembeladu:

Mhe. Spika, hospitali hii ambayo ni sehemu ya Idara ya Hospitali ya Mnazi Mmoja ina jumla ya vitanda 36 ambapo idadi ya wajawazito waliolazwa, waliojifungua kwa njia ya kawaida, waliofanyiwa upasuaji na waliofariki dunia inaonekana katika kiambatanisho namba 7.

Mhe. Spika, kwa dhamira ya kupunguza msongamano unaotokea katika hospitali ya kuu ya Mnazi Mmoja, wizara imekusudia kuimarisha huduma katika hospitali hii kwa kuipatia madaktari bingwa wa uzazi, ili iweze kutoa huduma za upasuaji.

Hospitali ya Wagonjwa wa Akili:

Mhe. Spika, hii ni hospitali pekee ya wagonjwa wa akili hapa Zanzibar ambayo ina jumla ya vitanda 110. Kuanzia Julai 2011 hadi Machi 2012 jumla ya wagonjwa wa nje 8,581 walipatiwa matibabu (4,118 ni wanaume na 4,461 ni wanawake). Aidha, wagonjwa wapya waliolazwa ni 176 (107 ni wanaume na 69 ni wanawake). Angalia kiambatanisho namba 7 kwa ufafanuzi zaidi.

Mhe. Spika, ujenzi wa jengo la ghorofa moja ambalo litatumika kwa ajili ya ofisi, mapokezi, huduma za matibabu ya nje pamoja na jiko umekamilika.

Mhe. Spika, pamoja na mambo mengine Idara ya Hospitali ya Mnazi Mmoja inatarajiwa kutekeleza kazi zifuatazo katika mwaka wa 2012/2013:-

- a) Kuendelea na matayarisho ya rasimu ya awali ya sheria ya kuifanya Hospitali ya Mnazi Mmoja kuwa shirika linalojitegemea.

- b) Kuendeleza matengenezo ya majengo yote ya Hospitali, vifaa, kuweka mitambo ya kisasa, pamoja na kuweka mazingira katika hali ya usafi.
- c) Kuimarisha utafiti juu ya magonjwa mbali mbali na matibabu yatolewayo Hospitalini.
- d) Kwa kushirikiana na wizara itashughulikia upungufu wa madakatari na wauguzi uliopo kwa kuajiri madakatari bingwa wa ndani na nje ya nchi, ili kukabili ongezeko la mahitaji ya huduma za afya.
- e) Kuimarisha mfumo wa mahusiano kati ya wagonjwa na uongozi wa hospitali.

Mhe. Spika, ili kutekeleza malengo yake kwa mwaka 2012/2013 Idara ya Hospitali ya Mnazi Mmoja inaomba kuidhinishiwa matumizi ya Tsh. 642,000,000.00 kwa kazi za kawaida.

Ofisi ya Mfamasia Mkuu wa Serikali:

Mhe. Spika, Ofisi ya Mfamasia Mkuu wa Serikali ina jukumu la kusimamia utekelezaji wa Sera ya Dawa (*National Medicine Policy*), kwa kuhakikisha upatikanaji wa dawa muhimu (*essential medicines*) na zana za tiba katika Hospitali na vituo vya Afya vya Serikali pamoja na kusimamia utumiaji sahihi wa dawa hizo (*rational medicine use*).

Mhe. Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2011/2012 serikali ilitenga jumla ya shilingi 748,487,000/= kwa ajili ya ununuzi wa dawa na zana za tiba na kwa upande wa washirika wa maendeleo (*DANIDA*) waliahidi kuchangia shilling billioni 1.5 kwa ajili ya ununuzi wa dawa pamoja na usambazaji ikiwemo gharama nyengine za kuendesha shughuli za dawa.

Hadi kufikia Machi 2012 jumla ya shilingi 1.0 bilion zimeshatolewa na *DANIDA* kwa ajili ya ununuzi wa dawa pekee na serikali imetoa jumla ya shilingi 279,201,000/= (37%) kwa ununuzi wa dawa. Washirika wengine wa maendeleo walichangia jumla ya shilingi 1,035,913,466/= ufafanuzi zaidi unaonekana katika kiambatisho namba 11.

Mhe. Spika, katika juhudi za kuhakikisha kuwa dawa zinawafikia walengwa utaratibu wa kuwataka madaktari kuandika cheti zaidi ya kimoja na nakala ya cheti hicho kubaki katika sehemu iliotolewa dawa umeanzishwa kwa majaribio katika hospitali ya Mnazi Mmoja. Iwapo mfumo huu utaonyesha mafanikio utatumika kwa hospitali na vituo vyote vya afya nchini.

Mhe. Spika, kazi ya kufanya ukaguzi katika hospitali na vituo vya afya ilifanyika kwa mafanikio makubwa na iliwezesha Ofisi ya Mfamasia Mkuu kugundua kasoro zilizojitokeza katika uhifadhi, utoaji na utumiaji wa dawa. Kasoro hizo ziliipelekea ofisi hiyo kuandaa mafunzo kwa madaktari wasaidizi yaliyohusu matumizi sahihi ya dawa.

Mhe. Spika, katika kuimarisha huduma za upatikanaji wa dawa bila usumbufu kwa wananchi, Wizara, Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo na Washirika wa Maendeleo wamekubaliana kwamba kuanzia mwaka wa fedha 2012/2013 kutumia mfumo wa "*Frame Work Contract*" katika ununuzi wa dawa. Mfumo huu utaruhusu kampuni itakayochaguliwa mwanzoni mwa mwaka kutuuzia dawa kwa kipindi chote cha mwaka.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2012/2013 Ofisi ya Mfamasia Mkuu wa Serikali itaanzisha mfuko maalum wa dawa muhimu (*Essential Medicine Basket fund*) ambapo serikali itaingiza shilingi 1.5 billioni na Danida watachangia 1.5 billion. Aidha, Wizara itaendelea kuwahimiza washirika wengine wa maendeleo kuingiza fedha za ununzi wa dawa kwa kutumia mfumo huu.

Mhe. Spika, ni matumaini ya wizara kuwa endapo fedha hizi zitapatikana kama zilivyopangwa kutakuwa na dawa za kutosha katika vituo vya afya hivyo wananchi hawatokuwa na haja ya kununua dawa muhimu.

Mhe. Spika, ili kutekeleza malengo yake kwa mwaka 2012/2013 Ofisi ya Mfamasia Mkuu wa Serikali, inaomba kuidhinishiwa matumizi ya Tsh. 1,547,000,000.00 kwa kazi za kawaida.

IDARA YA BOHARI KUU YA DAWA

Mhe. Spika, Idara ina jukumu la kupokea, kutunza pamoja na kusambaza dawa katika hospitali na vituo vyote vya afya vya Serikali Unguja na Pemba. Katika kutekeleza azma hiyo, idara hadi sasa inatumia mifumo miwili ya usambazaji wa vifaa vya tiba na dawa. Mifumo hiyo ni wa 'kit system' kwa dawa za vituo vya afya na 'bulk system' kwa ajili ya Hospitali za Wilaya na Hospitali ya Rufaa ya Mnazi Mmoja.

Mhe. Spika, ili kuleta ufanisi katika usambazaji wa vifaa vya tiba na dawa, idara ilianza kutumia mfumo kwa majaribio wa usambazaji wa dawa kulingana na mahitaji (*Pull system*) katika vituo vya afya 19 (10 Unguja na 9 Pemba) ambapo mahitaji halisi ya dawa na vifaa tiba hubainishwa na kituo cha afya kupitia wilaya husika. Majaribio haya yameonyesha mafanikio ya kuridhisha, ambapo idara itaongeza idadi zaidi kutoka vituo 19 hadi kukamilisha vituo vyote vya Unguja na Pemba.

Mhe. Spika, Idara kwa mwaka 2012/13 inakusudia kutekeleza kazi zifuatazo:-

- a) Kusambaza dawa na vifaa tiba katika hospitali na vituo vya afya kwa wakati
- b) Kuhakikisha kila Kituo cha Afya kinaboreshwa katika sehemu yake ya kuhifadhia dawa, kwa kuwa na vifaa sahihi vya kuhifadhia dawa

Mhe. Spika, ili kutekeleza malengo yake kwa mwaka 2012/2013 Idara ya Bohari kuu ya dawa, inaomba kuidhinishwa matumizi ya Tsh. 47,000,000.00 kwa kazi za kawaida.

OFISI YA MKEMIA MKUU WA SERIKALI

Mhe. Spika, Ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali ina jukumu la kutoa huduma za kitaalamu za uchunguzi wa ubora na usalama wa vyakula, maji, dawa, kemikali pamoja na kufanya uchunguzi wa vielelezo vinavyowasilishwa kutoka taasisi tofauti vinavyohusiana na makosa ya jinai.

Mhe. Spika, Ofisi ya Mkemia Mkuu kwa miaka mingi iliopita ilikuwa haina sheria ya kuiongoza, hivyo kuanzishwa kwa sheria ya Mkemia Mkuu inayojulikana kwa jina la "*Chief Government Laboratory Act No. 10* ya mwaka 2011" iliopitishwa na Baraza lako Tukufu, imeiwezesha ofisi hii kufanya kazi zake kisheria. Katika utekelezaji wa sheria hii Mwenyeketi na wajumbe wa Bodi itayosimamia utekelezaji wa sheria hii wameshateuliwa na tayari wameshaanza kazi rasmi baada ya kuzinduliwa na Wizara ya Afya.

Mhe. Spika, katika kipindi cha Julai 2011 hadi Machi 2012, maabara iliendelea na shughuli za kufanya uchunguzi ambapo jumla ya vielelezo 641 vilichunguzwa. Vielelezo hivyo vinatoka Jeshi la Polisi, Wizara ya Biashara Viwanda na Masoko, watu binafsi na kliniki za Mifugo. Ufafanuzi unapatikana kwenye kiambatisho namba 12.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2012/2013 maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali imejipangia kazi zifuatazo:-

- a) Kuandaa rasimu ya sheria ya kemikali
- b) Kununua vifaa vya kisasa vya kufanyia uchunguzi
- c) Kuwapatia mafunzo ya kiutaalamu wafanyakazi 8 wa maabara

Mhe. Spika, ili kutekeleza malengo yake kwa mwaka 2012/2013 Ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali, inaomba kuidhinishwa matumizi ya Tsh. 99,000,000.00 kwa kazi za kawaida Unguja na Tsh. 20,000,000.00 kwa Pemba.

Mhe. Spika, baada ya kutoa maelezo ya mafanikio na muelekeo wa baadae wa idara zinazotoa huduma za afya moja kwa moja kwa wananchi, sasa naomba unirusu kutoa mafanikio na muelekeo wa idara saidizi (*supporting functions*). Idara hizi ni Idara ya Sera, Mipango na Utafiti, na idara ya Utumishi na Uendeshaji.

IDARA YA SERA, MIPANGO NA UTAFITI

Mhe. Spika, Idara ina jukumu la kusimamia utekelezaji wa sera ya afya, kuratibu utayarishaji na utekelezaji wa mipango yote ya muda mfupi na muda mrefu. Aidha, idara ina jukumu la kufuatilia ukusanyaji, uchambuzi na

uwasilishaji wa takwimu mbali mbali za afya pamoja na kuratibu shughuli zote za tafiti zinazofanyika ndani ya sekta.

Mhe. Spika, tathmini na mapitio ya sera ya Afya ya mwaka 2011 imeonyesha kupatikana kwa mafanikio makubwa ndani ya kipindi cha miaka kumi iliyopita. Licha ya mafanikio hayo, sera ya afya imeainisha maeneo yenye upungufu na changamoto zinazoikabili sekta ya afya. Idara ya Sera, Mipango na Utafiti imeanza matayarisho ya kuandaa Mpango Mkakati wa Miaka mitano (2012/2017) ili kutekeleza sera hiyo.

Mipango na maendeleo ya kissekta

Mhe. Spika, muongozo wa kuchangia huduma za Afya umefanyiwa marekebisha, kwa kuangalia upya gharama halisi za kuchangia. Muongozo huo umeshajadiliwa na kupitishwa katika ngazi zote za Serikali, ikiwemo Kamati Tendaji ya Wizara, Kamati ya Makatibu Wakuu na mwishowe Baraza la Mapinduzi. Serikali imetoa maelekezo mapya kwa wizara ya Afya kwa haja ya kuufanya ueleweke kwa watendaji na wananchi ili kuepuka matatizo wakati wa kutekeleza.

Mhe. Spika, mpango wa kufanya maandalizi ya mfumo wa kutoa fedha kwa ngazi za vituo na hospitali kulingana na utendaji wa kazi unaofuata viwango (*Performance Based Financing*) upo katika hatua za matayarisho, hii ikiwa ni pamoja na kutoa mafunzo ya uwelewa kwa watendaji juu ya mfumo huu mpya. Mfumo huu unatarajiwa kufanyiwa majaribio (*Pilot*) katika wilaya ya Magharibi kwa Unguja na Mkoani kwa Pemba. Mfumo huu utasaidia kwa kiasi kikubwa kupandisha viashiria vya afya katika ngazi za Wilaya na kitaifa, vilevile kuwawezesha watendaji kubakia katika sehemu zao za kazi.

Mhe. Spika, umuhimu wa utafiti umepewa kipaumbele ili kuibua mambo mbali mbali ya kimaendeleo yatakayoongoza katika mipango na kutoa maamuzi sahihi juu ya utoaji huduma za afya kwa jamii. Katika kufanikisha mkakati huu shughuli za uratibu zinaendelea kufanywa na divisheni ya utafiti ili kuweza kujua tafiti zilizofanywa na zinazoendelea kufanywa kuanzia mwaka 2010/2011. Tafiti hizi ziko katika makundi matatu, zile ambazo zimekamilika na matokeo yake yameshatolewa, na ambazo zimekamilika na ziko katika uchambuzi, na zile ambazo zinaendelea. Uchambuzi zaidi unaonekana katika kiambatisho namba 13.

Mhe. Spika, mashirikiano ya pamoja na taasisi zinazoshughulika na tafiti ndani na nje ya nchi yameimarishwa, taasisi hizo zikiwemo *National Institute of Medical Research (NIMR)*, *Commission for Science and Technology (COSTECH)*, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii Tanzania Bara na Taasisi ya Tafiti za Baharini. Aidha mashirikiano kati ya Maabara ya Afya ya Jamii ya Chake Chake Pemba, Chuo Kikuu cha Taifa (SUZA) na Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais yameanza. Vile vile divisheni imefanya mkutano na wadau mbali mbali na kuzindua shughuli za Ofisi ya utafiti katika Sekta ya Afya.

Mhe. Spika, katika kutilia mkazo matumizi ya taarifa zilizo bora na sahihi katika kutimiza mipango na malengo na kutathimini mafanikio, divisheni ya taarifa za afya (HMIS) imezidi kuboresha mfumo wa kukusanya taarifa kwa njia ya computer (*District Health Information System-2*). Katika warsha za wizara za afya kwa nchi za Afrika ya mashariki na kusini iliyofanyika Dar es salaam, 2011, Wizara ya Afya Zanzibar ilitangazwa kuwa mshindi kwa kuwa na mfumo bora zaidi wa ukusanyaji wa taarifa za afya kwa nchi za ukanda huu. Mfumo huu hivi sasa unatumika kama mfano kwa nchi hizo. Hivi sasa divisheni taarifa za afya imeboresha matumizi ya teknolojia ya komputa kwa kuanzisha tovuti unaorusha taarifa mbali mbali za wizara kwa wananchi kwa kutumia lugha ya Kiswahili (www.zanhealth.go.tz).

Mhe. Spika, katika kipindi cha mwaka 2011/2012, mfumo wa taarifa za afya umepiga hatua kwa kuanzisha kitengo mama cha uratibu wa taarifa zote zenye kuhusiana na afya (Health Information System). Mfumo huu utakuwa na wigo mpana zaidi kwa kushirikiana na Ofisi ya Mrajis Mkuu wa Serikali kwa kupata taarifa za vizazi na vifo (*vital statistics*), na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali ili kupata taarifa za viashiria vya afya kupitia sensa na tafiti za sampuli (*survey*).

Mhe. Spika, divisheni ya ufuatiliaji na tathmini ina jukumu la kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa mpango wa wizara kulingana na malengo na makusudio yaliyowekwa. Kwa mwaka wa fedha 2011/2012 divisheni imeweza kufuatilia utekelezaji wa mpango kazi wa wizara kwa kuandaa ripoti za robo mwaka ambazo huwasilishwa kwa Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi katika mfumo wa Bango Kitita.

Mhe. Spika, divisheni imeweza kuandaa ripoti ya utekelezaji ya wizara kwa mwaka wa fedha 2010/2011 (Annual Performance Report) ambayo hutumika katika mkutano wa mwaka wa mapitio ya sekta ya afya. Ripoti hii inatumika kuelezea mafanikio na upungufu ikiwemo changamoto zinazojitokeza katika utoaji wa huduma za afya nchini, vile vile inatumika kutayarisha mpango wa muda wa kati wa matumizi wa wizara.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2012/2013 idara imejipangia kutekeleza kazi zifuatazo:-

- a) Kufanya makadirio ya mahitaji ya nyenzo na vifaa (Costing Exercise) za utoaji wa huduma za afya.
- b) Kutoa mafunzo kwa wakuu wa vitengo vya wizara juu ya Program based budgeting.
- c) Kutayarisha mpango wa uwekezaji wa wizara (*Investment Plan*).
- d) Kufanya tathmini ya vyanzo vya fedha na mtiririko wa matumizi ya fedha kwa sekta ya afya (*National Health Account*).
- e) Kutayarisha mpango kazi wa shughuli za utafiti kwa mwaka 2012/2013 na kuuwasilisha kwa wadau wa mambo ya utafiti.
- f) Kufuatilia tafiti za afya zilizofanywa na taasisi mbali mbali (*Health system research mapping*)
- g) Kusimamia utekelezaji wa mfumo wa kutahmini ufanisi kwa ngazi ya kituo na hospitali (*Performance Based Financing*)
- h) Kuanzisha mfumo wa majaribio wa ukusanyaji wa taarifa za kina mama waja wazito kwa njia ya komputa katika hospital ya ya Chake chake.

Mhe. Spika, ili kutekeleza malengo yake kwa mwaka 2012/2013 Idara ya Sera, Mipango na Utafiti, inaomba kuidhinishiwa matumizi ya Tsh. 132,000,000.00 kwa kazi za kawaida Unguja na Tsh. 66,000,000.00 kwa Pemba.

IDARA YA UTUMISHI NA UENDESHAJI

Mhe. Spika, majukumu ya Idara ya Utumishi na Uendeshaji ni kusimamia nidhamu, uwajibikaji pamoja na kujenga uwezo wa wafanyakazi na kutayarisha mazingira bora ya kazi ili kuongeza ufanisi. Aidha, Idara ina wajibu wa kusimamia haki, maslahi, na stahiki zote za wafanyakazi pamoja na kuimarisha uwekaji wa kumbukumbu za Wizara. Majukumu haya yanatekelezwa kupitia vitengo husika ikiwemo vya Utawala na Uendeshaji, Utumishi na Utunzaji wa Kumbukumbu. Mbali na hayo, Idara pia inahudumia utendaji wa kazi za taasisi maalum za Wizara.

Utawala na Uendeshaji

Mhe. Spika, kwa kushirikiana na vitengo husika, wizara kupitia Kitengo cha Sheria imeweza kuzipitia sheria mbali mbali zikiwemo Sheria ya chakula, dawa na vipodozi (*The Zanzibar Food, Drugs and Cosmetics Act, No.2 of 2006*) na Sheria ya Wauguzi na Wakunga (*The Nursing and Midwifery Act*) ambazo bado ziko katika hatua za awali. Vile vile imeandaa rasimu ya mswada wa sheria mpya itakayolinda kada na wataalamu wa afya mazingira (*Environmental Health Practitioners Act*) pamoja na rasimu ya sheria ya Afya ya Jamii (*Public Health Act*). Sheria zote hizi zimeshapitia ngazi zote na ziko hatua za mwisho kuwasilishwa katika Baraza la Wawalikilishi.

Mhe. Spika, Idara kwa kupitia Kitengo cha Ufundi, imekua ikifanya matengenezo ya miundombinu ya Idara na Vitendo mbali mbali vya Wizara. Katika kipindi cha mwaka 2011/2012 kitengo cha ufundi kwa kushirikiana na uongozi wa shehia ya Fujoni, kimefanikiwa kufanya matengenezo makubwa ya jengo la kituo cha Afya Fujoni, mfumo wa umeme katika jengo la Mapinduzi mpya na mfumo wa maji katika kituo cha Afya Chaani Masingini. Aidha, vipuri vya genereta la Hospitali ya Mnazi mmoja vilinunuliwa na kuliwezesha jenereta hilo kufanya kazi muda wote. Kitengo pia kimeanzisha tovuti iitwayo 'www.zanhealth.go.tz/hceu' ambayo itatumika kwa ajili ya hospitali na vituo vya afya kutuma maombi yao ya matengenezo pale yanapohitajika.

Nguvu Kazi kwa Ajili ya Sekta ya Afya

Mhe. Spika, katika kipindi cha mwaka 2011/2012 Idara kupitia Divisheni ya Nguvu Kazi imeendelea kutoa mafunzo ya muda mrefu na mfupi kwa wafanyakazi. Jumla ya wanafunzi 236 wamejiunga na mafunzo ya muda mrefu, chini ya ufadhili wa SMZ, Benki ya Maendeleo ya Afrika (ADB), Danida na Italian *Cooperation*. Wafanyakazi 14 wamepata mafunzo ya muda mfupi chini ya ufadhili wa Serikali za China, Belgium na UAE. Vile vile jumla ya wafanyakazi 90 wa fani mbali mbali waliopata mafunzo ya muda mrefu wamerejea kutoka masomoni na kupangiwa maeneo ya kazi. Ufafanuzi zaidi unaonekana katika kiambatisho namba 14.

Mhe. Spika, kwa nia ya kuimarisha nidhamu katika kazi idara pia imetoa mafunzo yanayohusu kanuni za utumishi serikalini ambapo jumla ya wafanyakazi 60 wamepatiwa mafunzo hayo. Wakati huo huo, idara imefanikiwa kuandaa mpango mkuu wa mafunzo (*training Plan*) wa wizara na utanza kutekelezwa mwaka ujao wa fedha 2012/2013. Aidha muhtasari wa muongozo wa mafunzo kwa wafanyakazi tayari uko katika hatua za mwisho.

Mhe. Spika, Wizara imefanikiwa kuajiri jumla ya wafanyakazi wapya thelathini na tisa (39) wa kada mbali mbali, pamoja na wafanyakazi sita 6 wa mkataba wa muda. Aidha, wizara imeweza kustaafisha jumla ya wafanyakazi 85, ambao arobaini na moja (41) wamestaafu kwa kufikia umri wa miaka sitini 60, na wafanyakazi arobaini na nne (44) wa mkataba wamestaafu kwa kumaliza muda wao wa mkataba. Pamoja na upungufu wa wafanyakazi unaoikabili sekta ya afya katika ngazi zote, lakini pia hakuna uwiano wa wafanyakazi wanaostaafu ukilinganisha na wale wapya wanaojiririwa. Kiambatisho namba 15a, 15b, na 15c vinaonyesha hali halisi ya wafanyakazi, mapungufu na wale wanaotarajia kustaafu kwa kipindi cha miaka mitano ijayo.

Mhe. Spika, katika jitihada za kuhakiksha upatikanaji wa taarifa sahihi za wafanyakazi idara imeimarisha matumizi ya mfumo wa elektroniki kuhifadhi na kuchambua taarifa za rasilimali watu (*human resource data base*) ambao umeimarisha upatikanaji wa taarifa za wafanyakazi kama vile kiwango cha elimu, muda wa kustaafu, kima cha mshahara, mahala anapofanyia kazi na stahiki zake. Aidha, kwa kutumia mfumo huu, wizara imekuwa na uwezo wa kutoa taarifa sahihi za wafanyakazi na kwa wakati.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2012/2013 idara imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

- a) Kuendelea kuwapatia mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi wafanyakazi wa Wizara ya afya ambapo, jumla ya wafanyakazi 45 wanatarajiwa kusomeshwa katika ngazi ya cheti, stahada na shahada kwa gharama za SMZ na washirika wa Maendeleo
- b) Kutayarisha Mipango na miongozo mbali mbali ya mafunzo kwa kutumia takwimu halisi zilizopo ndani ya data za mtandao wa nguvu kazi (*human resource database*).
- c) Kufuatilia upatikanaji wa ajira serikalini ambapo jumla ya nafasi 502 zimeombwa.
- d) Kutayarisha scheme of services za wafanyakazi wa sekta ya afya kwa kushirikiana na Wizara ya Nchi Ofisi ya Raisi Utumishi wa Umma na Utawala Bora.
- e) Kusimamia maandalizi ya kufikisha rasimu ya Sheria ya Afya ya Jamii (*Public Health Law*), na Sheria ya Wataalamu wa Afya ya Mazingira (*Environmental Health Practitioners Act*) katika Baraza la Wawakilishi.
- f) Kuendelea matengenezo ya miundo mbinu ya Wizara kama vile majengo, vifaa, maji, umeme kila inapohitajika.
- g) Kusimamia taratibu za uondoaji wa mali chakavu zinazomilikiwa na Wizara ya Afya.
- h) Kuzikusanya, kuzitathmini na kuzisajili nyaraka zote ambazo zitahitaji kupelekwa katika Idara ya nyaraka za Taifa kwa kuhifadhiwa au kuharibiwa pamoja na kuandaa orodha yenye kutathmini majalada ambayo yanafaa kuhifadhiwa na ambayo hayafai kwa hatua za kuharibiwa (*retention and disposal schedule*).
- i) Kuifanyia marekebisho sheria ya Hospitali Binafsi (*The Private Hospital Regulations Act, no. 4 of 1994*).

Mhe. Spika, ili kutekeleza malengo yake mwaka 2012/2013 Idara ya Utumishi na Uendeshaji Unguja, inaomba kuidhinishiwa matumizi ya Tsh. 9,998,034,000.00 kwa kazi za kawaida. Kati ya hizo Tsh. 9,649,034,000.00 kwa ajili ya mishahara na maposho, na Tsh. 349,000,000.00 kwa matumizi mengineyo (OC). Pia Idara kwa upande wa Pemba inaomba kuidhinishiwa jumla ya Tsh. 4,247,046,000.00 kwa kazi za kawaida. Kati ya hizo Tsh. 4,082,046,000.00 kwa ajili ya mishahara na maposho, na Tsh. 165,000,000.00 kwa matumizi mengineyo (OC).

TAASISI MAALUM ZA WIZARA YA AFYA

Chuo cha Taaluma za Sayansi za Afya, Zanzibar

Mhe. Spika, Chuo cha Taaluma za Sayansi za Afya Zanzibar kina jukumu la kufundisha wataalamu wa afya wa fani mbali mbali ili kukidhi mahitaji ya wataalamu hao katika sekta ya afya.

Mhe. Spika, chuo kinaendelea kutoa mafunzo kwa kiwango cha Diploma katika fani za Uuguzi (*General Nursing*), Wasaidizi Madaktari (*Clinical Officer*), Maafisa Afya ya Jamii na Mazingira (*Environmental Health Officer*), Mafundi Sanifu wa Maabara (*Laboratory Technicians*), Madaktari wa Meno (*Dental Therapy*) na Mafundi Sanifu wa Madawa (*Pharmaceutical Technicians*). Katika mwaka 2011 jumla ya wanafunzi 343 walihitimu katika mafunzo mbali mbali, wakati katika mwaka huu wa 2012 jumla ya wanafunzi 173 wamehitimu mafunzo yao ikiwa ni kada moja tu ya wauguzi. Hadi hivi sasa jumla ya wanafunzi 764 wa kada tofauti wanaendelea na mafunzo yao chuoni hapo. Ufafanuzi zaidi unapatikana katika kiambatisho namba 16 na 17.

Mhe. Spika, katika kipindi cha mwaka 2011/2012 chuo kimeweza kufungua tovuti “web site” inayopatikana kwa anuani ya <http://www.zchs.ac.tz/>, tovuti hii itatumika katika mawasiliano baina ya wadau mbali mbali na chuo. Aidha, tovuti hii pia itatumika wakati wa uwasilishaji wa maombi ya wanafunzi wanaotaka kujiunga na chuo.

Mhe. Spika, Chuo kinatarajia kuendelea na kazi ya kuipitia mitaala ya fani ya Afisa Tabibu na Afisa Afya ya Jamii na Mazingira, kazi hii itafanikishwa kupitia Mradi wa kupunguza Vifo Vitokannavyo na Uzazi. Aidha, mradi huu pia umesaidia kuajiri walimu wanne wa kudumu wa kada za Usaidizi Udaktari, Maabara na Famasia. Kazi hii ni muhimu katika kuhakikisha kuwa hadhi ya chuo kinafikia viwango vinavyokubalika Kitaifa na Kimataifa.

Mhe. Spika, kufuatia wimbi lililoibuka la uvamiaji wa maeneo ya chuo na watu kujenga majengo bila kujali na kuheshimu umiliki wa chuo hicho, chuo kimeamua kujenga ukuta unaolizunguka eneo lote la chuo. Kazi hii inafanywa na Idara ya Chuo cha Mafunzo Zanzibar, na itagharimu Tsh. 176,000,000.00

Mhe. Spika, wizara kwa kushirikiana na Serikali ya Oman inendelea na ujenzi wa madarasa na dakhalia za wanafunzi, kazi hii inatarajiwa kukamilika mnamo mwezi wa November 2012. Majengo haya yataongeza uwezo wa chuo kuchukuwa wanafunzi wengi zaidi.

Mhe. Spika, katika juhudi za kuinua hadhi ya chuo, kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Umoja wa mataifa chuo kimeanza matayarisho ya ujenzi wa maabara maalum “*Skilled laboratory*” ambayo itatumika kufundishia wanafunzi mafunzo ya vitendo wakiwa katika mazingira ya chuo. Michoro ya maabara hiyo ipo katika hatua za mwisho za matayarisho, na ujenzi utaanza katika mwezi wa Julai 2012.

Mhe. Spika, Katika mwaka 2012/13, Chuo kitaanza utekelezaji wa mtaala wa mafunzo ya utengenezaji wa vifaa vya hospitali (*Biomedical Engineering*), ambapo mkupuo wa awali utaanza na wanafunzi 10. Kuanzishwa kwa mtaala huu kumetokana na msaada mkubwa unaotolewa na hospital ya Chuo Kikuu cha Haukland cha Norway.

Mhe. Spika, mbali na mafanikio hayo, chuo bado kinakabiliwa na changamoto ya upungufu wa wafanyakazi wa kudumu hasa walimu, wataalamu wa teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA), Afisa tabitu, Daktari wa Meno, Maafisa wa Afya ya Jamii na Mazingira, pamoja na upungufu wa vitabu vya kisasa vya kufundishia.

Mhe. Spika, katika mwaka 2012/2013 chuo kimejipangia kutekeleza kazi zifuatazo:-

- a) Kuwaendeleza walimu katika fani zao walizonazo kimasomo na maslahi pamoja na kutafuta waalimu wapya kwa lengo la kuinua kiwango cha utoaji wa taaluma.

- b) Kutafuta mbinu mpya za jinsi chuo kitakavyojitegemea kifedha.
- c) Kuendeleza mashirikiano yaliyopo kati ya chuo na vyuo vyengine, wizara na taasisi nyengine za Serikali na binafsi ndani na nje ya nchi.
- d) Kuipitia mitaala ya fani za Afisa tabibu na Afisa Afya ya Jamii na Mazingira.

Mhe. Spika, ili kutekeleza malengo yake kwa mwaka 2012/2013 Chuo cha Taalum za Sayansi za Afya, kinaomba kuidhinishiwa Ruzuku ya Tsh. 556,920,000.00 kwa ajili yauendeshaji wa Chuo.

Bodi ya Ushauri wa Hospitali Binafsi

Mhe. Spika, bodi hii ilizinduliwa mwezi wa Juni 1995 na kuanza kazi zake za kusimamia mwenendo wa Hospitali binafsi kwa mujibu wa sheria za kuendesha Hospitali hizo (*Private Hospital Regulation Act No. 4 of 1994*). Kazi kubwa za Bodi hii ni kusimamia uanzishaji na uendeshaji wa Hospitali na vituo binafsi vya Afya kwa kuzikagua na kuzipatia maelekezo au hata kuzifunga kabisa na kuzisitisha kutoa huduma pale zinapokosa vigezo vinavyotakiwa. Aidha Bodi huhusika na usajili, kutoa leseni na kuweka masharti ya uanzishwaji wa Hospitali hizo, kwa hivi sasa kuna jumla ya vituo vya Afya binafsi 71, (Unguja 60 na Pemba 11).

Mhe. Spika, wajumbe wa bodi wameweza kukutana mara 6 katika kipindi cha mwaka mmoja ili kujadili masuala mbali mbali yanayohusiana na uendeshaji wa Hospital Binafsi. Aidha, bodi ilifanya ukaguzi wa hospital na vituo vyote 68 ambapo jumla ya vituo 9 vilifungwa kutokana na bodi kutoridhika na utaratibu wa uendeshaji. Baadhi ya vituo vilivyofungwa vilifunguliwa baada ya kufuata maelekezo yaliyotolewa na bodi hiyo.

Mhe. Spika, kwa mwaka 2012/2013 bodi imejipangia kazi zifuatazo:-

- a) Kufanya ukaguzi wa pamoja na wakaguzi kutoka Kamisheni ya utalii kwa hospitali zilizomo katika Hoteli za kitalii.
- b) Kuendelea na ukaguzi wa hospital na vituo vyote vya binafsi kwa nia kuhakikisha wanafuata sheria.

Bodi ya Chakula, Dawa na Vipodozi

Mhe. Spika, Bodi ya Chakula, Dawa na Vipodozi imeanzishwa kwa sheria ya Chakula, Dawa na Vipodozi Namba. 2. ya mwaka 2006 ili kusimamia ubora na usalama wa chakula, dawa, vipodozi na vifaa vya tiba vinavyoingia nchini.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2011/2012, bodi ilisajili Maduka 81 ya Chakula ya jumla na rejareja, Ghala 11 za Chakula, Bekari 9, Hoteli 10, Vioski 6, Viwanda vidogo vidogo vya Chakula 5, Supermaket 5, Maduka ya kuuzia nyama (*Butchers*) 99, Machinjio 4, Maduka ya Dawa baridi 173, Maduka ya Vipodozi 35, Ghala za Dawa 2 na aina 9 za dawa.

Mhe. Spika, bodi ilikagua Maduka 131 ya Chakula ya jumla na rejareja, Ghala 8 za Chakula, Hoteli 57, Mikahawa 8, Viwanda vya Chakula 7, *Supermarket* 6, Maduka ya kuuzia Nyama 174, Machinjio 17, Tani 20,430 za Chumvi, Lita 169,353 za Maziwa, Kilo 35,909 za Bidhaa na mazao ya baharini, Maduka ya Dawa 128, Ghala 6 za Dawa na Maduka ya Vipodozi 21.

Mhe. Spika, Maabara ya Bodi ya Chakula, Dawa na Vipodozi ilichunguza sampuli 835 za Chakula, sampuli 819 zilikuwa salama na sampuli 16 hazikufaa kwa matumizi ya binaadamu. Aidha, sampuli 35 za Dawa zilichunguzwa, ambapo sampuli 27 zilipasi na sampuli 8 zilifeli. Pia sampuli 63 za Vipodozi zilichunguzwa ambapo sampuli 60 zilionekana zinafaa kwa matumizi ya binaadamu na sampuli tatu (3) zilifeli. Sampuli 8 za Dawa za Mitishamba ambapo zote zilionekana zinafaa kwa matumizi ya binaadamu.

Mhe. Spika, Bodi iliteketeza jumla ya tani 5.48 za bidhaa za Chakula zisizofaa kwa matumizi ya binaadamu. Vile vile iliweza kuzuia kuingizwa nchini jumla ya tani 780 za unga wa ngano ambao ulibainika kuwa haufai kwa

matumizi ya Binaadamu. Bodi ilifanikiwa kumfikisha mfanyabiashara mmoja katika vyombo vya sheria kwa kosa la kutupa dawa kinyume na taratibu zilizowekwa.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2012/2013 bodi imekusudia kutekeleza kazi zifuatazo:-

- a) Kushiriki kikamilifu katika mpango wa uwiyo wa usajili wa Dawa kwa nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.
- b) Kuimarisha udhibiti na ukaguzi wa chakula, dawa na vipodozi hasa kisiwani Pemba.
- c) Kufanya marekebisha ya Sheria mbali mbali zinazohusiana na chakula, dawa na vipodozi.
- d) Kuendelea na kazi za ukaguzi katika sehemu mbali mbali.

Maabara ya Afya ya Jamii (PHL – IdCF) Pemba

Mhe. Spika, maabara ya Afya ya Jamii (PHL – IdCF) ni Taasisi ya Wizara ya Afya inayoendeshwa kwa kushirikiana na Taasisi ya IVO-de Carneri ya Milan Italy. Lengo kuu la taasisi hii ni kufanya tafiti juu ya mienendo ya maradhi yanayoathiri afya ya jamii pamoja na kutafuta mbinu mbali mbali za kuyadhibiti. Hii ikiwa ni sambamba na utoaji wa mafunzo kwa wafanyakazi wa sekta za afya wa ndani na nje ya nchi juu ya kufanya utafiti huo.

Mhe. Spika, maabara kwa kushirikiana na JOHN HOPKINS UNIVERSITY inafanya utafiti unaoitwa ‘*Chlorehexidine study*’, utafiti huu unaohusiana na kupunguza idadi ya vifo vya watoto wachanga ndani ya siku 28 za mwanzo tangu kuzaliwa kwa kutoa huduma sahihi ya vitovu vya watoto wachanga (*Cord care*). Hadi March 2012 jumla ya watoto 10,099 walihudumiwa kati yao 5,244 wanaume na 4,855 ni wanawake, kati ya hao 4,231 walizaliwa Hospitalini na 5,726 walizaliwa majumbani.

Mhe. Spika, bado Maabara inakabiliwa na changamoto ya uhaba wa watalamu wenye sifa na ujuzi katika nyanja za utafiti na wenye ubunifu wa tafiti zitakazowavutia wafadhili na kujenga mashirikiano na taasisi nyingine.

Baraza la Wauguzi na Wakunga

Mhe. Spika, Baraza la Wauguzi na Wakunga, Zanzibar linaendelea kutekeleza majukumu yake ikiwemo kusajili wauguzi na wakunga wote hapa Zanzibar, kutoa leseni kwa muuguzi au mkunga atakaetaka kufanyakazi nje ya Zanzibar, kuchukua hatua za kinidhamu pamoja na kumfutia usajili yeyote atakaekwenda kinyume na maadili ya uuguzi na ukunga. Majukumu haya yanatekelezwa chini ya sheria namba 9 ya mwaka 1985 iliyopitishwa na Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Spika, sheria ya wauguzi na wakunga imefanyiwa mapitio mwaka huu ili kukidhi na kuendana na mabadiliko ya shughuli za uuguzi na ukunga duniani. Rasimu ya sheria hii kama nilivyoanisha mwanzo ipo katika hatua za kukamilishwa.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa 2012/2013 Bara la Wauguzi litatilia mkazo zaidi mambo yafuatayo:-

- a) Kuhakikisha kwamba sheria mpya ya Baraza la Wauguzi na Wakunga ina kamilika na kufanyiwa kazi.
- b) Baraza lithakikisha kwamba huduma zote zinazotolewa na wauguzi kuwa ni Bora zaidi kwani wajumbe wa Baraza watafanya ukaguzi katika hospital zote za Unguja na Pemba.
- c) Baraza limejipangia kutayarisha “*Nursing Procedure manual*” ambazo zitasambazwa katika Hospital zote za Unguja na Pemba na kutakiwa kufuatwa na wauguzi wote.
- d) Kusimamia uvaaji wa Uniform kwa wauguzi wote pamoja na vitambulisho vyao yaani “*Identit*”.

- e) Katika kuadhimisha siku ya wauguzi duniani inayofanyika kila mwaka baraza kwa mwaka huu litafanya uchunguzi wa awali wa saratani ya shingo ya kizazi “*early screening of cervix carcinoma*” kwa akinamama na watakaogunduliwa na matatizo watapewa huduma zinazostahiki.

Baraza la Tiba Asili na Tiba Mbadala

Mhe. Spika, Baraza la Tiba Asili na Tiba Mbadala (*Traditional and Alternative Medicine Council*) ni chombo kilichoundwa chini ya sheria No 8 ya mwaka 2008, baraza hili linafanyakazi kisheria katika kusimamia, kudhibiti, kutangaza, kusaidia maendeleo ya shughuli za tiba asili na tiba mbadala, Zanzibar.

Mhe. Spika, kazi za baraza hili zimekuwa ni zenye kufanikishwa kupitia vikao vya baraza, ukaguzi wa maduka, dispensary, clinics za tiba asilia na vilinge, usajili wa waganga wa jadi, maduka ya dawa za asili, vituo vya tiba Asili pamoja na kueleimisha kwa kutumia vyombo vya habari kama vile Television na radio.

Mhe. Spika, katika kipindi cha 2011/2012, baraza liliongeza idadi ya waganga wa jadi waliosajiliwa kufuatia kutimiza masharti ikiwa ni pamoja na kuwa na sehemu za kudumu za kutolea huduma, ambapo jumla ya waganga wa jadi 39 walisajiliwa na kufikisha idadi ya waganga wa jadi waliosajiliwa kufikia 120, kutoka 81 waliosajiliwa mwaka 2010/11. Aidha jumla ya maduka 11 ya kuuza dawa asilia yameruhusiwa na kutimiza jumla ya maduka 19 kutoka 8 ya mwaka 2010/11.

Mhe. Spika, katika kuwadhhibiti waganga wa jadi wasiofuata sheria na taratibu zilizowekwa, baraza limefanikiwa kwa kiasi kikubwa kudhibiti matangazo ya Waganga wa Tiba Asili na waganga wanaokuja kutoka nje ya Zanzibar ambao si wa waganga halisi. Aidha, baraza limefungua mashtaka kwa mtu mmoja baada ya kukaidi kufuata sheria zinazohusiana na tiba asilia na tiba mbadala na kesi hiyo bado inaendelea.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2012/13 Baraza la Tiba Asili limedhamiria kufanya kazi zifuatazo:-

- a) Kuimarisha kuwepo kwa vikao vya Baraza vya kila baada ya miezi mitatu.
- b) Kuendelea kufanya ukaguzi na usajili wa Waganga, maduka na vituo vya afya vya Tiba Asili na Mbadala kwa lengo la kuelimishana kuhusu Tiba Asili na Mbadala.
- c) Kuendeleza kuelimisha wananchi juu masuala ya tiba asilia na tiba mbadala kwa kutumia program za televisheni na radio.

MIRADI YA MAENDELEO

Mhe. Spika, baada ya kuelezea utekelezaji wa kazi za kawaida kupitia Idara husika na Taasisi maalum za Wizara, sasa naomba uniruhusu kueleza utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Uendeshaji wa miradi hii unatokana na fedha za serikali, misaada na mikopo kutoka kwa washirika wetu wa maendeleo. Katika mwaka wa fedha ujawo 2012/2013, wizara inatarajia kutekeleza miradi kumi na mbili kati yao miradi mine ni mipya.

Mradi wa kusaidia kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi (SMMRP)

Mhe. Spika, Mradi wa Kusaidia Kupunguza Vifo Vitokanavyo na Uzazi umeanzishwa miaka 5 iliyopita, kufikia mwishoni mwa Disemba 2012 utakuwa umekamilisha miaka 5 ya utekelezaji wa majukumu yake. Juhudi za kutaka mradi uongezewe muda zinaendelea vizuri kwani maombi yamewasilishwa Benki ya Maendeleo ya Afrika (ADB). Taarifa za awali tulizozipata ni kwamba maombi hayo yatakubaliwa kwani mradi umefanikiwa kutekeleza zaidi ya asilimia tisini (90%) ya majukumu yake tokea kuanzishwa.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha wa 2011/2012 mradi ulipata mafanikio katika utekelezaji wa majukumu uliyojipangia. Wafanyakazi watatu wa fani ya “*Dental Therapist*” wamepelekwa Muhimbili Tanzania bara kwa masomo ya “*Assistant Dental Officer*” kwa muda wa mwaka mmoja na nusu. Vile vile mfanyakazi mmoja kutoka Chuo cha Taaluma za Sayansi za Afya alipatiwa mafunzo ya muda mfupi nchini Uganda kujifunza Mipango na Tathmin. Aidha, wafanyakazi watano wa mradi wameshiriki mafunzo mafupi ya Usimamizi wa Fedha na manunuzi huko Tanzania Bara.

Mhe. Spika, katika bajeti ya mwaka wa fedha 2011/2012 wizara yangu ilitoa taarifa ya kuanza ujenzi wa jengo la kuhudumia magonjwa ya maradhi ya akili kisiwani Pemba. Ujenzi unaendelea vizuri na umo kwenye hatua za mwisho. Mategemeo yetu Wizara itakabidhiwa jengo hilo si zaidi ya miezi mitatu ijayo.

Mhe. Spika, jukumu jengine ni kukisaidia Chuo cha Taaluma za Sayansi za Afya – Mbweni kiweze kujitegemea kwa kutafuta mtaalamu wa kutayarisha Mpango Endelevu wa Uzalishaji (*Sustainable Business Plan*). Hatua zilizofikiwa ni uchambuzi wa maombi (*Tender*) yaliyotumwa kutoka kwa wataalamu wenye nia ya kufanya kazi hiyo. Ripoti ya uchambuzi huo tayari imeshatumwa ADB kwa maelekezo na hatimae kufanya maamuzi.

Mhe. Spika, juhudi za kuvifanyia matengenezo vituo vya afya vya Bogoa na Weshu zimechukuliwa. Tenda kwa matengenezo ya kituo cha Bogoa imeitishwa na tathmini imefanyika, matengenezo yameanza na yanategemewa kukamilika baada ya miezi mitatu.

Mhe. Spika, Mradi kwa mwaka 2012/2013 umejipangia kutekeleza mambo yafuatayo kutegemea kuongezwa muda wa mradi:-

- a) Matengenezo makubwa ya jengo la huduma za uzazi na watoto kwenye Hospitali ya Wete
- b) Matengenezo ya vituo vya afya vya Mzambarauni na Weshu – Pemba na Mwera Unguja
- c) Kukamilisha utengenezaji wa “Sustainable Business Plan” kwa Chuo cha Taaluma za Sayansi za Afya mbweni
- d) Kuvipatia samani na vifaa vituo vitakavyojengwa upya
- e) Kulipatia vifaa na samani jengo la huduma za uzazi na watoto

Mradi Shirikishi wa Afya ya Uzazi na Mtoto (*Integrated Reproductive and Child Health Program*)

Mhe. Spika, Mradi Shirikishi wa Afya ya Uzazi na mtoto unajumuisha maeneo manne muhimu ambayo ni Afya ya uzazi na mtoto, chanjo kwa ajili ya kina mama na watoto (EPI), kuzuia maambukizi ya virusi vya Ukimwi kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto (PMTCT) na matibabu ya watoto (IMCI). Lengo kuu la kitengo hiki ni kuimarisha huduma za afya ya mama na mtoto. Shughuli zake zinachangia katika kufikia Malengo ya 4 na 5 ya Millennium, MKUZA na Dira ya Maendeleo ya 2020.

Mhe. Spika, Matokeo ya ukusanyaji wa taarifa za afya yanaonyesha kwamba vifo vitokanavyo na uzazi bado viko juu nchini mwetu (kati ya kina mama 100,000 wanaojifungua katika hospitali 284 hufariki kutokana na uzazi). Kwa mujibu wa utafiti uliofanywa “*Tanzania Demographic and Health Survey 2010*”, asilimia 49.2 ya kinamama wanaojifungua huzalishwa na wataalam wa huduma za uzazi. Hali hii si nzuri, kwani zaidi ya nusu ya kinamama wanazalishwa na watu wasiokua na taaluma za uzazi.

Mhe. Spika, kwa upande wa vifo vya watoto wachanga waliochini ya umri wa mwaka mmoja (*infants*) 54 hupoteza maisha kila mwaka kati ya watoto 1,000 walio hai. Pia kati ya watoto 1,000 walio chini ya umri wa miaka mitano 73 hupoteza maisha kila mwaka. Hali hii inaonyesha kwamba kwa vifo vya watoto chini ya mwaka mmoja tunaelekea kufikia malengo ya MKUZA II ya vifo 48 kati ya watoto 1000 ifikapo 2015, kwa upande wa vifo vya watoto chini ya miaka 5 bado kunahitajika jitihada zaidi ili kufikia malengo ya MKUZA ya kupunguza vifo kufikia 50 kati ya watoto 1000.

Mhe. Spika, moja kati ya jitihada zilizochukuliwa na mradi ni kutengeneza muongozo wa sera juu ya huduma ya mama baada ya kujifungua (*Post Natal Care Guidelines*). Aidha, mradi umetengeneza muongozo wa kufundishia wafanyakazi juu ya huduma hizo (*Training Manuals*). Pia mradi umekamilisha matayarisho ya kutathmini mahitaji ya huduma za dharura za afya ya uzazi na mtoto. Tathmini hiyo imeshaanza mwanzoni mwa mwezi huu wa Julai 2012.

Mhe. Spika, hivi sasa mradi huu hauna ofisi ya kudumu ambayo itaweza kuifanikisha utendaji wa mradi, kwa min-ajili hiyo wizara imekusanya nguvu za kuhakikisha kwamba jengo la mradi huu linajengwa katika eneo la Hospitali ya Kidongo Chekundu litakalogharimu Tsh. 950 milioni zitakazotolewa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Jengo hili pia litakuwa na sehemu maalumu ya kuhifadhiwa dawa za chanjo.

Mhe. Spika, juhudi za kuepusha maambukizi ya VVU kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto zimefanyika. Tathmini imefanyika kwenye vituo vya afya 61 kwa ajili ya kuanzisha huduma za kuzuia maambukizi ya mama kwenda kwa mtoto (PMTCT). Tathmini hii ilijumuisha vituo vya afya 36 vya Unguja na vituo 25 kutoka Wilaya za Pemba. Hii itapelekea kuwa na vituo 111 ambayo ni sawa asilimia 72% ya vituo vyote vinavyotoa huduma ya afya ya uzazi na mtoto. Jumla ya wajawazito 38,797 walichunguzwa VVU katika kliniki na wodi ya wazazi na kati yao wajawazito 284 waligundulika na VVU (0.7%).

Mhe. Spika, Muongozo mpya wa kuzuia maambukizi ya VVU kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto unaojumuisha mapendekezo yaliyotolewa na Shirika la Afya Duniani tayari unatumika, na wafanyakazi wa vituo vyote wameshapatiwa mafunzo ya matumizi ya muongozo huo.

Mhe. Spika, Katika kuimarisha utoaji wa huduma za afya ya uzazi na mtoto, wafanyakazi 240 walipatiwa mafunzo mbali mbali yakiwemo ya huduma ya mtoto mchanga, njia mbali mbali za uzazi wa mpango, huduma baada ya kuharibu mimba na uzuiaji maambukizi ya VVU kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto.

Mhe. Spika, Kitabu cha “Uislamu na Uzazi wa Mpango” kimetengenezwa na kuzinduliwa kwa dhamira ya kuelimisha na kushajihisha jamii juu ya kukubali njia bora na sahihi za uzazi wa mpango kwa mnasaba wa desturi za Dini ya Kiislamu. Aidha, mradi umeanzisha vikundi vya vinara (*champions*) wa uzazi wa mpango vyenye kushajihisha jamii na ushiriki wa wanaume katika masuala ya afya ya uzazi. Halikadhalika, siku maalumu zimepangwa kwa ajili ya kutoa huduma za afya ya uzazi jambo ambalo limesaidia kuongeza watumiaji wa huduma hizo.

Mhe. Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2011/2012, Wizara ilifanya Kampani za chanjo ya surua na polio kwa watoto na matokeo yalikuwa ni; Chanjo ya surua na ugonjwa wa kupooza kwa watoto wenye umri wa chini ya miaka mitano yalikuwa ni zaidi ya asilimia 91. Mchanganuo huo unaonekana kwenye kiambatisho namba 18, na kwa upande wa chanjo za kawaida unaonekana kiambatisho namba 19a na 19b.

Mhe. Spika, mnamo mwaka 2011 kulitokea miripuko ya surua iliyoripotiwa kutoka wilaya za Magharibi, Mkoani, Chakechake, Wete na Micheweni. Ufatiliaji wa chanzo cha miripuko hiyo ulifanyika kwa mashirikiano na wataalamu wa shirika la Afya Ulimwenguni na Shirika la kimataifa la kuhudumia watoto. Mashirikiano hayo yalitupa mafanikio na kuweza kuthibiti miripuko yote.

Mhe. Spika, wagonjwa wawili (2) wa pepopunda ya watoto wachanga waligundulika kutoka wilaya za Mjini na Micheweni na Ugonjwa wa kupooza uligundulika kwa wagonjwa wanne (4) waliotoka katika wilaya za Mjini, Magharibi, Kaskazini-B na Wete.

Mhe. Spika, katika kufanikisha malengo yake kwa mwaka 2012/2013 kitengo kimepanga kutekeleza kazi kuu zifuatazo:-

- a) Kufanya mapitio ya utekelezaji wa mpango mkakati (*Road map review*) wa mradi kwa lengo la kuimarisha ubora na viwango vya huduma.
- b) Kufanya tathmini ya kina ya shughuli za mradi wa afya ya uzazi na mtoto kuangalia mafanikio, changamoto ili kuweza kupanga mpango wa uhakika (*evidence based plan*).
- c) Kuimarisha huduma za afya ya uzazi kwa vijana.
- d) Kuimarisha huduma za dharura za afya ya uzazi.
- e) Kuendelea kutoa huduma za chanjo kwa mama na watoto katika vituo vyote vya huduma za mama na watoto pamoja na kusimamia huduma za mikoba (*Outreach services*) katika maeneo mbalimbali.
- f) Kuendeleza jengo la ofisi za mradi shirikishi wa afya ya uzazi.
- g) Kuelimisha na kushajihisha jamii juu ya mbinu na mikakati sahihi ya kuimarisha afya ya mama na mtoto.

- h) Kuendeleza chanjo ya pepopunda kwenye skuli za sekondari.
- i) Kufanya matengenezo ya ofisi ya chanjo Pemba na kujenga vyumba vya baridi (*cold rooms*) Unguja na Pemba.
- j) Kuwaendeleza wafanyakazi wa ngazi zote kwa kuwapatia mafunzo mbali mbali (yakiwemo ya uongozi na ya utekelezaji wa kazi za chanjo za kila siku).
- k) Kuanzisha chanjo mpya dhidi ya maradhi ya homa ya mapafu na homa ya uti wa mgongo (*pneumococcal vaccine*).
- l) Kuimarisha mfumo wa ufuatiliaji wa magonjwa ili kufikia viwango vilivyowekwa na Shirika la Afya Ulimwenguni (*WHO*).

Mradi shirikishi wa kudhibiti Ukimwi, Kifua Kikuu na Ukoma (*Zanzibar AIDS/TB & Lep. Control Programme*)

Mhe. Spika, mradi shirikishi wa Ukimwi, Kifua kikuu na Ukoma ni muunganisho wa Mradi wa Kudhibiti Ukimwi na Kitengo cha Kudhibiti kifua kikuu na Ukoma. Azma ya kuanzishwa mradi huu ni kuweza kuimarisha nguvu kazi na kurahisisha utendaji.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2011/2012 mradi umefanikiwa kufanya ukaguzi katika vituo vinavyotoa huduma za tiba za Ukimwi, kifua kikuu na ukoma. Lengo kuu ni kuangalia ubora wa huduma zinazotolewa kulingana na muongozo wa taifa wa huduma za tiba. Ukaguzi huo uligundua kuwa huduma, kiwango cha elimu cha wafanyakazi na uwezo wao katika utowaji huduma zinarithisha.

Mhe. Spika, Ili kuongeza uelewa juu ya Ukimwi, kifua kikuu na ukoma kwa jamii na kuongeza ufanisi wa utoaji huduma, Elimu ya afya juu ya Kifua kikuu na Ukoma ilitolewa kwa njia ya redio na mikutano ya kijamii katika vijiji na maeneo tofauti vikiwemo Kizimkazi Mkunguni, Kambodia, Jang'ombe Urusi na Mtoni. Aidha, vipeperushi kuhusiana na maradhi hayo vilitolewa.

Mhe. Spika, Mafunzo kwa wafanyakazi 90 kuhusu kuzuia maambukizi ya maradhi (IPC), umuhimu wa kutumia dawa chini ya uangalizi (DOTS) pamoja na uhusiano wa Kifua Kikuu na Ukimwi yalitolewa. Isitoshe, mafunzo kwa waganga wa kienyeji na wahudumu wa maduka ya dawa, juu ya dalili za kifua kikuu ili kuweza kuwapa rufaa washukiwa kwenda vituo vinavyochunguza maradhi hayo yalifanyika kwa kushirikiana na Shirika la PATH Tanzania. Vile vile elimu ya afya kuhusu Kifua Kikuu imetolewa katika skuli za Nyerere, Mwembeladu na Shauri moyo.

Mhe. Spika, huduma za wagonjwa majumbani ziliendelea, ambapo jumla ya nyumba - 43 walizotoka wagonjwa wa kifua kikuu, na nyumba sita za wagonjwa wa maradhi ya ukoma zilitembelewa, na kutoa elimu kwa jamaa 210 wa wagonjwa na kuchunguzwa afya zao. Kati yao mtu mmoja alionekana na maradhi hayo na kutibiwa, vile vile watoto 9 chini ya umri wa miaka mitano wanaoishi na wagonjwa wa maradhi ya kifua kuu (*contacts*) walipatiwa dawa za kinga. Pamoja na hayo, jozi 42 za viatu maalumu zilitolewa kwa wagonjwa wa ukoma.

Mhe. Spika, kitengo kiliwachunguza watu 1,030 kwa kutumia maabara za Unguja na Pemba, kati yao watu 96 sawa na asilimia 9.3 walionekana na maradhi ya Kifua kikuu na kupatiwa matibabu.

Mhe. Spika, katika kipindi hiki wagonjwa 387 wa kifua kuu walishauriwa kupimwa maambukizi ya virusi vinavyosababisha Ukimwi. Kati yao 343 walikubali kupimwa, na kati ya hao waliopimwa 57 (27 ni wanawake na 30 ni wanaume) walionekana kuwa na matatizo yote mawili (Kifua kikuu na Ukimwi). Vile vile wagonjwa 73 waligunduliwa na ugonjwa wa Ukoma.

Mhe. Spika, Mafunzo kwa watoa huduma za afya yalitolewa juu ya Ushauri nasaha na uchunguzi kwa wagonjwa waliolazwa na wanaotibiwa katika vituo vya afya na hospitali (PITC), Utumiaji wa dawa za kupunguza makali ya virusi vya Ukimwi (ARVs), tiba kwa watoto wenye Ukimwi, ufuatiliaji wa matumizi sahihi wa dawa za ARVs (*Adherence Counseling*), Lishe bora kwa wanaotumia dawa za ARVs.

Mhe. Spika, sambamba na hayo jumla ya watu 51,861 walichunguzwa ili kujua kama wana maambukizi ya VVU, kati yao 930 (1.8%) waligundulika kuwa na maambukizi. Halkadhalika sampuli 2,084 zilichunguzwa vipimo vya CD4 kutoka vituo 9 vinavyotoa huduma za maabara kwa wagonjwa wanaotumia dawa za ARV. Vile vile Sampuli 7,436 za damu zilichunguzwa kwa ajili ya ufuatiliaji wa wagonjwa ambao wameshaanza kutumia dawa za ARV ili kuangalia kama hazina madhara katika miili yao.

Mhe. Spika, kliniki mbili mpya za tiba dhidi ya Ukimwi zimeongezwa katika hospitali za Makunduchi kwa Unguja na Mkoani kwa Pemba. Hii imefanya jumla ya kliniki kufikia 10 (6-Unguja na 4-Pemba) zinazotoa huduma za tiba kwa wanaoishi na VVU na UKIMWI. Hadi kufikia mwezi wa Machi 2012, watu wanaoishi na virusi 6,175 wameshasajiliwa kwenye kliniki hizo. Miongoni mwao wagonjwa 3,348 (54%) wanatumia dawa za ARV, kati ya hao 332 (10%) ni watoto.

Mhe. Spika, hadi sasa Zanzibar kuna jumla ya vituo 56 vinavyotoa huduma za Ushauri nasaha na kupima kwa hiari (Unguja 40 na Pemba 16) vikiwemo vituo 41 vya Serikali, vituo 5 vya hospitali binafsi na vituo 7 vya asasi zisizo za Serikali (NGOs). Katika kipindi cha mwaka 2011, jumla ya watu 87,306 (wanawake 42,360 na wanaume 44,946) walichunguzwa katika vituo hivyo pamoja na vituo vya dharura (Outreach). Kati ya idadi hio watu 1,774 (2.0%) waligundulika kuwa wanaishi na VVU (wanawake ni 1,090 na wanaume ni 684).

Mhe. Spika, maelezo yaliyotangulia juu ya maradhi ya Ukimwi, hayatoi matumaini. Inaonekana kuwa pamoja na juhudi zote zinazofanyika na serikali, bado maradahi haya ni tishio kwa jamii, na kuna haja kwa wananchi kuwa na hadhari zaidi kwani badala ya kupungua yanaonekana kuongezeka zaidi.

Mhe. Spika, katika kufanikisha malengo yake kwa mwaka 2012/2013 mradi umepanga kutekeleza kazi kuu zifuatazo:-

- a) Kuendelea kuimarisha tiba na ushauri kwa kuwapatia dawa za kupunguza makali dhidi ya VVU, Kifua kikuu na Ukoma bila malipo kwa wananchi wote wanaostahiki
- b) Kusimamia, kufuatilia na kutathmini kazi za mradi shirikishi wa Ukimwi, kifua kikuu na Ukoma
- c) Kusimamia upatikanaji na utumiaji sahihi wa vifaa na mahitaji muhimu ya uchunguzi wa huduma za Ukimwi, kifua kikuu na ukoma
- d) Kuongeza uelewa juu ya Ukimwi, kifua kikuu na ukoma kwa wafanyakazi wa afya na jamii kwa kutumia mbinu na mikakati mbali mbali
- e) Kutathmini mwenendo wa maambukizo ya Ukimwi, Kifua kikuu na Ukoma katika makundi mbali mbali
- f) Kuanzisha huduma ya chanjo ya kujikinga na maambukizi ya homa ya ini (aina ya Hepatitis B vaccine) kwa makundi hatarishi, wanaochangia damu na wafanyakazi wa afya
- g) Kuanzisha huduma mbadala ya kuwapatia dawa za kupunguza hali ya uraibu na utegemezi wa madawa ya kulevya wateja 200 (*Methadone Assisted Therapy*) kwa wanaojidunga sindano, ili kupunguza kasi ya maambukizi ya VVU.
- h) Kulifanyia kazi pendekezo la Shirika la Afya Duniani la kupunguza maambukizo mapya ya VVU lenye ujumbe wa kutumia dawa za ARVs kama ni kinga kwa kuufanyia marekebisho muongozo wa tiba kwa wanaoishi na VVU

Mradi wa Kusomesha Madaktari

Mhe. Spika, upungufu wa wafanyakazi na hasa madakatari ni tatizo kubwa. Katika kukabiliana na tatizo hilo wizara imeendelea kusimamia shughuli za mafunzo katika chuo chake cha madaktari ambacho kinaendeshwa na walimu kutoka Cuba. Hadi hivi sasa chuo hiki kina wanafunzi 38 Unguja na 12 kwa upande wa Pemba. Tokea kuanzishwa kwake chuo hichi kimekuwa kikiendeshwa kwa gharama za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar pekee.

Mhe. Spika, Mazingira mazuri ya kusoma na kusomeshea yameimarishwa pamoja na kukifanyia ukarabati chumba cha kompyuta na kununua samani kwa ajili ya matumizi ya chumba hicho. Vile vile mfumo mzima wa internet umesawazishwa. Aidha, vitendea kazi bora vilinunuliwa chini ya ufadhili wa *Italian Corporation* na kuwapatia wanafunzi na walimu wao mashine za kupimia Presha na vifaa vya kupimia moyo na mapafu (*Stetothoscope*).

Mhe. Spika, katika kufanikisha malengo yake kwa mwaka 2012/2013 mradi umepanga kutekeleza kazi kuu zifuatazo:-

- a) Kukamilisha taratibu za kukifanya chuo kitambulike na taasisi ya Elimu ya juu Tanzania
- b) Kufuatilia upatikanaji wa miundombinu bora ya utekelezaji wa shuhuli za chuo
- c) Kusajili madaktari wazalendo wengi zaidi na wenye sifa
- d) Kuongeza idadi ya ziara (*field visits*) za madaktari za kuwatibu wananchi kwenye sehemu zisizofikika kirahisi (*hard to reach areas*) angalau kufikia maeneo mawili kwa mwaka katika kila wilaya

Mradi wa Kupandisha Daraja Hospitali za Vijiji Kuwa za Wilaya

Mhe. Spika, mradi huu una jukumu la kuzipandisha hadhi hospitali za vijiji za makunduchi, Kivunge, Micheweni na Vitongoji kuwa za Wilaya na Hospitali za Abdalla Mzee na Wete, kuwa za Mikoa. Katika kuzipandisha daraja hospitali hizo kunahitajika kuongezeka kwa baadhi ya majengo, vifaa na vitendea kazi. Wizara tayari imefanya makisio ya awali yagharima halisi za kuzipandisha daraja hospitali hizi.

Mhe. Spika, Zoezi la kupima maeneo yote ya hospitali hizo ili kupata hati miliki za maeneo hayo lilifanyika. Aidha, wizara baada ya kujua mipaka ya hospitali zake imeanza kujenga ukuta katika hospitali ya Kivunge, na hili litaendelea katika hospitali zote za vijiji Unguja na Pemba kwa kipindi cha mwaka ujao wa fedha (2012/2013).

Mhe. Spika, miongoni mwa mafanikio yaliyopatikana katika kuipadilisha hadhi hospitali ya wete ni kumalizika kujengwa maabara pamoja na sehemu ya kuwatibu na kuwahudumia wagonjwa wa ukimwi (*Care and Treatment Centre - CTC*), ujenzi wa jengo maalum la wagonjwa wa akili (*mental wing*) na kitengo cha kujifunza kazi wagonjwa wa akili waliopata nafuu (*occupational therapy*).

Mhe. Spika, Ujenzi wa mitambo ya kuchomea taka taka unaendelea vizuri katika hospitali zote za vijiji isipokuwa kwa hospitali ya Makunduchi ambao unahitaji matengenezo madogo yanayotegemewa kufanyika mapema mwaka wa fedha ujao.

Mhe. Spika, katika kufanikisha malengo yake kwa mwaka 2012/2013 mradi umepanga kutekeleza kazi kuu zifuatazo:-

- a) Kufanya matengenezo na utanuzi wa majengo ya Hospitali ya Kivunge na Micheweni, matengenezo haya yatajumuisha wodi ya watoto na Maabara za hospitali hizo
- b) Ununuzi wa vifaa mbali mbali kwa ajili ya kuongeza huduma katika Hospitali hizo
- c) Kufanya matengenezo ya nyumba za wafanyakazi wa hospitali

Mradi wa Mabadiliko ya Sekta ya Afya

Mhe. Spika, Mradi wa Mabadiliko ya Sekta ya Afya una lengo la kuratibu utekelezaji wa Sera ya Afya, kutengeneza miongozo mbali mbali ili iweze kutumika katika sekta ya afya, pia unahusika na utengenezaji na usimamizi wa utekelezaji wa Mpango Mkakati wa Wizara.

Mhe. Spika, Idara imeanza kutayarisha mpango mkakati mpya baada ya mapitio ya Sera ya Afya kukamilika nakukubalika na Serikali. Pia Idara imekamilisha utayarishaji wa muongozo wa kufanya tathmini ya utekelezaji wa kazi utakaotumika katika hospitali za Wilaya na hospitali za vijiji (*Performance assessment tool*). Sambamba na hilo Idara pia imefanikiwa kutayarisha hadidu reja (*Terms of Reference ToR*) za utayarishaji Mpango Mkakati wa Maradhi yasioambukizwa (NCDs).

Mhe. Spika, ripoti ya awali ya mapitio ya matumizi ya fedha katika Sekta ya afya kwa mwaka 2010/2011 (*Public Expenditure Review*) imekamilika na tayari imewasilishwa kwa wizara ili kuweza kujiweka mikakati ya fedha kwa mwaka wa fedha 2012/2013.

Mhe. Spika, mradi umefanikiwa kuratibu mkutano wa sita wa Mapitio wa Sekta ya afya (*6th Annual Joint Health Sector Review Meeting*), wenye kazi ya kutathmini utekelezaji wa mpango kazi wa mwaka 2010/2011 kwa kuangalia mafanikio na changamoto zinazoikabili sekta.

Mhe. Spika, katika kufanikisha malengo yake kwa mwaka 2012/2013 mradi umepanga kutekeleza kazi kuu zifuatazo:-

- a) Kufanya mikutano minne juu ya uelimishaji wa Sera ya Afya kwa wafanyakazi wa wizara ya afya Unguja na Pemba
- b) Kutayarisha muongozo wa rufaa (*Referral guideline*) na kuutambilisha kwa watendaji wa vituo na hospitali za Unguja na Pemba
- c) Kutayarisha muongozo wa mashirikiano baina ya sekta binafsi na sekta ya umma (*Public Private Partnership guideline*)
- d) Kuwapa mafunzo ya utendaji kazi wafanyakazi wapya walioajiriwa katika Hospitali na vituo vya afya
- e) Kufanya mkutano wa siku nne kwa wadau juu ya Mpango Mkakati wa Wizara ya Afya (*Health Sector Strategic plan III*)
- f) Kuandaa mkutano wa saba wa mapitio ya sekta ya afya utakaowashirikisha wadau mbali mbali (*7th Annual Health Sector Review Meetig*)

Mradi wa Kuimarisha Huduma ya Afya ya Akili

Mhe. Spika, lengo la mradi huu ni kuimarisha huduma za afya ya akili Zanzibar, ikiwemo kusimamia afya na ustawi wa watu wenye matatizo ya afya ya akili.

Mhe. Spika, Huduma za vijijini (*Out-reach Services*) ziliendelea kutolewa kwa wilaya zote ili kuwaondoshea usumbufu watu wenye matatizo hayo. Katika kipindi cha July 2011 hadi Machi, 2012 jumla ya wagonjwa 950 (Wanawake 537 na Wanaume 413) waliopatiwa huduma katika vijijini mbali mbali vya Unguja na Pemba.

Mhe. Spika, mafunzo ya siku tano wafanyakazi 22 wa Hospitali za Wete, Chakechake, Abdalla Mzee, Vitongoji na Micheweni, wenye kutoa huduma za afya ya akili yalifanyika. Kwa upande wa Unguja mafunzo hayo yalitolewa kwa watoa huduma za mama na mtoto katika vituo vya afya ya msingi 16 na hospitali za Kivunge, Makunduchi, Mnazimmoja na Hospitali ya wagonjwa wa akili. Vile vile mafunzo ya siku moja kwa waganga wa jadi 25 kutoka Wilaya ya Mjini na Magharibi yalifanyika. Sambamba na hilo watendaji wawili wa huduma za afya ya akili wanaendelea na mafunzo nchini Cuba na Tanzania Bara.

Mhe. Spika, Wizara imeweza kufanya matengenezo ya jingo la wodi nambari moja na mbili la wanaume katika hospitali ya wagonjwa wa akili Kidongo Chekundu. Vile vile ujenzi wa jiko na jengo la litakalotumika kwa shughuli za utawala na matibabu wagonjwa wan je (OPD) umekamilika.

Mradi wa ujenzi wa Bohari Kuu ya Dawa

Mhe. Spika, Mradi una lengo la kuwa na ghala kubwa na la kisasa ambalo litakuwa na Uwezo mkubwa na la kisasa kwa kuhifadhi dawa kwa ajili ya hospitali na vituo vya Afya Unguja na Pemba, pamoja na kuboresha huduma za usambazaji dawa hizo.

Mhe. Spika, katika kuhakikisha upatikanaji bora wa huduma wizara inaendelea na ujenzi wa Bohari kuu ya dawa hapo Maruhubi na kwa sasa uko katika hatua ya kumalizika. Jumla ya Tsh. 278,397,000/= kutoka SMZ zilitengwa na hadi kufikia Machi 2012 jumla ya Tsh. 265,717,000 zimeshatolewa sawa na asilimia 95, ambazo zilitumika kwa ajili ya malipo ya umeme, maji, ununuzi wa fanicha na ujenzi wa kantini katika bohari hiyo. Bohari ya dawa imejengwa kwa msaada wa USAID na DANIDA kwa thamani ya dola za kimarekani 1,200,000.00 Wizara inatarajia kukabidhiwa rasmi jengo hilo mnamo mwisho wa mwezi wa Julai 2012.

Mhe. Spika, katika kufanikisha malengo yake kwa mwaka 2012/2013 mradi umepanga kutekeleza kazi kubwa ya ununuzi wa vifaa vya kutendea kazi pamoja na samani za afisi.

Mradi wa ujenzi wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali

Mhe. Spika, mradi huu umeanza mwaka 2011, ukiwa na lengo la kujenga maabara kubwa na ya kisasa ambayo itawezesha kutoa huduma za uchunguzi kitaalam kwa sampuli mbali mbali kwa ufanisi unaotakiwa.

Mhe. Spika, jengo hili linajengwa katika maeneo yaliyokuwa kiwanda cha sigara Maruhubi, na hatua za ujenzi huo tayari zimeshaanza na zinaendelea vizuri Jumla ya Tsh. 121,684,000.00 zilitengwa kutoka SMZ na hadi kufikia Machi 2012 jumla ya Tsh. 50,000,000.00 zimetolewa ikiwa ni sawa na asilimia 41 tu.

Mhe. Spika, katika kufanikisha malengo yake kwa mwaka 2012/2013 mradi umepanga kutekeleza kazi kuu zifuatazo:-

- a) Kuendelea na ujenzi wa jengo jipya la maabara ya kisasa
- b) Kununua vifaa vya kisasa vya kufanyia uchunguzi
- c) Kuwapatia mafunzo ya kitaalamu wachunguzi wa maabara kwa ajili ya kuimarisha huduma zake

Mradi wa Kuipandisha Hadhi Hospitali ya Mnazi Mmoja Kuwa ya Rufaa

Mhe. Spika, mradi huu ulianza mwaka 2011. Lengo kuu la mradi ni kuimarisha miundombinu ya kiafya kwa kuongeza upatikanaji wa huduma katika hospitali hii zikiwemo za mama na mtoto na uhakika wa huduma za upasuaji.

Mhe. Spika, hatua za awali zimeshachukuliwa ikiwemo kutayarishwa kwa michoro kwa ajili ya ujenzi wa jengo la ghorofa tatu katika jengo lililokua la kiwanda cha madawa. Aidha, ukarabati wa maabara ya hospitali hii ulifanyika na sasa vipimo vingi vinafanyika katika maabara hiyo. Pia ununuzi wa vifaa kwa ajili ya matengenezo ya ICU na kitengo cha meno ulifanyika, na sasa vimeshaanza kutumika.

Mhe. Spika, katika kufanikisha malengo yake kwa mwaka 2012/2013 mradi umepanga kutekeleza kazi kuu zifuatazo:-

- a) Matayarisho ya nyaraka za zabuni za ujenzi (*Tender Documents*) kwa ajili ya utanuzi wa hospitali kupitia mradi wa ORIO
- b) Ununuzi wa tanuri kubwa la kuchomea taka taka za hospitali (*incinerator*)
- c) Kuanzisha kitengo cha huduma za maradhi ya mafigo (*dialysis*)

Mhe. Spika, mbali ya kutekeleza miradi hiyo, wizara kwa mwaka wa fedha 2012/2013 itatekeleza miradi mipya miwili ambayo ni:-

- a) Mradi wa kuimarisha huduma za afya Wilayani (*Busket fund*)
- b) Mradi wa kustawisha siha za Wazanzibari

Mhe. Spika, ili miradi hii iweze kutekeleza malengo yake kwa mwaka 2012/13 Wizara ya Afya inaomba kuidhinishwa jumla ya Tsh. 21,982,205,000.00 kati ya hizo mchango wa Serikali Tsh. 2,731,600,000.00, Ruzuku kutoka kwa washirika wa maendeleo ni Tsh. 16,889,112,000.00 na mkopo ni Tsh. 2,361,493,000.00.

CHANGAMOTO

Mhe. Spika, pamoja na mafanikio mazuri yaliyopatikana, wizara inakabiliwa na changamoto kadhaa katika utekelezaji wa majukumu yake. Sera ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni kutoa huduma zote za afya bila malipo. Hili ni jukumu kubwa la serikali na kwa miaka takriban 50 limekua likitekelezwa hatua kwa hatua. Katika

kutekeleza lengo hilo, Sera ya Afya inatuagiza kutoa huduma ya afya iliyo **sawa kwa wote, iliyo bora, yenye kupatikana na yenye gharama nafuu. Kwa lugha ya kingereza, “equitable, of good quality, accessible and affordable to an ordinary mwananchi”**. Hata hivyo utekelezaji wake umeendelea kuzaa changamoto kadhaa zikiwemo upungufu wa wafanyakazi, ongezeko la vituo vya afya kuzidi uwezo wa kuvihudumia na kuibuka kwa maradhi mapya.

Upungufu wa Wafanyakazi Wataalamu

Mhe. Spika, moja ya sababu zinazopelekea upungufu wa wafanyakazi ni muda na gharama kubwa ya kuwasomesha madaktari. Kwa wastani mafunzo ya daktari huchukua muda wa miaka 5 hadi saba kutegemena na chuo alichosomea. Gharama za mafunzo kwa miaka mitano si chini ya Tsh. 70,000,000.00 kwa wale wanaosoma ndani ya Tanzania, na inakuwa kubwa zaidi ikiwa mafunzo hayo yatakua nje ya Tanzania.

Mhe. Spika, sababu nyengine inayopelekea uhaba huo ni malalamiko ya maslahi duni ya wafanyakazi ambayo kwa kiasi kikubwa husababishwa na mazingira magumu ya kufanyia kazi; yakiwemo upungufu pamoja na uchakavu wa vifaa, kutokuwepo kwa mfumo wa kuwaendeleza wafanyakazi kimaslahi na kiutaalamu, upungufu wa sehemu za makaazi hasa katika hospitali zilizoko vijijini, pamoja na kutozingatia malipo ya wafanyakazi baada ya saa za kazi au wanapoitwa kwa dharura. Hali hii inawapelekea wafanyakazi kujihisi kuwa hawatoi huduma kama zinavyotakiwa na huchangia kwa kiasi kikubwa kuwa na mkanganyiko wa mawazo.

Mhe. Spika, kama nilivyoieleza hapo juu, gharama za kuwasomesha madaktari ni kubwa mno na hupelekea Wizara kupokea wastani wa madaktari 4 tu kila mwaka. Lakini uhakika wa kubaki na kuendelea kutoa huduma kwa wananchi si wa kutegemea sana kulingana na sababu nilizoieleza hapo juu. Jambo la kusikitisha zaidi madaktari bingwa ambao ni wachache ndio wanaoongoza kwa kuodoka nchini. Isitoshe, wale ambao wameamua kubakia wanazeeke na wanashindwa kukabili kazi kwa ufanisi kama walipokua vijana. Tukiwaenzi wafanya kazi wa afya wale walioko nje ya Zanzibar watakata moyo kurudi kwao kushirikiana na Serikali yao kujenga taifa lao la Zanzibar mpya.

Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, haijakaa kimya katika kulipatia ufumbuzi tatizo hili, kwani kuanzishwa kwa Chuo cha Madaktari Zanzibar, ni moja kati ya jitihada za kukabili uchache huo, kwa malengo ya kupata madaktari wengi na kwa wakati mmoja. Pia Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora imekubali kujielekeza katika kulisaidia suala la maslahi na stahiki za wafanyakazi wa sekta ya afya kuanzia mwaka huu wa fedha kwa kasi zaidi. Kwa nia ya kulipatia ufumbuzi wa kudumu suala hili, Wizara ya Afya imeunda kamati ya wataalam wenye kuwakilisha kila kundi la kada ya sekta hii, ili kufanya mapendekezo ya maslahi stahiki na hatimae tuyafikishe Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala bora kwa mazingatio na kutolewa ufumbuzi.

Ongezeko la Vituo vya Afya Kuzidi Uwezo wa Kuvihudumia

Mhe. Spika, changamoto nyingine ya Wizara ya afya ni kuwa na vituo vingi vya afya ambavyo vinaupungufu wa wafanyakazi, vifaa na nyumba za wafanyakazi. Serikali ina vituo vya afya vya kutosha (134) katika umbali kati ya kituo na kituo ulio chini ya kilo mita tano. Zaidi ya vituo hivi, kuna vituo na zahanati za watu binafsi 71 Unguja na Pemba. Kwa mfano, wakati Kibweni kuna hospitali ya KMKM, Bububu kijijini kuna kituo cha afya cha Serikali na kwenye kambi ya Jeshi la wananchi hapo Bububu kuna hospitali ya Jeshi. Hospitali hizi na vituo vyote vinawahudumia wananchi wa Bububu. Kwa hivyo Zanzibar hatuna upungufu wa hospitali isipokua katika maeneo machache yenye ugumu wa kufikika. Sasa, naomba kutumia fursa hii kuwaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, pamoja na Viongozi wengine kujihusisha zaidi katika kujenga nyumba za wafanyakazi na vifaa vya kufanyia kazi, badala ya kufikiria kujenga vituo vipya vya afya.

Kupiga Vita Maradhi Mapya Yanayoibuka

Mhe. Spika, changamoto ya tatu inayoikabili sekta ya afya Zanzibar ni ongezeko la maradhi yanayoambukiza na yasiyoambukiza. Maradhi haya ni pamoja na Shinikizo la damu, Kisukari, maradhi ya moyo, VVU/Ukimwi pamoja na matatizo ya afya ya akili yanayosababishwa kwa kiasi kikubwa na utumiaji wa dawa za kulevya. Maradhi haya yanahusishwa na sababu anuwai na baadhi yake zinaegemea zaidi na mabadiliko ya mfumo wa maisha ya mwanadamu. Hali hii ya kuongezeka kwa maradhi yasiyokua ya kuambukiza kunailazimisha serikali kutumia fedha nyingi sana kwa kuwapeleka wagonjwa wetu nje ya nchi kufuata matibabu. Gharama hii ni kubwa, lakini hakuna bei ya uhai na hivyo serikali inawajibika kugharimia matibabu haya. Nilishaeleza huko awali ya hotuba hii kwamba,

kwa mwaka wa 2010/11 Serikali ilitumia Tsh. 906,295,038 na mwaka huu hadi Machi Tsh. 616,091,417 zimeshatumika.

Mhe. Spika, nimelazimika kutumia muda wako mkubwa kueleza changamoto na nini tunakusudia kufanya katika kukabili changamoto hizo kwa sababu ya umuhimu wa huduma za afya kwa jamii. Kasma ya Serikali kwa Sekta ya Afya imeendelea kuwa ndogo kutokana na sababu nyingi ikiwemo hali ya uchumi, ongezeko la watu pamoja mwenendo wa kasi ya ongezeko la maradhi. Nawaomba wale wote walio na uwezo wa kutusaidia katika nyanja hizo nilizozitaja waje kuonana na Wizara ili tushirikiane katika kutimiza wajibu wetu.

MALENGO YA WIZARA KWA MWAKA 2012 - 2013

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo wizara ya afya kwa mwaka 2012/13 itajielekeza kufikia malengo yafuatayo:-

- a) Kujenga jengo la ghorofa moja la ofisi ya Mradi Shirikishi wa mama na mtoto
- b) Kujenga wodi ya mama wajawazito katika hospitali ya Wete
- c) Kukamilisha uandaaji wa mfumo wa malipo ya mishahara na maslahi ya wafanyakazi pamoja na utaratibu wa upandishwaji vyeo
- d) Kukamilisha maandalizi ya kuzifikisha sheria za Afya ya Jamii na ya Wataalamu wa Afya Mazingira katika Baraza la Wawakilishi na kusimamia utekelezaji wake
- e) Kufanya uchambuzi wa mahitaji ya kifedha wa kila huduma ya afya inayotolewa
- f) Kukamilisha matayarisho ya mpango wa mahitaji na mafunzo ya wafanyakazi wa Sekta ya Afya
- g) Kuimarisha utoaji wa elimu ya afya kwa jamii ikiwemo kuanzisha redio maalum "Afya FM Redio"

HITIMISHO

Mhe. Spika, Maendeleo yaliyopatikana katika utekelezaji wa malengo na majukumu ya wizara yalitegemea kwa kiasi kikubwa juhudi na maarifa ya watendaji ndani ya Wizara, michango, maelekezo na ufuatiliaji wa utekelezaji wa majukumu ya Wizara kutoka kwa viongozi wakuu wa Serikali, wajumbe wa Baraza lako tukufu na wadau wengine wa afya.

Mhe. Spika, utaratibu aliojiwekea Mhe: Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kukutana na mawizara kila baada ya miezi mitatu ulisaidia sana kuchangamsha wizara yangu na kuifanya kuwa macho wakati wote kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Tunaupongeza utaratibu huu na tunapenda uendeleo.

Mhe. Spika, wajumbe wa Baraza lako wamekuwa mstari wa mbele kuchangia na kufuatilia aidha mmoja mmoja au kupitia kamati maalum utekelezaji wa wizara yangu. Nawashukuru wote na ninawaomba waendeleo na utaratibu huo.

Mhe. Spika, nichukuwe nafasi hii pia kuwashukuru viongozi wote na wafanyakazi wa wizara ya Afya kwa mashirikiano walioyaonesha wakati wote kwa kuniwezesha kusimamia majukumu yangu kwa wepesi, nategemea mashirikiano ya aina hiyo yataendelea kwa miaka mingi ijayo.

Mhe. Spika, nitakuwa sikufanya haki ikiwa sikuwashukuru wananchi wa Zanzibar kwa kuwa pamoja nasi wakati wote na kutupa mashirikiano mazuri muda wote. Sinabudi pia kuzishukuru taasisi nyengine za serikali na zisizozaserikali kwa mchango wao mkubwa wanaoutoa katika suala zima la utoaji wa huduma za afya.

Mhe. Spika, msukumo mkubwa umeendelea kutolewa na mashirika ya kitaifa na kimataifa, pamoja na nchi marafiki. Msukumo huo wa hali na mali umesaidia kutoa huduma bora kwa wananchi. Nachukuwa fursa hii adhimu kuwashukuru wote hasa Benki ya Maendeleo ya Afrika (ADB), WHO, UNICEF, UNDP, JICA, Jhpiego, HIPZ, CLINTON FOUNDATION, GLOBAL FUND, WORL BANK, DANIDA, ITALIAN FOUNDATION, SAVE THE CHILDREN, IVODE CARNERI, Pia shukrani ziende kwa nchi marafiki za India, Israel, Cuba, Marekani, Italy, Nertharland, Ufaransa, Belgium, China, Misri, Oman, Turkey na wale wote ambao sikuwataja katika orodha huu.

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Kazi za Kawaida na Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013.

Mhe. Spika, Wizara yangu inajukumu la kuchangia mfuko mkuu wa Serikali kutokana na vyanzo mbali mbali vya mapato vilio ndani ya wizara yangu. Kwa mwaka wa fedha (2011/2012), Wizara ilipangiwa kuchangia Tsh.

537,000,000.00 ambapo kufikia Machi 2012, jumla ya Tsh. 217,487,334.00 sawa na asilimia 40% zimesakusanywa. Kwa mwaka ujao wa (2012/2013) Wizara ya Afya imepangiwa kuchangia milioni mia tisa na ziada hii hapa (Tsh. 805,500,000.00) imekosewa.

Mhe. Spika, kwa mwaka 2012/2013 Wizara yangu imepangiwa kutumia jumla ya Tsh. 18,234,000,000.00 ikiwa ni Tsh. 4,502,920,000.00 kwa kazi za kawaida (OC), Tsh. 13,731,080,000.00 kwa ajili ya mishahara na maposho. Pia Wizara imepangiwa kutumia jumla ya Tsh. 21,982,205,000.00 kwa kazi za maendeleo, kati ya hizo mchango wa Serikali ni Tsh. 2,731,600,000.00, Ruzuku kutoka kwa washirika wa maendeleo ni Tsh. 16,889,112,000.00 na mkopo ni Tsh. 2,361,493,000.00.

Mhe. Spika, mategemeo yangu wajumbe wa Baraza lako wameipokea hotuba hii, watajadili kwa kina na watatoa michango yao kwa madhumuni ya kuiwezesha wizara yangu kupata mafanikio makubwa katika kutekeleza majukumu yake. Wizara yangu itaipokea michango yote itakayotolewa na kuifanyia kazi kama inayostahili kwa faida ya nchi yetu.

Mhe. Spika, baada ya hayo naliomba baraza lako tukufu kuidhinisha jumla ya Tsh. 40,216,205,000.00 kwa matumizi yake yote kwa mwaka 2012/2013.

Mhe. Spika, kwa heshima na taadhima na uvumilivu mkubwa ulionistahamia naomba kutoa hoja.

Mhe. Spika: Niwashukuru Waheshimiwa Wajumbe, na namshukuru sana Mhe. Waziri. Waheshimiwa Wajumbe leo nimefurahi sana mmekuwa wasikivu muda wote mko ndani, ni heshima kubwa kwa wananchi wetu waliotuleta humu ndani, kuona kwamba tunakuwa tayari kuwafanyia maendeleo yao. Hoja imeungwa mkono hiyo maana yake tuanze kujadili.

(Hoja ilitolewa ijadiliwe)

Mhe. Amina Iddi Mabrouk (Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii): Mhe. Spika, kwanza napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia kusimama mbele ya Baraza lako tukufu nikiwa mzima wa afya, kwa lengo la kuwasilisha maoni ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Afya kwa mwaka wa fedha 2012/2013.

Mhe. Spika, aidha kwa niaba ya kamati napenda kuchukua fursa hii kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja hii ya Wizara ya Afya kuhusu mapendekezo ya bajeti ya wizara yake.

Mhe. Spika, pia napenda nimshukuru Waziri, Naibu Waziri, pamoja na watendaji wa Wizara ya Afya kwa kuwasilisha mbele ya kamati taarifa ya utekelezaji wa Bajeti ya mwaka 2011/12 na muelekeo wa Bajeti ya wizara kwa mwaka mpya wa fedha 2012/2013.

Mhe. Spika, nawashukuru pia Wajumbe wa Kamati ya Baraza la Wawakilishi ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii, kwa michango yao wakati wa kuijadili na kuichambua kwa kina Bajeti ya Wizara ya Afya, na hatimae kuweza kutoa mapendekezo pamoja na kuishauri serikali. Sasa naomba niwataje Wajumbe kama ifuatavyo:-

- | | |
|-------------------------------|-------------------|
| 1. Mhe. Amina Iddi Mabrouk | Mwenyekiti |
| 2. Mhe. Hijja Hassan Hijja | Makamo Mwenyekiti |
| 3. Mhe. Jaku Hashim Ayoub | Mjumbe |
| 4. Mhe. Asha Abdu Hajji | Mjumbe |
| 5. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa | Mjumbe |
| 6. Mhe. Saleh Nassor Juma | Mjumbe |
| 7. Mhe. Nassor Salim Ali | Mjumbe |
| 8. Mhe. Ashura Sharif Ali | Mjumbe |
| 9. Nd. Talib Enzi Talib | Katibu |
| 10. Nd. Asha Said Mohamed | Katibu |

HALI YA MAPATO

Mhe. Spika, nianze na ukusanyaji wa mapato. Kamati yetu inapata mashaka na haivutiwi hata kidogo na utaratibu wa utoaji wa taarifa za ukusanyaji wa mapato katika Wizara ya Afya. Kutokana na uzoefu, Kamati yetu tuna wasi wasi mkubwa kuwa kuna taarifa za mapato zaidi ya wizara ambazo zinafichwafichwa.

Mhe. Spika, tumeona tueleze hayo kutokana na hali inavyoendelea kujitokeza. Wakati Kamati ilipokaa kupitia Bajeti ya Wizara ya Afya mwaka jana, iligundua kuwepo kwa vyanzo vya mapato zaidi ambayo wizara haikuweza kuviainisha katika kitabu cha Mswada wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali ambapo baada ya kujadiliana, Kamati tuliagiza vyanzo hivyo vya mapato lazima viainishwe katika kitabu hicho na tupatiwe marekebisho yake. Awali jumla ya makusanyo ya mapato yaliyoainishwa yalikuwa ni shilingi milioni 52, na baada ya kuingizwa vyanzo vyengine ambavyo Kamati ilivyovibaini. Makisio ya makusanyo hayo yaliweza kufika jumla ya shilingi milioni 537.

Mhe. Spika, hali kama hiyo imejitokeza tena katika kupitia bajeti ya Wizara ya Afya kwa mwaka huu mpya wa fedha. Jumla ya makisio ya mapato yaliooneshwa awali yalikuwa ni shilingi 805,500,000 ambapo baada Kamati kutaka kuainishwa chanzo kilichoachwa cha mapato yatokanayo na huduma za eneo la *FAST TRACK*, ambalo mwenyewe hatumjui ni nani. Makisio hayo yaliongezeka hadi kufikia shilingi 995,500,000. Kimsingi Kamati yetu imebaini kuwa makusanyo ya huduma za *Fast Track* ni shilingi milioni 190. Mhe. Spika hiyo ndiyo hali halisi.

Mhe. Spika, hali hii hatuipendelei, na kama Kamati, tunatoa indhari kwa wizara, iwapo Kamati katika bajeti zijazo, itabaini na kuthibitisha kuwepo vya vyanzo zaidi vya mapato ambavyo haviainishwi katika Bajeti ya Serikali, basi wahusika lazima wawajibishwe.

IDARA YA MIPANGO, SERA NA UTAFITI

Mhe. Spika, mfumo mzima wa utoaji wa huduma za afya nchini unahitaji sera imara pamoja na sheria zinazotekelezwa ipasavyo. Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii inaipongeza wizara kwa kuona umuhimu wa kufanya mapitio makubwa ya Sera ya Afya ya mwaka 1999. Sera mpya ya afya itatoa wigo mpana zaidi wa utekelezaji wa mikakati na malengo ya wizara pamoja na mabadiliko yanayotokea.

Mhe. Spika, aidha Kamati yangu inaunga mkono wizara ya afya katika juhudi za kuhakikisha kuwa inaimarisha nguvu kaz,i ikiwemo mafunzo katika kada mbali mbali za afya pamoja na kuajiri wafanyakazi wapya katika vituo na hospitali zetu. Hatua hiyo itasaidia kuondokana na tatizo kubwa la uhaba wa wafanyakazi katika Sekta ya Afya.

Hata hivyo, bado kuna changamoto kwa wizara na serikali kwa ujumla ya tishio la kumalizika kwa kada maalum za wataalamu wa afya kutokana na sababu mbali mbali. Hivyo Kamati inaishauri wizara kufikiria kuanzisha miradi ya miundombinu, ili kuweza kulinda rasilimali watu iliyopo na hata kufanya utafiti kubaini mahitaji ya wataalamu wa kada mahsusi ambao kwa kiasi kikubwa hatunao.

Mhe. Spika, ushirikishaji wananchi katika utoaji wa huduma ni jambo muhimu, Kamati yangu inaipongeza wizara kwa kuweza kutayarisha Mpango Mkakati wa Afya ya Jamii (*Community Health Strategy*), ambapo kamati kiongozi za afya za shehia zitakuwa kiungo baina ya wafanyakazi wa afya na wananchi.

UTEKELEZAJI WA MUONGOZO WA UCHANGIAJI WA HUDUMA ZA AFYA.

Mhe. Spika, Kamati yetu inaipongeza wizara kwa kuufanyia marekebisho muongozo wa kuchangia huduma za afya kupitia uzoefu wa nchi mbali mbali zilizoendesha mpango huo. Hatua hiyo imefanya gharama za kuchangia huduma za afya kupangwa upya kulingana na gharama halisi za utoaji wa huduma za afya.

Mhe. Spika, ingawa wizara inakabiliwa na changamoto kwa upande wa msamaha katika uchangiaji huduma za afya, Kamati yetu inampongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kufanya maamuzi ya makusudi kuwaondolea malipo kinamama katika huduma za kujifungua kwa njia ya kawaida na kwa upasuaji.

Kamati yetu Mhe. Spika, inaiagiza Wizara ya Afya kuhakikisha kwa namna zote maamuzi hayo ya Mhe. Rais yanasimamiwa na kutekelezwa kwa vitendo.

Mhe. Spika, wizara ihakikishe kuwa maafisa wa afya wanatekeleza agizo hili kwa mujibu wa maelekezo ya Serikali, kwa vile uzoefu uliokuwepo katika masuala kama hayo, unaonesha kuwa baadhi ya watendaji mara nyingi hukiuka maagizo ya Serikali na kuanza kuwatoza wananchi malipo kinyume na utaratibu.

Tunatoa rai kwamba lazima uandaliwe utaratibu maalum kwa kinamama kutoa taarifa kunakohusika, iwapo atatokezea mgonjwa kutozwa ada ya malipo ya kujifungua.

Mhe. Spika, napenda kuungana na wizara kusisitiza kina mama wajawazito kujenga utamaduni wa kufika kliniki kupima, na vile vile wajifungulie kwenye hospitali ama vituo vya afya vinavyotoa huduma hizo. Kama tatizo lilikuwa ada basi Mhe. Rais amefanya utafiti juu ya kuendelea kuwepo kwa ada hiyo ama ameona kuwa serikali inaweza kusimamia utoaji wa huduma hizo kwa wananchi bila ya malipo.

Mhe. Spika, mbali na hayo, Kamati yetu inaishauri serikali kufanya utafiti ili kuelewa huduma nyengine za matibabu ya afya ambazo kwa asilimia kubwa zinawashinda wananchi wengi, kutokana na ukubwa wa gharama zake, ili serikali nayo itafute namna ya kuwasaidia wananchi ambao wengi ni masikini, na baadhi ya wakati huweza hata kupoteza maisha kutokana na kushindwa kumudu gharama kubwa za matibabu hasa kwa maradhi mazito.

IDARA YA HOSPITALI YA MNAZI MMOJA

Mhe. Spika, kamati yangu imefurahishwa na mpango wa serikali kuanzisha mradi wa kuipandisha hadhi Hospitali ya Mnazi Mmoja na hospitali nyengine za vijiji. Tunaikumbusha wizara kuwa ingawa mpango huo upo na ni wa manufaa, lakini kwa kweli kukamilika kwake ni mpango wa muda mrefu. Changamoto iliyopo ni kwamba baadhi ya hospitali zetu hasa Pemba hali si nzuri, tunaweza kusema hakuna dalili hata za kuanza utekelezaji wa mpango huo, majengo mengi yanahitaji ukarabati angalau wa awali.

Mhe. Spika, kuhusu chumba cha wagonjwa mahututi *ICU* na upasuaji katika Hospitali ya Mnazi Mmoja, kamati inaipongeza Wizara kwa juhudi kubwa zilizofanyika katika kuimarisha huduma katika sehemu hizo. Kwa kweli hivi sasa kuna mabadiliko ukilinganisha na wakati wote tuliokuwa nao, tulipiga kelele kuhusu sehemu hizo. Ukarabati umeanza kwa hatua ya kuwekwa vifaa.

Aidha Mhe. Spika, kamati yetu tunashauri umuhimu wa hospitali za vijiji kujiwekea na kuainishiwa malengo yake mahsusi katika bajeti, ili kamati husika iweze kukagua utekelezaji wake kwa ajili ya manufaa ya wananchi katika sekta hiyo ya afya. Ukiachilia mbali Hospitali ya Magonjwa ya Akili ya Kidongo Chekundu, hakuna hospitali iliyojiwekea malengo mahsusi ya utekelezaji.

BODI YA CHAKULA, DAWA NA VIPODOZI

Mhe. Spika, kamati inapongeza kazi zinazotekelezwa na bodi hii. Aidha, hatua ya Bodi ya Chakula, Dawa na Vipodozi kuandaa kanuni kushajihisha wananchi kutumia chumvi zenye madini joto. Hicho ni kilio cha muda mrefu, la kushangaza kumekuwa na ucheleweshaji wa kutolewa kwa kanuni hizo.

Mhe. Spika, kamati imebaini kuwa hakuna sheria inayowabana wadau wanaozalisha chumvi isiyo salama. Asilimia 58 ya wananchi wanaotumia chumvi isiyo salama ni tatizo kubwa kiafya kwa wananchi wetu.

Mhe. Spika, wizara imekamilisha rasimu ya Sheria ya Lishe kipindi kirefu na kuiwasilisha katika Afisi ya Mwanasheria Mkuu. Tunamuomba Mwanasheria Mkuu atueleze tatizo liko wapi ili haraka hatua zichukuliwe, na wizara iweze kuwa na sheria hiyo. Aidha, kamati inaiagiza Wizara ya Afya kuhakikisha kuwa inaanzisha sheria itakayohakikisha usalama wa Bodi ya Chakula katika kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

MPANGO WA DAMU SALAMA

Mhe. Spika, wizara imeanzisha mpango wa uchangiaji wa damu salama katika maabara maalum iliyoko Sebleni kwa lengo la kuondoa usumbufu wa kutafuta jamaa wa mgonjwa kumchangia damu wakati inapohitajika. Pia kuwezesha kuwepo damu wakati wowote ikiwa tayari imechunguzwa na inakubalika kutumika kwa wagonjwa. Ni hatua ya mafanikio. Ipo haja kwa serikali kuchangia *program* muhimu kama hizi, mpango huu ni vyema uingizwe katika

miradi ya maendeleo. Aidha, kuna haja kwa serikali kuangalia suala la bima kwa matibabu katika hospitali za umma na binafsi, ili kusaidia kufikia lengo la Mpango wa Damu Salama kuweza kujitegemea.

Aidha Mhe Spika, ni muhimu kuimarishwa huduma za Mpango wa Damu Salama kwa upande wa Pemba kwani hali sio nzuri.

KITENGO CHA TAKWIMU, MIENENDO YA MARADHI NA UTAFITI

Mhe. Spika, kitengo hiki kimefanya kazi kubwa na hatimae kuweza kufikia malengo yaliyowekwa kwa ufanisi. Kimeweza kukusanya taarifa za hospitali zote kutoka kila wilaya na kuziingiza katika mpango wa “*data base*”, kukamilisha kitabu cha taarifa za afya, kukamilisha mpango wa kuzieneza taarifa hizo pamoja na muongozo wa sera na mpango mkakati wa mfumo wa taarifa za afya. Kwa kweli kamati inakipongeza. Licha ya mafanikio hayo, kamati imeona kuwa kitengo kina upungufu mkubwa wa wataalamu wenye fani za kuweka kumbukumbu za taarifa za afya.

Aidha, katika baadhi ya hospitali za binafsi kuna tatizo la kutoa taarifa za afya kwa ujumla, matokeo yake utumiaji wa taarifa za serikali pekee huweza kuwa na kasoro na kupelekea kuchelewa kukamilisha uandaaji wa mipango ya maendeleo katika sekta ya afya. Wizara ni vyema kulisimamia suala hilo.

MRADI WA UJENZI WA BOHARI KUU YA DAWA NA AFISI YA MKEMIA MKUU WA SERIKALI ZANZIBAR

Mhe. Spika, kamati imeridhika na hatua ya maendeleo ya Mradi wa ujenzi wa Bohari Kuu ya Dawa Zanzibar chini ya Washirika wa Maendeleo *US AID* na *DANIDA* pamoja na mchango wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Serikali imechangia jumla ya shilingi milioni mia moja kati ya shilingi milioni mia mbili zilizopangwa kutolewa. Kamati inaisisitiza wizara kuendelea kuimarisha ufuatiliaji ili kuhakikisha kuwa ujenzi huo unamalizika kwa wakati kama ilivyokusudiwa.

Hata hivyo, kamati yetu inaiagiza Wizara ya Afya kuharakisha kuanza ujenzi wa jengo la ofisi za Mkemia Mkuu wa Serikali ili chombo hicho muhimu kiweze kufanya kazi zake kwa ufanisi.

Aidha, kwa upande wa Pemba kamati yetu imeona kuwa jengo la Bohari Kuu ya Dawa haikidhi haja, mahitaji yanaendelea kuongezeka, ambapo hayawiani na nafasi ya jengo iliyopo. Mhe. Spika, dawa nyingi zenye gharama kubwa zimewekwa chini hali ambayo wakati wowote zinaweza zikaharibika.

MRADI WA KUZUIA MAAMBUKIZI YA UKIMWI

Mhe. Spika, Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii inapongeza juhudi za washirika wa maendeleo katika kuendeleza mapambano ya kuzuia maambukizi ya UKIMWI Zanzibar. Taarifa mbali mbali za takwimu zinaeleza kuwa bado kuna ongezeko la maambukizo ya virusi vya UKIMWI. Elimu zaidi inahitajika kwa jamii ili Zanzibar iweze kukabiliana vyema na janga la UKIMWI. Aidha, kuna haja kwa wizara kuhakikisha kuwa inaendelea miradi itakayosaidia katika mapambano ya kuzuia maambukizi ya UKIMWI nchini.

MRADI WA KUSOMESHA MADAKTARI ZANZIBAR

Mhe. Spika, lengo la mradi huu ni kuendeleza sekta ya afya kwa kuongeza idadi ya wataalamu ili kukabilina na upungufu wa madaktari watabibu Zanzibar. Mradi huu unaendesha mafunzo ya udaktari kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha *Mantasas* cha *Cuba* ambapo wanafunzi 50 wamepata mafunzo hayo.

Mhe. Spika, kamati yetu imesikitishwa na bajeti ndogo ya mradi huu ikilinganishwa na ile ya mwaka jana. Tuna wasiwasi katika utekelezaji wa malengo hasa ukizingatia changamoto za msingi zinazoukabili mradi. Tunaitaka wizara iharakishe kukifanya chuo kitambulike na elimu ya juu pamoja na kusajili wanafunzi wazalendo wenye sifa zinazohitajika. Hata hivyo, tunaipongeza serikali kusimamia mradi muhimu kama huu bila ya mchango wa washirika wa maendeleo.

HITIMISHO

Mhe. Spika, kwa ujumla kumekuwepo na maeneo ya mafanikio katika bajeti ya mwaka jana pamoja na changamoto zinazohitajika kuchukuliwa. Hata hivyo, kamati yangu imeziainisha awali, lakini Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii hairidhiki na ufinyu wa bajeti inayopewa Wizara ya Afya. Asilimia 80 ya bajeti ya wizara inategemea wahisani, ni dhahiri kuwa bajeti hiyo haina uhalisia katika utekelezaji wake bila ya mazingatio ya upangaji wa kibajeti hasa katika sekta ya afya, elimu na ustawi wa watu, tutaendelea kuwasakama roho watendaji bure.

Mhe. Spika, baada ya kutoa maoni ya kamati yangu sasa kwa kuwa kanuni haziniruhusu kuchangia tena bajeti hii, naomba sasa nitoe mchango wangu mdogo unaohusiana na bajeti hii.

Mhe. Spika, kuna madai kwa baadhi ya ma-nurse waliosoma Chuo cha Afya Mweni kwa ngazi ya *diploma*, ma-nurse hawa mpaka leo hawakupatiwa vyeti vyao. Wanafunzi hawa wamesoma katika chuo hicho katika miaka ya 1992 hadi 1995. Mhe. Waziri naomba atapokuja kutoa majumuisho atueleze sababu gani zilizopelekea kukwama kutolewa vyeti hivyo.

Lakini jengine Mhe. Spika, naomba nichukue nafasi hii kwa dhati kabisa kupongeza serikali pamoja na Wizara ya Afya kwa kuifanyia matengenezo mbali mbali *ICU* yetu iliyopo katika Hospitali yetu ya rufaa ya Mnazi Mmoja, kama alivyotueleza Mhe. Waziri wakati alipokuwa anasoma bajeti yake.

Mhe. Spika, pamoja na hayo, wizara iliona ipo haja ya kuwepo kwa *ICU* ya watoto ili kuiondolea mzigo *ICU* kuu iliyopo katika Hospitali ya Mnazi Mmoja. Wizara iliamua kwa makusudi kwa sababu inaonekana kwamba si vyema watoto wetu wadogo kuchanganywa na watu wazima, lakini kama hilo halitoshi watoto wetu hawawezi kumudu baridi ambayo ipo katika *ICU*.

Mhe. Spika, wizara hapo siku za nyuma iliandaa mpango maalum katika hospitali ya watoto ya mabao, na ikatenga chumba kwa ajili ya *ICU* ya watoto, lakini Mhe. Waziri mpango ule ulikwama, sasa namuomba Mhe. Waziri atapokuja atueleze ni kitu gani kilichosababisha mpango ule hadi leo kutotekelezeka.

Mhe. Spika, baada ya hayo machache kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha.

Mhe. Spika: Mwenyekiti tunakushukuru, tumsikilize sasa Mhe. Jaku Hashim Ayoub, kama muda utakuwepo tumsikilize Mhe. Makame Mshimba Mbarouk.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, awali ya yote sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu *Subhanahu Wataallah*, aliyeniwezesha kusimama hapa, na kunipa uwezo wa kuzungumza machache na hivyo kunijaalia pumzi za kupumua kwa muda huu. Kwa neema hizo namshukuru Alhamdulillah.

Vile vile Mhe. Spika, nikushukuru wewe kwa kunipa fursa hii kuweza kunisimamisha hapa na kuzungumza mawili au matatu. Mhe. Spika, nitakuwa sijafanya haki kama sikumpa haki Mhe. Babu Juma Duni Haji, kwa kazi nzuri anayoifanya kwa Hospitali ya Mnazi Mmoja na nyenginezo. Kwanza Mhe. Babu Juma ni muwazi, mkweli na ni waziri wa mwanzo katika kufahamu kwangu mimi, aliyefika hatua ya kutaka kujiuzulu kwa uchungu wa nchi hii kuhusu *ICU*, Babu Juma hongera sana. (*Makofi*).

Mhe. Spika, Babu Juma kafanya hivi kwa sababu ya uchungu wa nchi hii, hakung'ang'ania kuwa anataka madaraka, kafanya kwa uchungu wa kisiwa hiki. Mhe. Spika, baada ya kutoka huko nianze katika Hospitali ya Mnazi Mmoja.

Mhe. Spika, Hospitali ya Mnazi Mmoja imekuwa chafu kupita kiasi. Kwanza tu ukiingia pale kuna shimo karibu miezi sita sasa, Spitali unaingia kwenye geti pale panapotolewa dawa dirishani kuna shimo kubwa, sijui anatuambia nini kuhusu shimo lile, karibu miezi sita sasa liko pale. Wagonjwa wanaopakiwa kwenye vigari vya matairi matatu, vigari vile viko vitatu tu, kutokana na shimo lile inabidi mgonjwa anyanyuliwe na kupelekwa pengine. Mhe. Spika, sehemu ile ya barabara ya kuingilia ndani na kutokea haifai.

Mhe. Spika, nafikiri hapa tuombe msaada wa Waziri anayehusika, angalau pale ni padogo angefanya matengenezo ya kuziba. Kama haikuwezekana hata mimi niko tayari kujitolea kutia japo zege kwa kipande kile. Ukitoka hapo

Mhe. Spika, mkono wa kushoto kuna vitanda vibovu vimewekwa katika hospitali ile ni kitendo cha aibu. Leo sijui ni miezi mingapi vitanda vile vibovu viko pale, ni aibu iliyoje.

Mhe. Spika, ukipanda juu katika sehemu ya *ICU* pana mashimo yamezibuka pale kwenye *corridor* ni hatari vile vile, hasa wakati wa usiku kutokana na sehemu ile wakati mwingine taa haziwaki kwenye ngazi, sijui ni gharama ya kiasi gani inayohitajika pale.

Mhe. Spika, nije katika sehemu za vyoo. Hapa mimi nitahitaji maelezo, vyoo havina milango vile ni aibu iliyoje. Mtu akitaka kwenda haja inabidi amtafute mtu amkamatie kwanza mlango amsubiri baadae akishamaliza ndio aondoke. Vyoo vile nitahitaji maelezo kwa kweli ni vya muda mrefu na haviridhishi.

Mhe. Spika, ukiingia katika kitengo cha *Ultra Sound* ni sehemu chafu kupita kiasi, hilo jaa lina afadhali kuliko mule ndani. Sisemi kwa kubahatisha mimi, na Mhe. Waziri akitoka hapa aende akaangalie mule ndani, muna viboksi vya sindano mule ndani ni hatari. Nimeshakwenda karibu wiki mbili nimevikuta, hata leo asubuhi nimekwenda kuhakikisha nimevikuta Mhe. Spika, maana yake nisije nikasema uongo hapa Barazani vipo. Wananchi pale wanapata shida na kama hakuna bao, basi wawekewe japo magogo ya minazi, wanagaragara chini mama zetu mule ndani, wanaumia vibaya. Huwa wanalipia sio bure huduma hiyo, leo wanateseka pale. Mhe. Spika, yangewekwa japo magogo ya minazi yakawekwa pale angalau wakaweza kukalia wale watu.

Mhe. Spika, magodoro ya wagonjwa hayaridhishi kabisa mule ndani, ni uchafu ulioje. Ile ghala ya yale magodoro sijui ni kiasi gani yanaweza kufika, tuiangalie ile sakafu utafikiri udongo wa Makunduchi ile sakafu yake ilivyo. Ni hali mbaya iliyoje yale mazingira yake mule ndani, kweli ndio tutamsaidia mtu afya yake na halafu leo tunawalaumu wananchi wetu kwenda pale kuangalia wagonjwa. Wananchi wetu hawana makosa, matibabu pale hayaridhishi kabisa, wananchi sasa inabidi wafuatilie mtu pale akaulize kuna kishindo gani ndani, tusiwalaumu wanaokwenda kukaa pale.

Mhe. Spika, mimi niliwaambia wajenge banda angalau la kuwasitiri wale watu. Waswahili wanasema '*shika shika na mwenyewe uko nyuma*'. Sasa unampeleka mgonjwa unamtupa ndani halafu utegemea pana matibabu, pakihitajika kitu ukitafutwa uko wapi. Wale hawana makosa, wao wanachohitajika kusikiliza wagonjwa wao. Pakihitajika kifaa utakipata wapi, ukamtupe tu mgonjwa. Kumezuka tabia kwa baadhi ya *ma-nurse* wetu sasa hivi, baadhi yao hasa katika kile kitengo cha *ICU* wamekuwa jeuri. Juzi mtu anakata roho mimi nipo, akamwita na kumwambia niitie mtu wangu nje, angalau apate kumuusia, anakata roho anamwambia lala tu lala tu, mtu anakufa lala tu, mpaka roho ikamtoka, sio utendaji huo. Sibahatishi hayo Mhe. Spika, nazungumza kwa kuyajua. Mimi huwa nakuwepo pale mpaka usiku pale Mhe. Spika. Nilikuwa nikipiga kelele humu Wajumbe wakawa wanania kama mwendawazimu kuhusu habari ya kuzaa. Mhe. Rais kafika suala hilo kalijua na ukweli ukaonekana.

Mhe. Spika, nije kwenye Hospitali ya Makunduchi, nyumbani kule Mhe. Spika, kitengo kile kinasaidiwa kwa kiasi kikubwa na mfadhili. Lakini watu wa Makunduchi wamekuwa na kilio, lita 180 kwa mwezi mafuta yale hayakidhi kuleta wagonjwa wa rufaa kuja mjini huku, ni wagonjwa 8 au 9 ukifanya hesabu kwa lita 20. Kwa hivyo, hiki kitengo kinahitaji kuongezwa mafuta. Kwenye hospitali ambayo inategemewa kuwa ya rufaa, sijui tutafika lini kwa hali kama hii. Kuna upungufu wa vyombo vya kutilia damu na sehemu ya mkojo.

Vile vile nitakuwa sijawafanyia haki wananchi wa Pemba Mhe. Spika, kama sikuwatendea hapa. Wananchi wa Pemba hivi sasa wana kilio kikubwa sana kuhusu upungufu wa madaktari. Kuna upungufu wa hali ya juu kisiwani Pemba. Leo hospitali mbili tu ndio zinazofanya kazi, ikiwemo Micheweni na Wete. Hospitali ya Mkoani imeharibika na Chake Chake imeharibika sijui tutafika wapi.

Mhe. Spika, nije kwenye kitabu chako hiki cha Wizara ya Afya katika ukurasa wa 107, jamani nisaidieni hapa, kiambatisho nambari 10

Mhe. Spika: Ielekee zaidi *microphone* yako ili Waziri akusikie vizuri.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante Mhe. Spika. Nawaomba Waheshimiwa Wajumbe munisaidie kwenye ukurasa wa 107, hospitali hii kweli tutafikia rufaa kwenye kiambatanisho hiki nambari 10. *General physician* mahitaji halisi moja waliopo ziro, ndio hospitali ya rufaa ambayo tunaitegemea jamani, *Cardiology* mahitaji watatu, waliopo mmoja, upungufu wawili. *Pharmacist* wanne, waliopo mmoja, upungufu watatu. *Nephrology* mahitaji wanne, waliopo ziro, upungufu wanne. *Radiologist* mahitaji sita, aliopo mmoja mapungufu watano. Tunategemea hospitali

ya rufaa hii jamani huko tunakokwenda Mwenyezi Mungu atujaalie. *Haematology* saba tunahitaji hao, waliopo mmoja, mapungufu sita. *Anaesthesiology* wanane, upungufu mmoja.

Kwa ufupi kitabu hiki Mhe. Spika, orodha kubwa mahitaji sijui wangapi, tunategemea hospitali ya rufaa, kwa hali hii tutafika kweli. Huku ni kutiana mchanga wa macho Mhe. Spika.

Mhe. Spika, katika kiambatanisho nambari 14. Tumewapeleka wataalamu kwenda kusoma 90, kati ya hao serikali ya SMZ imepeleka 3 tu, mwelekeo ni mzito huu. Wananchi wetu watakuwa na imani vipi na hospitali hii ya rufaa. Mhe. Spika, wanachi wetu wanazidi kuteseka baada ya pesa nyingi kupeleka wagonjwa kwenda kutibu nje badala ya kuimarisha kitengo kilichoko pale. Mimi nitahitaji hao waliopelekwa nje hapa kwa majina yao Mhe. Waziri niwajue, maana yake kunakuwa na kilio wanyonge wanakuwa hawapati haki hii. Utakapokuja hapa Mhe. Waziri unieleze kwa majina tuwajue. Lakini kwa uwazi wako hakuna tatizo hilo Mhe. Waziri.

Mhe. Spika, nije katika kitengo cha upasuaji. Kitengo hiki ni cha muda mrefu na kina masikitiko makubwa. Chombo cha kupikia vifaa vile vya upasuaji, leo inayofanya kazi ni moja tu, watafanya kazi katika mazingira gani watendaji wetu hawa. Baya zaidi ni taa ya operesheni ambayo imefungwa kamba utafikiri ng'ombe anataka kukamwa maziwa, ikenda hivi ugeuke hivi, ukenda uende hivi. Gharama yake ni shilingi laki saba, kweli Wizara inashindwa kutoa shilingi laki saba, katika sehemu kama hii nyeti ya upasuaji. Waheshimiwa Wajumbe kama mimi nasema uongo twendeni mukaangalie, karibu mwaka mzima kitu hiki kimeharibika, utampasua vipi mgonjwa, taa ikienda upande si utamshona sivyo. Sio kuwa nabahatisha mimi.

Mhe. Spika, vitanda vya upasuaji mule ndani havikidhi. Sijui kama hakuwekwi makumbi upande wa pili mgonjwa anakowekewa kichwa. Hiyo ndio hali ya Hospitali ya Mnazi Mmoja hiyo ambayo tunategemea kuwa ya rufaa. Pale unaposubiria upasuaji yale makochi yaliyokuwepo pale ni aibu tupu. Twendeni mkaione ile hali ilivyo, je anaweza kukaa mtu pale akamsubiri mgonjwa wake. Feni halifanyi kazi, hatuwezi kufika hali kama hii.

Mhe. Spika, nije katika kitengo cha wagonjwa wa akili. Kwa kweli hapa utaona huruma kupita kiasi, milo yao hairidhishi. Asubuhi wanapewa mkate mmoja wa boflo na chai au uji. Nikupongeze Mhe. Waziri kwanza kwa kupata sindano ambayo inaitwa *modicated* ambayo imepatikana na inaendelea na huduma hiyo. Lakini kuna kilio cha dawa moja ambayo inaitwa *Alpidorol*, hiyo haipatikani ya kidonge imekuwa kilio mule ndani.

Mhe. Spika, mchana huo wali wanaopewa nafikiri kwa kukisiwa tonge mbili au tatu wanakula wagonjwa wale, yamo ndani mule. Nazungumzia hospitali ya Kidongo Chekundu. Wakati mwengine usiku wanalala kwa maji matupu wale, siku nyengine wanapata chakula na siku nyengine hawapati. Vyoo vyao vimefurika uchafu, na kuna baadhi ya wazee wakishawapeleka wale wagojwa hawapati hata kuwashughulikia, maana yake hata sijui tuseme vipi, maana yake kusema binadamu mwenzako ananuka haelekei, na sisi hatujesha kuumbwa, lakini hali zao za afya haziridhishi hospitali ya Kidongo Chekundu, pale panahitaji kuangaliwa.

Mhe. Spika, naomba kupata maelezo, kwani kuna kitengo kile cha Mkemia Mkuu kimepewa shilingi milioni 50. Kweli kitengo kile kitafanya kazi kwa milioni 50, kitengo muhimu kwa Wazanzibari kweli kimetengewa milioni 50, kitafanya kazi kwa milioni 50. Ndio hayo tunarudi kitengo cha rushwa na hiki kimetengewa milioni 50. Hapa nitahitaji maelezo. Hiyo Ofisi ya Mkemia Mkuu iko wapi.

Mhe. Spika, kwa hayo machache naomba nifikie hapo.

Mhe. Spika: Mhe. Jaku Hashim Ayoub tunakushukuru. Muda uliobaki ni mchache mno usingemtosha Mhe. Makame Mshimba Mbarouk kumaliza mchango wake. Kwa hivyo, yeye pamoja na wengine watachangia jioni, kwa maana hiyo niwaombe wafike mapema. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, Mhe. Mohamed Said Mohamed Dimwa, Mhe. Abdalla Juma Abdalla, Mhe. Abdalla Mohamed Ali, Mhe. Omar Ali Shehe, Mhe. Asha Bakari Makame pamoja na Mhe. Nassor Salim Ali. Niwaombe pamoja na Wajumbe wengine tufike mapema ili tuendelee na shughuli yetu.

Waheshimiwa Wajumbe, nimetumwa niwatangazie Waheshimiwa Wajumbe wanawake, kwamba ule mkutano wao wa mafunzo utakuwa unaendelea leo mnamo saa 7:30, pale ukumbi wa juu. Waheshimiwa Wajumbe, wote wanawake mnaombwa mfike kwenye mafunzo hayo saa 7:30 leo.

Waheshimiwa Wajumbe, baada ya hayo sasa niakhirishe kikao hiki hadi saa 11:00 jioni leo.

(Saa 6:50 mchana Baraza liliakhirishwa hadi saa 11:00 jioni)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano Yanaendelea)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe majadiliano yanaendelea, kwa jioni hii tuanze kumsikiliza Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, ambaye atafuatiwa na Mhe. Mohammed Said Mohammed.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Spika, ahsante sana na mimi kuweza kunipa leo kufungua dimba jioni ya leo hii na kuipa baraka Hotuba ya Mhe. Waziri wa Afya kuweza kuchangia kwa ufasaha zaidi na taaluma ndani yake.

Mhe. Spika, nianze moja kwa moja na suala la kwenye *Hansard*. Katika *Hansard* hiyo ya Hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa nia nzuri na kuleta ufanisi mzuri na kuweza kuokoa fedha za wavuja jasho.

Mhe. Spika, nilianza kusema kwamba tunazo mashine ambazo lengo kuu la kuitangaza Hospitali ya Mnazi Mmoja katika mwelekeo wa Rufaa. Kwa kweli huwezi kuwa na Hospitali ya Rufaa kama huna baadhi ya mambo ambayo yanayokwenda na wakati.

Mhe. Spika, nilisema kwa vifaa hivi tumenyang'anywa au tumepigwa changa la macho. Kwa kweli inasikitisha Mhe. Spika na nilisema vile na kufikiria kuwa lengo na madhumuni wahusika watakuja kunijibu vizuri na nia nzuri ya kuokoa.

Lakini mara nyingi sana tunasema kwamba Mawaziri tukifika pahala kuna mambo mengine tusilindane, kwa sababu tukilinda mtu tunajiboa sisi wenyewe na halafu tukisema huku juu tena wewe ndio unapewa kila aina ya majina, kama vile si mwenzetu, sijui nani, lakini kwa nia nzuri tu. Lengo la *backbencher* kuiona serikali na kuipa shindikizo kwa utendaji wake wa kazi.

Mhe. Spika, mimi ninayo *Hansard* ya Mhe. Naibu Waziri wa Afya na naomba kunukuu kidogo Mhe. Spika, alisema hivi “Baada ya Maabara kuwa tayari wameambiwa wale watu waje kuvihifadhi vile vitu, vikatolewa Mbweni na kupelekwa Mnazi Mmoja vifaa vilivyokuwemo na vingi vyao ni vifaa vya kisasa. Kwa kweli kuhimili kishindo cha leo Mnazi Mmoja kesho Mbweni, kesho kutwa Mnazi Mmoja athari imetokea na kama baadhi ya vifaa vimepata mikwaruzo”.

Sasa hapa mikwaruzo, nini maana ya mikwaruzo najiuliza kama mimi ni *specialist* nikitumia neno la kusema kwamba mikwaruzo, hapa Mhe. Spika nachanganyikiwa, kwa kweli vitu hivi ukitoa nje. Kwa mfano, twende kwenye *vespa* ukiitoa nje *package* yake inakuwa babu kubwa, inafika hapa kwa sababu wenyewe wataalamu wanajua wazi kama hivi vitu vinakwenda masafa marefu na wawimbi ya bahari basi *package* yake inakuwa ni nzuri. Lakini leo unasema mikwaruzo pengine Mhe. Naibu Waziri hata hivyo vyombo vyenyewe havijui, kwa sababu ikiwa ni mikwaruzo *it means* vimekwaruzika wapi?

Mhe. Spika, isitoshe na jambo la kusikitisha sana. Vyombo vile nilisema kwamba havikutimia na wale jamaa wa *laboratory equipment* hawakukamilisha vile vyombo. Kwa kweli sababu ya kutokukamilisha vile vyombo nitasema, kwa sababu vipo vingi tu hakuna na vimepata mikwaruzo hivyo vyombo, kuna mashine nyengine zimeshakuwa *old model* zimeshatumika.

Mhe. Spika, nadhani mpaka leo Mhe. Naibu Waziri hajaviona na sijui kama Mhe. Waziri ameshaviona au vipi. Lakini Mhe. Waziri hakutoa hoja yoyote labda kwa sababu hajaviona na hakuweza kuji-*commit* kwa kuwa hajaviona.

Lakini Mhe. Naibu wangu alisema kitu hajakiona. Mhe. Spika, sisi wengine hapa ni watoto wa mjini, maana yake tuseme ukweli wengine hatukuja kwa mwenge. Sasa unapokuwa kitu unakitaka basi lazima utakipata kwa

uchunguzi kwa damu tu ya zile fedha za walipakodi na tukifika kukisema hapa ujue kwamba tunakwambia kitu ni *pure* tena kwa ushahidi. (Makofi)

Mhe. Spika, ukitaka ushahidi kama huogopi hasara basi unda Kamati Teule na tumia kifungu chako cha 120 na wala sina dhana hiyo, lakini itabidi twende kwenye dhana hiyo, kwa sababu Kamati Teule Mhe. Spika ndio inayotoa vitu vyote *cream* na wala haifichi kitu, hapa tutakuja kujibiwa tu inavyotakiwa.

Mhe. Spika, mashine hizo ni mashine *special* ya kutizama utafiti wa *cancer*, Mhe. Spika, tunakufa wengi. Kwa mfano, kule wenzetu Bara kuna msururu mrefu na siku moja nilichukua kitu ambacho wanaita *bioses* cha mgonjwa mwenyewe, ilikatwa nyama na nilisema wacha niende mwenyewe.

Wallahi nilipokwenda kule Mhe. Spika kizunguzungu, nilikuta nyama za wenzangu tele zimejazana, lakini unajua Mheshimiwa tena nimeingia na jina la Mheshimiwa amekuja, basi nilipewa siku tatu na niliridhika, kwa sababu sikutaka niripuliwe, isipokuwa niondoke pale na kupewa kitu cha uhakika, basi nilipewa na baadaye nikarudi. (Makofi)

Kwa kweli Tanzania nzima ndio pale, sasa leo wenzetu hawa wametuletea mashine kwa ajili ya kuondoa tatizo hilo na kuleta hapa Zanzibar kwa kuwa hivi sasa tunayo hospitali ambayo tunataka tuibadilishe iwe rufaa, yaani iwe Hospitali ya Rufaa.

Mhe. Spika, mashine ile kuna *cassette* za kutilia nyama zenyewe hazimo kwenye hiyo mashine na utashangaa kwa kuwa Mhe. Makame Mshimba Mbarouk amezijuaje ah! Kwani kusoma kwenye ubao tu, unaweza kusoma kwa *practical* kwa kuangalia kitu tu tayari unaweza kusoma. (Makofi)

Vile vile kuna mifuko ambayo inahifadhia hayo masuala yenyewe, pia kuna ndoo za kutilia hizo nyama zenyewe mashine ile hazimo. Sasa baya zaidi Mhe. Spika, mtaalamu anashindwa kuziendesha zile hazina hata ile *catalogue* yake, hata saa Mhe. Spika inayo *catalogue* je zile mashine zisiwe na *catalogue*. (Makofi)

Jengine ambalo ni baya zaidi Mhe. Spika nilipata karatasi mimi hata huyo mwekezaji mwenyewe alikubali kwamba kuna vifaa vimekuja ni pungufu, *still* napingwa na barua hiyo anayo Mhe. Makamu wa Pili wa Rais na wala barua hiyo sikuandika mimi ni yetu wenyewe.

Mhe. Spika, naomba sana kwa kuwa fedha nyingi sana zimetolewa na sijui kiasi gani ambacho zimegharimu mashine hizi, lakini sina hakika si chini ya dola milioni 200 na wala sina uhakika na bei, isipokuwa ni dhana zangu gharama yake si chini ya dola 200 tunazipoteza. (Makofi)

Mhe. Waziri alisema baada ya wiki mbili hapa itakuwa tayari mashine zimeshafungwa na kazi inaendelea na mpaka leo hakuna kilichofanyika Mhe. Spika na tunalidanganya Bango Kitita.

Mhe. Spika, hili Bango Kitita kuna mambo mengine hapa tunaletewa kuhusu vifungu, mimi naomba Mhe. Spika kwa makusudi na tunaanzia wizara hii, hebu watuletee zile *activities* zao, wakija kufanya marekebisho ya vifungu, basi na vile vifungu viende sambamba na zile *activities* na watuletee hapa tuone kwamba jinsi gani fungu lile litatumika moja, mbili, tatu na sio watuletee makabrasha ya kubadili nusu ya kitabu chako hiki. Kwa hivyo, tunataka na *activities* zije hapa, ili tuone kama zitalingana *activities* na vile vifungu vilivyoelezwa humu kwenye kitabu.

Mhe. Spika, mimi nasema sana kama sikupewa jibu rasmi kuhusu mashine hizi sitounga mkono na wala sitopitisha kifungu na nitakuwa mkali sana, kwa sababu hizi fedha sijui za *UNDP* au serikali, lakini ni fedha ambazo tutumie kwa ajili ya kutafuta mashine hizi.

Kwa kweli mashine hizi zilipokwenda *laboratory* hazikupokewa, kwa sababu hazina *delivery*, sasa tumtafute huyo aliyekwenda kupokea ni nani, yaani aliyejitia kimbelebele na kwenda kupokea bila ya kufanyiwa *checkout* na mambo mengine ni nani? Mhe. Spika, kuna harufu ya rushwa hapa, lazima ipo rushwa, *ten percent* ipo. Sasa sijui nani aliyehusika na *ten percent* watajikamata wenyewe na tutawaweka askari nje hapo Mhe. Spika na tukimjua mtu tunamtia pingu. (Makofi)

Mhe. Spika, kitu hichi kinasikitisha sana.

Nikiendelea na mchango wangu sasa niende kwenye ukurasa wa 4 kuhusu suala la malaria nakubaliana nalo na waendeleo kulipukutisha kwa nguvu zaidi, kwa sababu tunajua maradhi ya malaria ni kitu hatari.

Vile vile kwenye ukurasa wa 13 kuhusu *Program* za Huduma za Macho, pia nakubaliana nao kwa asilimia mia moja. Kwa nini nakubaliana nazo? Mhe. Spika, na mimi nasema ni *member* wa macho tangu nimeumwa juzi *temporary* nitasema na mimi ni *member*.

Kwa mfano, kuna mashine nzuri sana ya kupima *Pressure* ya Macho. Kwa kweli ni chombo kizuri sana na tusijisifu kama sote ni wazima hapa, kwani mimi nilikwenda kule najiona niko *fit* nafika pale naambia mzee na wewe unayo kidogo unarandiwa na *Pressure* ya Macho, basi nilizimia, yaani hili tatizo kidogo tu nimeshakuwa hivi, kumbe vile ni muhimu na wala si mchezo *Pressure* ya Macho.

Lakini chombo hichi Mhe. Spika kipo Unguja tu, hivyo naomba kipelekwe na Pemba, kwa sababu kile ni Zanzibar nzima chombo kile kipo hapa na wala hakiwezi kuhamishwa hapa na pale. Mhe. Spika, naomba sana na Mhe. Waziri atafute *funds* kwa ajili ya kuletewa chombo chengine kama kile, ili watu wa Pemba na wao wafaidike na huduma kama hizo, vyenginevyo vyovyote tukikihangaisha kile tutakuja kukimaliza na fedha hatuna za kuweza kusaidia. (*Makofi*)

Mhe. Spika, katika lile jengo la macho ni hatari tupu. Mimi mwenyewe nilikwenda kule juu kuna *tissue* fulani nikazifuata kwa ajili ya kusafishia jicho na pia kuna dawa nyengine lazima nikaipate pale. Mhe. Spika, chumba wanachokaa wale *Nurses* ni hatari, yaani ile sakafu au saruji imezuiwa na *asbestos* au sijui na kitu gani kile, wakati wowote watu watahuka kwa *lift* na saruji yao. Kwa kweli hii ni hatari na wala si kitu cha mchezo na tukaangalie kule ni hatari tupu.

Mhe. Spika, ni kitu ambacho kwa nini hatupendi kutembelea masuala haya. Kwa mfano, siku moja nilisema hapa bajeti iliyopita hebu watafutwe *special ground* hawa na wajengewe jengo lao, wanavyo vitanda saba tu kwa ajili ya *operation* na vyengine wanakodi katika jengo jengine na Mapinduzi Kongwe kule. Mhe. Spika, vitengo hivi tunaviputa kusema kweli.

Tukija kwenye Kitengo cha Sukari nacho ndicho kinatupwa kabisa haina hakijulikani haina baba wala mama. Kwa kweli sijui sababu gani Mhe. Spika au sijui wenyewe wanadhibiti vizuri na watu hawapati fedha za kula au vipi na hilo siwezi kujua, lakini vitengo vyenye ulaji watu mbio wanavipa heshima na taadhima. Mhe. Spika, naomba sana tuangalie ndugu zetu hawa ambao wenye matatizo haya.

Mhe. Spika, ukurasa wa 36 sasa ndio naingia kwenye hospitali yenyewe na huko kote nilikuwa nikiranda tu. Mhe. Spika, nitoe hongera sana kwa *ICU* na mimi mwenyewe shuhuda.

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, bado dakika tano.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Hee! Mhe. Spika, nilifikiria leo nimeanza mwanzo jioni angalau utanipa dakika 30, lakini haya tunaendelea na wala sitaki nikukere.

Mhe. Spika, hivi sasa hospitali kuna hali ngumu. Kwa mfano, tukienda kwenye fungu la chakula hapa kuna shilingi 79,732,000/=, lakini chakula hakuna sasa niseme fungu hili halitoshi au linatosha, lakini hali ni ngumu na tutakuja kusema baadaye baada ya kupata maneno mazuri ya Mhe. Waziri na kuweza kupitisha vifungu tutakuja kupambana hapo. Hiyo nimetoa indhari tu kwa sababu chakula hivi sasa hakuna. (*Makofi*)

Lakini Mhe. Spika, najiuliza nani Daktari Bingwa? Hivi kweli sisi tunao Daktari Bingwa wanaofika 27 kwenye ukurasa huu, ambapo Wazalendo ni 13 natafuta Daktari Bingwa.

Mhe. Spika, Daktari Bingwa ninavyofahamu mimi nilivyosomeshwa ni watu walio-*specialise* hao ndio najua madaktari Bingwa tunao watatu tu na aje Mhe. Waziri anikatalie na waliobakia wote wamekimbia, kwa sababu fedha kidogo na wasikimbie vipi Mhe. Spika, hivi sasa hata hawa *Nurses* wanakimbia mshahara kidogo na kesho kutwa *Orderlies* watakimbia fedha kidogo. (*Makofi*)

Mhe. Spika, ninachotaka kumuomba Mhe. Waziri anataka kusomesha wengine na tabu ya nini, kwa sababu hizo fedha zote ambazo unazotaka kusomesha kwanza walinde hawa watatu waliobakia tena unawahesabu hasa.

Kwa mfano, sehemu ya koo ame-*specialise* Dkt. Naufal Kassim na wengine tumewapa uongozi kabisa, maana yake tunaye Dkt. Mohammed Jidawi ni *specialist* hasa yeye, lakini tumemtia kwenye mambo ya *management* na tumemziba. Vile vile yuko mwingine Dkt. Maliki *specialist* na yeye ndio kabisa, isipokuwa wanakwenda kule zile sifa zao tu, lakini hawamo katika kundi la kusema kwamba tunawataka wawe katika kundi kama hili. (*Makofi*)

Mhe. Spika, nafikiria watu kama wale tusiwape madaraka kwa ajili ya kutuokoa sisi binadamu na tuwaongeze mishahara, kwa sababu tunaposhindwa kuwapa mishahara ndipo tunapowageuza kuwapa vyeo kama vile Katibu na Wakurugenzi, kwa kuwa hatuna uwezo wa kuwalipa ndio maana tunawabadilisha hivyo.

Lakini Mhe. Spika, kwa kumalizia haraka haraka namuomba sana Mhe. Waziri kwamba ajitahidi sana zile fedha ambazo anazotaka kusomesha hivi sasa basi awaenzi hawa watatu kwanza na ajue kwanza hawa anawapa fedha nzuri na wasiondoke Mhe. Spika.

Kwa mfano, madaktari wameshatukimbia hapa na wala hatuna madaktari wa mifupa, kwa sababu wameshatukimbia na kila siku mimi nasema na hizi kada ziangaliwe vizuri. Vile vile wale *Nurses* hawapewi *risk allowance*, *night allowance* na wala hawa *Orderlies*, pia hawa *Orderlies* wasomeshwe nao, ili waweze kufika katika hizo kada mnazozitaka, hebu zifanywe kwa makusudi, yaani wakasomeshwe *as a group*.

Mhe. Spika, kwa kumalizia naomba nizungumzie kuhusu *lift*. Kwa kweli *lift* zile ni mbovu na wala haijulikani hiyo mpya hivi sasa vipi na ukiingia ni *yaumushaka*.

Vile vile naishukuru sana wizara imeunda wale watu wanaokusanya fedha na wala wafanyiwe wawe kama ni askari wa Hospitali ya Mnazi Mmoja wale vijana wanaokusanya fedha tena waongezwe, kwa sababu kule Mapinduzi Mpya watu wanaibiwa kila leo. Kwa hivyo, wale vijana wapewe mafunzo vizuri pamoja na kulipwa fedha vizuri na wageuzwe kama kule wenzetu Muhimbili wanao watu kama wale, wakati na sisi tunakusudia kufanya Hospitali yetu kuwa ya Rufaa.

Mhe. Spika, namuomba sana Mhe. Waziri wale waongezwe ni kidogo, sare zao nzuri zinapendeza na nini, lakini sujui fedha zao kama zitalingana na sare zao, kwani inawezekana sare nzuri na mishahara ukawa mdogo na wala haina maana itakuwa haifai. (*Makofi*)

Mhe. Spika, nimalizie kwa kuheshimu dakika zako, lakini kidogo umeninyima, isipokuwa nataka niheshimu kiti chako. Naomba nimalizie kwa Hospitali ya Wagonjwa wa Akili. Kwa kweli tunajua sote katika hospitali ile, nasikia pale kunataka kujenga jengo la Wazazi, mtawamaliza wazazi kuwa kuwauwa kwa wagonjwa wa akili na wala vitu hivyo havilingani kabisa. (*Makofi*)

Mhe. Spika, hospitali ile tunaielewa ina *special* ya nini, yaani ya wagonjwa wa akili, sasa leo unakwenda kumpeleka mzazi ambaye anakwenda tumbo liko mbele na yule anaweza kufikiria beni atakwenda kumvamia mama yule kwa kumpiga, atajibu nani makosa. Kwa kweli pale nasikia pale panatakiwa kujengwa jengo la wajawazito, basi ni vyema kutafuta sehemu nyengine kwa ajili ya kubadilisha.

Kwa hayo machache Mhe. Spika, kwa kuheshimu wakati wako. Lakini kuna vile vituo vidogo vidogo kwa mfano kama kule Kitope kuna *Dispensary* kule analipa nani umeme na umeme umeshakatwa kule na kila siku nagombana na watu wa umeme, wananiungia, lakini hamuwalipi na humu mafungu ya kulipwa. Sasa vituo kama vile nani wa kulipa naomba Mhe. Waziri wakati atakapokuja kufanya majumuisho aje aniambie. (*Makofi*)

Mhe. Spika, kwa hayo machache nasema sitoiunga mkono kama sikupewa taarifa rasmi ya kupata mashine hizi za Kitengo cha Kuchunguza Saratani kwa hapa Zanzibar. (*Makofi*)

Kwa hayo machache, Mhe. Spika naomba kukaa kitako. (*Makofi*)

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, tunashukuru na sasa tumkaribishe Mhe. Mohammed Said Mohammed na baadaye Mhe. Abdalla Juma Abdalla.

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Spika, nikushukuru kwa jioni hii ya leo kunipa nafasi hii. Lakini nichukue nafasi hii kumpongeza babu yangu Juma Duni Haji kwa uwasilishaji wake mzuri kabisa ingawa alikuwa akinywa maji mengi najua *speed* ilikuwa ni kubwa. (*Makofi*)

Vile vile nimshukuru Mhe. Naibu Waziri kwa kuweza kutujibu maswali uzuri, kwa ufasaha tena kwa sauti kubwa sana. Pia niwashukuru watendaji tena watendaji wote wa Wizara ya Afya kwa kukusaidia wewe Mhe. Waziri kuandaa bajeti hii na kuja hapa ukaisoma kwa ufasaha zaidi nakupongeza sana. (*Makofi*)

Mhe. Spika, nianze kwenye ukurasa wa 13 kuhusu *Program* ya Huduma za Macho, ili niweze kwenda haraka haraka niweze ku-*meet* na muda wako. Juzi wakati Mhe. Waziri alipokuwa akijibu hii *Primary Eye Clinic* hivi sasa haipo. Lakini mimi najua kitengo hichi kilikuwepo tangu zamani na kiko katika Idara ya Kinga na hawa waliokuwa wakiiongoza kitengo hichi ni *Help Aid International*, lakini tangu kuondoka *Help Aid International* nayo ime-*paralyse* kabisa haipo na wala haifanyikazi vizuri.

Mhe. Spika, kitengo hichi ni kizuri ambacho kilikuwa kinasaidia hata kupita katika zile Nyumba za Wazee na kuweza kuwafanyia *investigation* za hapa na pale. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri wakati atakapokuja aniambie ni lini hichi kitengo kitarudishwa, ili kiweze kutusaidia kupita vijijini na kuweza kutibu kuliko kuachia zile *Private Institution*, ambayo kama hivi sasa ipo tunataka serikali iweze kuchukua mkondo huu na iweze kuwasaidia wananchi wake.

Nikiendelea na mchango wangu sasa niende kwenye ukurasa wa 38 kuhusu *ICU*. Mhe. Spika, nataka kusema kwamba nimpongeze sana Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake wote, kwa sababu muungwana ni kitendo. Katika bajeti ya mwaka jana Mhe. Waziri alituhidi haifiki miezi sita *ICU* itakuwa tayari. Mhe. Waziri nichukue fursa hii kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Mpendae kukupongeza kwa makusudi kwa hatua yako kubwa sana. (*Makofi*)

Lakini *ICU* mimi mwenyewe najua na nimetembelea na vifaa vilivyopo ni bora sana Mhe. Spika. Vile vile namuomba Mhe. Waziri atakapokuja aniambie kwamba je, yupo *Incharge* pale ambaye ni *Physician* au hakuna pale, nataka nijue utaratibu huu kwa sababu gani? Kwa kweli juzi nilipita pale kuna mgonjwa, lakini hayupo Daktari na yupo *Nurse On Call* tu ni siku ya *holiday*. (*Makofi*)

Sasa nataka kujua pengine mwananchi hawawezi kujua daktari watampata wapi au *Physician Specialist* yupo pale au tumeweka mtu pale kufanyakazi hii, basi naomba Mhe. Waziri ukija hapa uweze kuniambia na mimi angalau niweze kuwaelimisha wananchi wangu. (*Makofi*)

Mhe. Spika, sasa niende kwenye ukurasa wa 43 kuhusu Idara ya Hospitali ya Mnazi Mmoja. Mhe. Spika, Hospitali yetu ya Mnazi Mmoja tunajitahidi sana kwa usafi na ni bora sana, lakini kuna mapungufu tena sio madogo au makubwa. Kwa hivyo, naomba niende kwenye *First Track* na kitu hichi ni kizuri ambacho mumekianzisha ni bora, tena kinasaidia watu wengi wale wenye uwezo wa kwenda katika *First Track*. (*Makofi*)

Lakini kitu kinachotokea pale hata Kamati au Mwenyekiti wa Kamati yako anasema limekuwa shamba la bibi fedha za pale hazijulikani ziko wapi na mimi nataka uniambie fedha za pale zinapelekwa wapi kama zinaingia kwenye Mfuko wa Serikali, basi tujue Mfuko wa Serikali wapi unakwenda, kwa sababu limekuwa shamba la bibi kile tunachokilipa hatukioni kwa matumizi ya kawaida. Lakini kama wanalipwa wafanyakazi basi tujue kwa njia gani wananchi wanaweza kulipa, ili tuweze kujua wafanyakazi wanalipwa vipi katika *First Track*. (*Makofi*)

Mhe. Spika, katika mchango wangu bajeti iliyopita katika wizara hii nilikuwa nikizungumza juu ya *Orthopaedic Clinic* au tunaita Kioski, sehemu ile watu wanapotiwa piopio. Kwa kweli nilisema kile kitanda cha. *Orthopaedic Clinic* sio kitanda, kwa sababu kile tunaweza kusababisha wananchi wetu kupata *tetnus* kwa kilivyo kibaya, yaani tangu mimi sijazaliwa kile kitanda kipo na mpaka hivi sasa kipo na leo asubuhi nilikwenda kunitizama kwa makusudi kimeondosha au bado kipo, lakini kile kitanda bado kipo. (*Makofi*)

Vile vile namuomba Mhe. Waziri katika hili pia aje aniambie kitanda kile atakiondoa vipi na nitakuwa mkaidi sana leo kwenye bajeti yako kupitisha vifungu kutokana na vitu kama vile, kwa sababu lazima tutengeze mazingira bora, ili wananchi watibiwe katika sehemu nzuri kabisa. (*Makofi*)

Mhe. Spika, sasa naomba nizungumzie kuhusu *X-Ray Department*. Kwa kweli *X-Ray Department* ni chombo chetu muhimu, lakini nacho kina mapungufu yake mengi pamoja na wafanyakazi wa pale hawalipwi yale maposho yao madogo madogo, lakini na kwenye utendaji hauko katika hali nzuri. (*Makofi*)

Mhe. Spika, tarehe 31 Machi, katika Jimbo langu Chuo changu cha Mpendae kilipata ajali, lakini hali ya mule niliikuta ngumu na tulijazana na hata *AC* haifanyikazi kwa wakati ule na inasikitisha sana na hata zile *films* tumekwenda kumtoa mtaalamu huko aliko kuja kutupa *films* pale na *films* zenyewe za kuunga unga yaani vipande na *films* kubwa hazipo. (*Makofi*)

Kwa hivyo, Mhe. Waziri atakapokuja namuomba kupitia kwako Mhe. Spika, aniambie kwamba *films* zinanunuliwa na kupatikana vipi hata usiku zikakosekana pale? (*Makofi*)

Mhe. Spika, siku hiyo ilibidi nivue joho langu na uheshimiwa na nikaingia udaktari hata *trolley* nilibeba mwenyewe na kupeleka watu wangu juu, kwa sababu ya upungufu ya wafanyakazi waliopo pale, kwani tuliambiwa *Orderlies* wapo wengi lakini bado hawajaajiriwa, lakini kipindi kile kilikuwa kigumu. Mhe. Waziri siku hiyo kama ungeniona basi ungedhani sijui mtu gani, kwa sababu nilikuwa nikibeba watu wawili wawili kama *Tayson* vile. (*Makofi*)

Sasa niende kwenye *Mini Theator* Mhe. Spika. Wakati ule ajali inatokea pale tulikusanya kwenye *Mini Theator*, lakini ile haitoshelezi na nilikuwa nikipiga kelele katika bajeti ya mwaka jana ile *Emergency Room* iko wapi, kwa sababu hivi sasa imekuwa ni empty room na Mhe. Waziri uniambie tokea mwaka jana nilitoa na ukiangalia *Hansard* utakuta hicho kitu kama nilikisema kwamba lazima tuweze kuimarisha ile *Emergency Room* kutokana na mambo mengi yaliyopo.

Kwa mfano, sababu moja ambayo niliyoitaja nilisema kwamba *traffic* hivi sasa imeongezeka Zanzibar na ajali zimekuwa nyingi, sasa bila ya kuwa na *Emergency Room* tutakuwa na hadith tu, kwa ile *Mini Theater* iliopo pale ilikuwa ni ndogo.

Hata zile *TS* ambazo nilikuwa nimenunua mimi mwenyewe, basi hospitali hakuna kwa ajili ya kuwapa wananchi wangu, basi tulikuwa tunawaweka kitako na kuwachoma, kwa sababu hakuna nafasi ya kutosha. Kwa kweli ile sio *Minor Theater*, isipokuwa ni kichocho tu na hata wale wafanyakazi wa pale nadhani hawawi katika hatua au mazingira mazuri ya kufanya kazi, tena nina wasi wasi wao wanaweza kupata maradhi, pia *risk allowance* sijui kama wanalipwa.

Mhe. Spika, jambo jengine ambalo nataka kusema ni kwamba huduma dhaifu hasa wakati wa siku za holiday na baada ya saa za kazi. Mhe. Waziri ningekuomba kwamba siku moja tufanye ziara ya kushtukiza na hiyo nimeshakuomba mara nyingi, kwa sababu kuna mambo mengine Mhe. Waziri anadanganywa na tufike pahala twende *field* wenyewe, ili tukaone wenyewe ule udhaifu ambao unaoweza kutokea. Mhe. Waziri, sisi ni kazi yetu ni *over site role*. Kwa hivyo, tunapita na kuona yale mambo ambayo yanayofanywa, kwa hiyo tunakusihhi sana. (*Makofi*)

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, ukizungumza na kiti itakuwa ni vyema zaidi kwa mujibu wa Kanuni zetu. (*Makofi*)

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Spika, nakushukuru. Sasa naomba niende kwenye ukurasa wa 46 kuhusu Idara ya Bohari Kuu ya Madawa. Mhe. Spika, jambo ambalo Mhe. Waziri anaweza kulipanga ni jambo zuri kuweka Huduma za Bohari Kuu ya Dawa ambayo tayari inasimamiwa au tunaanza kuijenga kule Maruhubi na hili ni jambo zuri sana.

Lakini kuna kasoro ambazo zinazoweza kutokea. Kwa mfano, hivi sasa Mhe. Spika, kuna kile Kiwanda cha Uchapaji (*Press*) kinajengwa pale, sasa *security wise* nafikiri kwa majengo kama haya nadhani sio nzuri, kwa sababu ya mchanganyiko.

Hali hii inatokana na kukosa *plan* ofisi yetu kama tulivyokosa *plan* ya Mji wa Zanzibar tukafika pahala hatuwezi kufanya kitu ndivyo kinavyoendelea. Wale wafadhili ambao wameisaidia tayari watataka upanuzi pengine wa mbele, hatuna tena. Pengine tutizame kule Keko MSD vipi walivyojenga yale magodauni yao na vipi *security* yao inavyokuwa nzuri. Mimi ningekuomba Mhe. Waziri hili ulifatlilie na uweze kuzijua kwa makini zaidi.

Mhe. Spika, Afisi ya Mkemia Mkuu Nambari 47, mimi nasema fungu lilotiwa hapa ni dogo sana haliwezi kukidhi haya ya Mkemia Mkuu, halafu tusije tukatafuta rushwa inatokea wapi. Mhe. Spika, fungu hili ni dogo sana, tunaomba sana lifikiriwe kama kuna sehemu nyengine liweze kupatiwa fungu hili.

Mhe. Spika, nije kwenye Chuo cha Taaluma za Afya. Mhe. Spika, Mhe. Rais wakati wa hotuba yake hivi karibuni alitaka kukiunganisha Chuo hichi na Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) hili ni jambo jema kwa sababu tutakuwa na chuo kishirikishi. Lakini tuiangalie ni taaluma gani inatolewa hapa. Hapa tunatoa diploma je, walimu wetu wanazo zifa za kusomesha digirii wa hapa. Tunampango gani wa kusomesha walimu wetu ili kurudi kusomesha hapa.

Mhe. Spika, inasikitisha sasa hivi tunaambiwa kada ya maabara, inawalimu wawili tu ambao wa kudumu lakini wote wanaokuja ni *part time*. Sasa tungekushauri hichi Chuo tungeweza kutengeneza taifa lililokuwa zuri, tukiwa na mipango mizuri baadae wanaotoka hapa tukawapeleka ili kuweza kufanya digirii pengine wakawa watendaji wazuri sana. Chuo hichi kina Bodi na Bodi ndio chombo kikuu cha kuendesha chuo hichi. Tunaomba sana Bodi ifikirie kuwapeleka walimu wale masomoni ili basi tuweze kupata wataalamu wengi wa kutosha.

Mhe. Spika, nije kwenye ukurasa wa 66 unazungumzia Baraza la Wauguzi. Katika kitabu cha mwaka jana na cha leo ya jana ndio yale yale, ya leo ndio yale yale, hadithi ndio ile ile, *copy and paste*. Tungeomba angalau tupewe hivi vipaumbele vyengine vilivyokuwa vipya, tusirudi nyuma. Zanzibar tumekuwa tunamchezo wa kurudi *reverse* tu kila wakati, tusirudi nyuma Mhe. Spika, tuende mbele. Hata hawa wauguzi waliokuwepo sasa hivi wapigania haki zao. Wenzangu wengi wanasema madaktari, madaktari, lakini kuna kada nyingi katika hospitali.

Mhe. Spika, kwenye hospitali kuna kada ya *pharmacy*, kuna kada ya *laboratory*, kuna kada ya *X-ray* na wauguzi, hawa watu wote wanafanya kuwa ni timu moja ndio inakuwa Hospitali inajengeka vizuri. Lakini leo tunamlipa *night call* daktari peke yake. Hawa tunawaweka katika fungu gani. Tualipa daktari *risk allowance* hawa tunawaweka katika fungu gani. Mhe. Waziri hebu niambie ukija hapa hawa tayari wameanza kulipwa hizi *night call* au hawana sifa gani za kuweza kulipwa au hawa sio watendaji wa wizara yako, naomba hilo.

Mhe. Spika, narudi kwenye ukurasa wa 89, kuanzisha huduma za mafigo, hili nilipoliona kwenye kitabu chako nilifurahika sana. Lakini nataka uniambie ni mashine ngapi za *dialyses* ambazo zitaweza kununuliwa na kuweza kufanya kazi. Kwa sababu hivi karibuni nilipata mgonjwa kwenye jimbo langu alikuwa ICU alitaka kusafirishwa kupelekwa Dar-es-Salaam tarehe 21/6/2012 ambaye figo zote zilikuwa tayari zimefeli.

Kwanza kabisa kwa masikitiko makubwa yule mgonjwa amefariki dunia baada ya kufika Dar-es-Salaam. Hii inatokana kuwa hatuna juhudi za kutosha, tungenunua mashine hizi angalau tungefanya *dialyses* kwa wakati, tukaweza kuokoa maisha ya watu wetu. Ingawaje hatuna *ethnologist* hata mmoja katika hospitali yetu.

Mhe. Spika, wangonjwa wetu wanaopelekwa Dar-es-Salaam wanakuwa katika hali ngumu sana. Wanaambiwa tu wakishakupewa *refer* nenda Dar-es-Salaam, lakini watakwenda kwa nini? Wananchi wetu masikini sana, hawana uwezo. Tarehe 29/6/2012 pia katika jimbo langu aligongwa mtoto mmoja ambaye ana miaka 20 akapelekwa pale, akaambiwa apelekwe Dar-es-Salaam. Tatizo lililojitokeza kwamba kaambiwa tu nenda na *file* zako na kule kulikuwa kuna mgomo mkubwa. Atakwenda vipi huyu bila ya kufanya *connection* yoyote, bila hata ya kupewa msindikizaji. Mhe. Spika, inasikitisha sana hospitali yetu.

Mhe. Spika, vile vile tarehe 27 mwezi wa 6 alikufa kijana mmoja pale katika hospitali ya Mnazi Mmoja ambaye anatokea katika jimbo la Mhe. Makamo wa Pili wa Rais. Yule kijana alikuja pale na *perforated peptic ulcers* tangu saa nane kalazwa, lakini upasuaji kafanyiwa saa 5 ya usiku, kupelekwa ICU dakika chache sana amefariki. Sasa huu tunauita uzembe na ndio maana nikauliza ICU tuna *physician* yoyote ambaye amewekwa. Kipindi chote cha saa 8 mpaka saa 5 usiku, ambaye Mkuu wa *Department* Dokta Yunus ndio kafanya *operation* hii. Ni muda mkubwa Mhe. Waziri, muda mkubwa tumekaa muda mwingi tuwahudumie wananchi wetu kwa mambo ambayo kuna vifo vyengine tunaweza kuvisaidia vikaja juu sio kukaa muda mwingi.

Mhe. Spika, nije moja kwa moja kwenye jambo la Jimbo langu la Mpendae. Katika hotuba yangu ya mwaka jana nilizungumza na tukazugumza na Mhe. Waziri na akatoa ahadi, tangu ilikuwa ahadi ya Rais na akatoa ahadi yeye kuwa atajenga lakini bila ya muda maalum kusema kwamba nitajenga lini hospitali ya jimbo la Mpendae.

Mhe. Spika, nilikuwa tupo tayari twende kwa Mhe. Waziri na tukakutana mara kadhaa. Kama serikali haitaki kutimiza ahadi ya Mhe. Rais, mimi nitatoa pesa za CDF kuweza kujengea hospitali yetu ili watukabidhi Hospitali ya Mpendae. Lakini mpaka leo imekuwa nenda rudi mpaka sasa hivi sijakabidhiwa chochote kupitia Hospitali ya Mpendae. Nataka nimwambie Waziri aje anijibu hospitali ya Mpendai imefikia hatua gani. Sitaweza kuunga mkono bajeti hii mpaka nijue hatima ya Mpendae.

Vile vile kama nitazuia kifungu kitapitishwa basi mimi nakuomba Mhe. Spika, nitoke nje ili nisione madhila haya wala sitaki historia iweze kuja kunihukumu. Sitapitisha bajeti hii, babu yangu duni nakupenda sana lakini hapa sitapitisha. Mhe. Spika, kwa hayo machache mimi siungi hoja hii hata asilimia moja. Nakushukuru.

Mhe. Abdalla Mohammed Ali: Ahsante Mhe. Spika, na mimi laasiri hii kunipatia fursa ya kusema machache kuhusu hoja iliyopo mbele yetu. Tokea kuanza kwa bajeti ya mwaka huu wajumbe wengi tumekuwa tukihoji kwamba kuna mafungu ambayo maelezo yake hayatuingii akilini. Mafungu ambayo yamewekwa katika mpango huu wa matumizi lakini tukiangalia ule umuhimu wake huwa hatuoni. Jumejaribu kuuliza maswali mengi ili tupate majibu turidhike roho zetu, lakini bado tunaendelea kuuliza maswali.

Mimi ningeanza kumuuliza Waziri anayeshughulikia Wizara ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Tukiangalia mafungu yaliyomo tunaona kuna mafungu ya nauli, kuna *medical allowance*, kuna manunuzi ya zawadi pamoja na mafungu ya likizo. Mimi ningependa tu kabla ya kuanza hotuba yangu nikapata maelezo.

Je, hivi sasa kuna utaratibu gani huko serikalini kuhusu mambo haya kwamba kuna *medical allowance* ambao Watumishi wa Umma wanatakiwa waipate na waipate katika njia tani. Waliingiziwa katika mishahara yao au kuna fungu maalum ambalo linawekwa wao wapewe. Je, hizo likizo zinatolewa vipi na kama zinatolewa ni kiwango gani kwa kila mtumishi wa umma anatakiwa apatiwe kwa kipindi hicho ambacho yeye atakuwa yupo likizo. Huo ni utangulizi.

Mhe. Spika, tuna taasisi yetu ambayo tunaitumia kwa kutoa wataalamu Chuo chetu ambacho tunakiita Chuo cha Afya. Nilikuwa nafikiria kuwa hivi sasa katika kipaumbele kikubwa cha Serikali ni kupata mdaktari kwa sababu ndio kilio kikubwa katika nchi yetu. Hivi karibuni serikali kwa makusudi iliongeza mishahara ya madaktari kwa kujua kwamba watu hawa wana umuhimu na watu hawa hatunao, hao tulionao wameanza kuondoka.

Mwaka jana nilikuwa nafikiria kwamba kwa vile Chuo hichi kina umuhimu wa pekee basi zile ada ambazo zimewekwa kwa ajili ya wanafunzi kujiunga katika chuo kile nilikuwa nafikiria zingekuwa za chini, kiasi kwamba kuwaruhusu wananchi wetu waliokuwa wanyonge wakapata kujiunga na chuo kile. Ili baadaye tupate hao wataalamu ambao tunawahitaji. Lakushangaza ni kwamba hivi sasa ada ya kuingia katika Chuo kile ni kubwa mno, kiasi kwamba walio wengi hawaweza kuifikia.

Mhe. Spika, ningemuomba Mhe. Waziri atakapokuja labda akanieleza je, ada hii iliyoruka mara nne, mwenzangu alisema trufu, trufu, ilikuwaje ikaongezeka kiasi kama hicho. Je, labda katika chuo hichi kuna ruzuku ambayo inatolewa na Serikali kama milioni 559. Je, wale ambao wanasoma pale wanafaidika nini na ruzuku hii au yote inatumika katika uendeshaji tu.

Mhe. Spika, katika kitabu chetu tumetaja kwamba kutakuwa na matengenezo au ujenzi wa Hospitali ya Abdalla Mzee iliyopo Mkoani. Najua fika kwamba hospitali hii tokea ilipojengwa miaka ya 70 ilikuwa ina wafadhili, makomredi wenzetu kutoka China. Tokea miaka hiyo hadi hii leo Hospitali hii bado inaendelea kupata ufadhili wao. Lakini katika hilo niseme kwamba labda Serikali imejisahau kwamba kwa vile kuna ufadhili huu wa wenzetu kutoka China basi wao watakuwa pembeni hawahusiki na chochote.

Mhe. Spika, hospitali inafika wakati inachosha hata kuiangalia. Kwamba huo ukarabati wake unachukua muda mrefu. Ninachokifahamu japo hospitali hii sio ya rufa lakini kule kwetu Pemba hospitali hii inahudumia wagonjwa wengi sana. Kwa maana ya kuwa katika hospitali ile kuna madaktari. Mimi katika hilo ningependa niulize hawa madaktari waliopo katika Hospitali ya Abdalla ambao ni wenzetu kutoka China, hivyo wana kiwango gani cha udaktari, ni madaktari bingwa au wana kiwango gani.

Nasema hivyo kwa sababu ikiwa madaktari hawa wamefikia kwamba wao ni madaktari bingwa gasi hospitali ile ilibidi iwezeshwe iwe na vifaa ambavyo wale madaktari bingwa tungewatumia kwa njia ambayo ingetusaidia zaidi. Leo madaktari wale wapo katika hospitali lakini na wao wanafanya *refer* kuja Mnazi Mmoja. Sijui ule utalamu wao

walionao unatosheleza kwamba wao ni mkubwa kiasi gani, kiasi kwamba waletwe Wachina kuja kutusaidia sisi. Lakini wanapofika hapa kile walicholetewa hakipatikani kwa sababu hawana vifaa. Ikiwa hospitali ile inataka kupandishwa daraza sasa je, daraja hilo litaongezwa kwa majengo tu kwamba tutapanua majengo ndio tutasema kwamba tumeongeza kiwango au kutaongezeka na huduma za afya ambazo zitatuonesha kwamba huduma sasa zimeboreka kwa maana hiyo imeongezeka daraja.

Mhe. Spika, cha kushangaza ni kwamba hivi sasa ninavyozungumza Mheshimiwa kwamba pale hata zile *X-ray* karibu miezi mitatu hazifanyi kazi. Niliwahi kuzungumza na Wahusika Waziri na wengineo. Wakanambia kwamba mafundi watakwenda na kweli mafundi walikwenda lakini badala yake wakagundua kwamba kinahitajika kifaa fulani. La kushangaza hadi hii leo kifaa hicho hakijapatikana. Kwa maana hiyo yule mgonjwa apewe *refer* ya kwenda Wete. Wakati anapotakiwa kwenda Wete anatakiwa atie *Ambulance* mafuta na kama ni mbonjwa mahututi sijui hali yake itakuwaje akifika Wete.

Namuomba Waziri kwamba labda kungekuwa kuna fungu maalum wakati wa kutokea dharura kama hii basi kule kwetu haraka sana ikatatuliwa, ili wananchi na wao waone kwamba Serikali yao inawathamini. Katika hospitali hiyo hiyo Mhe. Spika, leo utakutia matatizo mengi yaliyopo ni uongozi. Imekaa kama ni sehemu ya majaribio, mara unakutia huyu ndio muongozaji mara unakutia yule, kiasi kwamba hata wale waliyopo kuusaidia huo uongozi basi wanashindwa kufanya kazi zao. Kwa maana hiyo wengi wanashindwa na unakutia kuna uchelewaji uliokithiri, uchafu uliokithiri katika hospitali ile. Nathubutu kusema baada tu ya Serikali hii yetu tuliyonayo kuingia madarakani, wafanyakazi wale waliingia kwa moyo mmoja na ulikuwa ukifika hospitali unakutia wao wenyewe wanachukua vitambaa na kusafisha. Lakini kutokana na uongozi uliopo kima mmoja anajionelea aaah leo nimechoka na mimi sifanyi chochote.

Mhe. Spika, hapo hapo hospitali utakuja kukutia wale wanaofuatana na madaktari bingwa hao wa Kichina basi taaluma zao sijui wamezipatia wapi. Lakini leo ndio wanaotuendesha, nashukuru kwamba kuna vijana ambao wanatoka vijijini wanafuatiliwa bila ya kusoma. Kinachovunja moyo zaidi ni kwamba ukenda huko ambako wenyewe wanawake wanakuita kwenye dungu unakutia kuna wanaume. Hii inatokana na upungufu wa madaktari. Nashukuru kwamba walipelekwa wengi katika Hospitali ya Abdalla Mzee, lakini bado waliopo hawajatosholeza.

Katika kipindi kilichopita kuna madaktari karibu 174 au 73 walitoka, sijui kuna utaratibu gani wa madaktari wale kuwapeleka katika hospitali kuwagawa. Je, katika mango wa mara hii wa ugawaja au wa utumishi wamo wamewekewa fungu ili kukidhi mahitaji angalau kupunguza ule upungufu tulionao katika mahospitali yetu. Juu ya hayo katika hospitali hizi pia zinasaidiwa na hospital za vijijini. Sasa madaktari wengi wanaopelekwa kule wanakuwa hawakai kule, matokeo yake ukifika wakati mtu anahitaji msaada hayupo.

Namuomba Waziri wakati anapofanya uteuzi au upelekaji wa madaktari katika vijiji vyetu vinavyozunguka hospitali hizi akawaangalia wale wazalendo. Kama hakuna walendo badi kukaandaliwa mpango maalum wa kuwatafuta wanafunzi kutoka vijiji vile ambao watachukua mafunzo wakimaliza wakarejea katika vijiji vyao. Si hivyo tutaendelea kulalamika. Kuna daktari ambaye anasafiri kutoka kisiwa kimoja kwenda chengine, anakwenda katika kisiwa lakini anapofika ni saa 5 anakwambia anachelewa maji yamemtoka, itabidi nirudi, kwa hiyo hizo huduma hazipatikani.

Mhe. Spika, naondoka Mkoani nakuja Taifani sasa. Mhe. Spika, tuna kitengo chetu cha Tiba za Asisi, tumeamua kwa makusudi kwamba ili tusaidie afya zetu tumeweka vitengo hivi. Watu hawa tumewaruhusu ili wafanya kazi za kusaidiana na madaktari. Mimi wasi wasi wangu ni mmoja kutokana na wengi wa taaluma tulizonazo wananchi nahofia kwamba tutafika wakati wananchi tutasahau kwenda mahospitali na tutawaelekea watu hawa. Watu hawa mara nyingi wanakuwa ni watu wa biashara. Yeye bila shaka atatukueleza kwamba wewe unatatizo kwa hivyo utaendelea kulilea tatizo lile ifike hadi liwe ni *chronic* kwamba hata utakapokwenda hospitali basi wewe utakuwa tayari umeshamalizika.

Je, Mhe. Waziri hawa ambao tumewapa kazi hii tunawapitia na tunawaangalia na tunawapima uwezo wao kwa kutoa biba hizo au tunawaachia tu wanaendelea na tiba baadaye wanakuja kutusababishia mzigo mkubwa katika mahospitali yetu.

Mhe. Spika, kuna safari ambazo wagonjwa wanapelekwa. Safari hizi za nje ningependa kujua tu labda katika watumishi wa umma na wananchi pamoja na viongozi, ni wepi ambao wanapata huduma hii kwa wingi zaidi, ni viongozi au ni wananchi wa kawaida. Kwa sababu tunasikia kuna safari ya nje lakini ukiangalia utakutia ni daktari,

ni fulani ambaye kapata fursa ya kwenda nje. Je, kuna mgao au kuna sheha, ambayo inakuwaje kwa mfuko. Linapotoka fungu la kwenda nje ni wepi wanaoangaliwa zaidi, walionacho au waliokuwa hawana.

Mhe. Spika, katika hili ni kwamba mara nyingi tuna mazoea kwamba yule daktari ambaye anapeleka wagonjwa ndiye daktari bingwa katika hospitali zetu. Sasa inapotokea kwamba wagonjwa wanakwenda katika hospitali inaambiwa kwamba daktari bingwa kasafiri kenda kupeleka mgongwa. Je, kuna ulazima kwa daktari bingwa kwenda kupeleka mgongwa nje ya nchi. Hii inasababisha usumbufu, mimi ningependekeza au ningeonani ni vyema kwamba hawa madaktari bingwa wao mara zote wasiondoke, kama hakuna sababu maalum. Lakini leo imetumika kama ni kitega uchumi, anakwenda nani anakwenda Abdalla Mohammed, aah basi atafuatana na dokta fulani, kwa sababu anajua kwamba nitakaposafiri mimi kwenda kule basi nitapata chochote. Mimi nafikiri tabia hii tungeiwacha kabisa. Mhe. Waziri angeiangalia kwa kina wale wenaohusika kubakia wabakie.

Mhe. Spika, naomba nimalizie hapo.

Mhe. Asha Bakari Makame: Mhe. Spika, kabla ya yote nikushukuru wewe binafsi kwa kunipatia nafasi hii ya jioni ya leo kuchangia Wizara ambayo ni nyeti katika nchi. Naomba pia nichukue nafasi hii nimpongeze Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake wote ambao wamempangia kitabu hichi kwa ufasaha na kuweza kukisoma chote ingawa Mhe. Waziri alikunywa maji mengi, ndio mambo.

Mhe. Spika, nitakuwa mwizi wa fadhila kama sikuipongeza Kamati ya Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Wanawake na Watoto. Imeeleza mambo mengi ambayo haikuficha ili Wizara hii iweze kuyachukulia hatua.

Mhe. Spika, nije moja kwa moja katika vituo vya watu binafsi. Mimi nakaa najiuliza hivi vituo vya watu binafsi hawa madaktari wanatokea wapi. Ni madaktari wambao wametoka nje, ni madaktari wametoka humu humu, hawa wetu wa hospitali ya Mnazi Mmoja kila mmoja ana hospitali yake. Nitamuomba Mhe. Waziri aje anipe kinaga ubaga, kwa nini nikazungumza suala hili Mhe. Spika.

Tunapata shida sana unapokwenda hospitali, baadhi ya wakati madaktari huwa hawapo, lakini kumbe mtu ana hospitali yake nje anafanya kazi zake nje. Nitamuomba sana Mhe. Waziri, aje anipe ufafanuzi mzuri. Je, madaktari hawa wanapatikana wapi. Ndio maana saa nyengine haya madawa madawa utasikia hospitali hakuna. Yatakuwepo wapi hapo nafumbia.

Mhe. Spika, nije katika kisiwa cha Pemba, kwa kweli matatizo nitasema ki kwetu kemvu kemvu. Vituo vyote vya Kisiwa cha Pemba madaktari ni matatizo. Wala siwaiti madaktari ndiyo hayo aliyoyasema Mheshimiwa aliyemaliza sasa hivi. Mimi namuomba Mhe. Waziri, hebu akae kipindi cha mwaka huu ambao mwaka ujao, aorodheshe hospitali zake zile za vituo. Aangalie uwezekano gani ambao utaweza kumsaidia kuhakikisha angalau kila kituo kuwe na madaktari. Maana yeyote anayetibu kwetu sisi Wapemba tunamwita ni daktari, hata yule *older* yeye anamuona ni daktari. Ahakikishe anajipangia ili kuhakikisha kwamba wagonjwa wetu wanaokwenda kutaka matibabu hawasumbuki.

Mhe. Waziri, namuomba sana hili akae na wizara yake na maafisa wake ajiandae. Pahala popote tunapopeleka kituo cha Afya basi miundombinu ni muhimu, miundombinu ya madawa, ya njia na mengineyo. Kubwa zaidi ni nyumba ambazo wataishi wahudumu wa kituo kile katika mahala pale pale. Namuomba sana Mhe. Waziri juu ya hili.

Mhe. Spika, nije katika hospitali ya Wete. Kitabu kimeleza hichi kwanza niwapongeze katika sehemu ya kuzalia ni nzuri sio mbaya. Wodi ya wazazi ni matatizo, nitamuomba Mhe. Waziri ingawa kitabu chake kimezungumza vizuri, lakini nitamuomba sana kwamba ahakikishe kwamba wodi ya wazazi ya Hospitali ya Wete inajengwa na kumalizika, uzazi ni kitu chengine.

Nikija hapa Zanzibar wodi ya Wazazi Mhe. Waziri wewe mwenyewe huoni kama imeshakuwa ndogo watu wanalala watatu watatu, wengine wanabiringitia chini na uchungu wa uzazi siye wanawake ndio tunaoujua. Tafadhali naomba tufanye kila njia kwamba wodi ya Wazazi ya Zanzibar imeshakuwa ndogo. Tukiacha Hospitali ambayo tunaita ya Wazazi Mwembeladu. Pale Makao makuu hasa kwa kweli wodi ile imeshakuwa ndogo mno. Tunaomba mkae, mtafakari, mtizame ni aina gani ya kuweza kusaidia ile wodi ya wazazi ya Zanzibar.

Mhe. Spika, nikija hapo nitamuomba Mhe. Waziri ni vizuri sasa hivi tubadilike, wale watoto wetu ambao wanasoma Chuo cha Afya Mbweni mikataba yao lazima tuiandike mtu anakotoka ndiko atakokwenda kufanya kazi, tuna matatizo watoto wetu tunawasaidia lakini baadae ukimrejesha Pemba anaona kama umemtupa. Mimi naomba Mhe. Waziri isipokuwa pale kama kuna haja basi mikataba iandikwe, kama umetoka Tumbatu wende ukasaidie watu wa Tumbatu, kama umetoka Mtambwe wende ukasaidie watu wa Mtambwe isipokuwa kama kuna matatizo ya aina. Kwa sababu tukubali vijana wetu wengi wametoka Pemba wamesomeshwa hapa katika Chuo cha Mbweni wengine wamekataa kurudi, lakini upande mwingine siwalaumu kwa sababu hakuna nyumba mtu atumie pesa ile ile ya mshahara apande gari siku nyengine shilingi elfu tatu anakwenda kituo alichopangiwa.

Kwa hivyo, nakuomba Mhe. Waziri hili mkae mlizingatie muandike angalau kipengele hicho ili kuweza kusaidia watu wetu ambao wanakaa sehemu mbali mbali za miji.

Lakini Mhe. Spika, nje katika suala la mazingira ya sasa ya Hospitali yetu ya Mnazi Mmoja. Mimi kwa kweli Mhe. Spika, hayaniridhishi mazingira yake si mazuri tuseme ukweli, mazingira yake hayaridhishi si nje si ndani. Nakuomba Mhe. Waziri kwa sababu ile Hospitali ya Mnazi Mmoja ndio kioo cha Zanzibar ndio tunayoiita Hospitali Mama ile, pamoja na matatizo yote, mimi sitaki kuingia kwenye mafungu aa, lakini nasema tu kwamba hebu tuipe hadhi ya kwamba mtu akenda pale roho yake inaridhika. Lakini mgonjwa unakwenda saa nyengine unataka kutapika japo si maradhi ya kutapika, naomba sana tufanye kila jitihada Mhe. Spika, Hospitali ya Mnazi Mmoja kwa kweli tuipe hadhi yake, sitaji sehemu mana mimi nakuwa nakwenda sana pale na wagonjwa na katika mtu ambaye sipendi kuchukua madaraka ni mimi, kwa sababu nikihadithia hayo mambo yaliyonifika lakini aa, nawaacha bora nisiseme.

Mhe. Spika, kwanini nikaipongeza Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii kwa sababu baadhi ya mambo mengi sana imenifilisi, kwa hivyo nisiyarejee rejee.

La mwisho kwanza nimpongeze Mhe. Rais kwa imani yake ambayo ameitoa kwa akina mama kwa ajili ya ujauzito kwamba wasilipe, lakini ninaiomba Serikali kwa sababu Kiongozi Mkuu wa Serikali yupo hapa naiomba sana Serikali huduma za watoto naiomba Serikali watoto wasilipe huduma ya afya. Nasema tena Mhe. Spika, naiomba sana Serikali mpaka afike umri angalau kwa sababu mtoto hana uwezo na mama saa nyengine ana watoto sita mpaka saba, hana uwezo wa kuwalipia. Kwa hivyo, ninaiomba sana Serikali iangalie, itafakari, ikae kwa makini Mhe. Spika, ili kuwe na uwezekano watoto kutolipishwa.

Kwa sababu huko nyuma tulisema afya bure, skuli bure, maji bure, pamoja na kwamba sasa hivi tunatakiwa tuchangie kidogo lakini si kwa watoto Mhe. Spika. Kwa hivyo, suala hili namwachia mwenyewe Waziri akae alitafakari ili kuweza kumsaidia mtoto zaidi katika huduma za afya. Baada ya kusema hayo nilisema na mimi nigusie gusie tu Wizara hii Wizara nyeti, nisema naunga mkono hoja na namtakia kila la kheri Waziri wa Afya pamoja na naibu wake ili katika majumuisho Mwenyezi Mungu awasaidie waweze kujibu vizuri. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kusema mawili matatu yahusianayo na Wizara hii muhimu. Naomba kwanza nianze kwa kumpongeza sana Mhe. Waziri pamoja na Naibu Waziri kwa namna wanavyojitajidi kuisimamia Wizara hii ambayo kama walivyosema wenzangu ni Wizara mama na ni Wizara inayomgusa kila mtu. Mafanikio ya Wizara hii yametokana pia na ushupavu wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii ambapo muda mwingi kamati hufanya kazi kwa namna mbalimbali ya kuishauri Wizara katika kutekeleza majukumu yake. Kwa hiyo naomba pongezi zangu pia ziende kwa Kamati chini ya uongozi wa Mwenyekiti wa Kamati hiyo.

Mhe. Spika, baada ya pongezi hizo sasa naomba nianze kwa utangulizi wa kusema kwamba, ripoti nyingi za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali zinaonesha kwamba Wizara ya Afya inaongoza katika kuwa na matumizi yasiofuata utaratibu, hasa kwenye miradi. Kwa hivyo, wanapokuja hapa kutuomba fedha Waheshimiwa Wajumbe tuna wajibu wa kuona kwamba fedha tunazozidhinisha matokeo yake ni kutumiwa pasina kufuata utaratibu.

Hili ni angalizo kwa Mhe. Waziri kama msimamizi lakini Katibu Mkuu kama mwenye dhamana ya fedha hizi ambazo tutamuidhinisha. Mategemeo ya Baraza hili ni kuona kwamba fedha tunazozidhinisha ziende katika malengo ambayo tumekusudia kwa maslahi ya wananchi. Huo ulikuwa ni utangulizi.

Mhe. Spika, hapana shaka kwamba Wizara hii ni muhimu sana, hakuna yeyote kati yetu na wale walioko nje ya ukumbi huu aliyekuwa haguswi na Wizara hii ama moja kwa moja au kwa njia nyengine, lakini kwa vyovyote Wizara hii inatugusa sote. Kwa sababu haipati muda kila mtu anategemea ripoti kule kwa ajili ya kwenda kupata matibabu. Kwa msingi huo basi Serikali pamoja na Baraza hili linapaswa tuelekeze nguvu kubwa sana kuona kwamba Wizara ya Afya inawezeshwa kadiri inavyowezeshwa ili kufikia malengo yaliyokusudiwa na Serikali. Kwa hivyo, mimi binafsi nasema maendeleo ya sekta ya afya ingelikuwa ningeambiwa kwamba fedha hizi zichukue na uzipange katika kipaumbele basi ningeliweka maeneo manne Mhe. Spika, kama yafuatayo:-

Kwanza tungeliwekeza sana katika ujenzi wa Mahospitali pamoja na vituo vya afya kwa sababu bila ya kuwa na hospitali pamoja na vituo vya afya hatuwezi tukafanya chochote kinachohusiana na haya. Hii ni katika kukamilisha lile lengo la kwamba wananchi wasisafiri umbali usiozidi kilomita tano na kufikia hatua hiyo.

Mhe. Spika, katika hatua hii naomba niipongeze Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa namna walivyoweza kulitekeleza hili, sina takwimu sahihi lakini kwa utafiti mdogo tu tuliofanya inaonekana sasa hivi wananchi wetu hawawezi kusafiri zaidi ya kilomita tano kabla ya kupata huduma ya afya. Kwa hivyo, naipongeze Serikali katika juhudi hii pamoja na wananchi kwa kufikia hatua hiyoi.

Naungana na agizo au wazo alilolitoa Mhe. Waziri kwamba inaonekana kuwa ujenzi wa vituo vya afya sasa hivi tufike pahala turidhike na vituo vya afya tulivyonayo. Hakuna haja tena kutenga fedha nyengine wala kutumia fedha nyengine kwa ajili ya kujenga vituo, mimi nadhani kuna mambo mengine ya msingi sana ambayo tunapaswa kuelekeza nguvu zetu huko.

Lakini wakati Waziri akitoa kauli hiyo kuna *case study* moja ambayo nimeifanya katika jimbo la swahibu yangu hapa Mhe. Haji Faki Shaali, MBM; kwamba ndani ya jimbo lake la Mkanyageni kulikuwa kuna vituo viwili Kisiwapanza na Bogoa. Katika vituo vyote hivyo ukichukua hiki kituo cha Bogoa ambacho kiko juu watu katika jimbo zima walikuwa hawasafiri zaidi ya kilomita tano kukifika kile kituo, katika kila kona utakayokwenda katika Jimbo la Mkanyageni. Lakini sasa hivi kuna ujenzi wa Kituo cha Shidi ambacho ni kama kilomita mbili na nusu kutoka Bogoa mpaka hapo kwenye kituo.

Kadhalika kuna kituo cha Michenzani kama kilomita mbili na nusu kutoka Michenzani na Bogoa, kadhalika kuna kituo cha Tasini ni kama kilomita mbili na nusu kutoka Bogoa na kwenda Tasini. Sasa hiyo utaona ni namna gani ambavyo kwamba hilo agizo linakiukwa, tutafika pahala kwa kweli itakuwa ni kila nyumba kumi kunakuwa na kituo cha afya.

Sasa Mhe. Waziri wakati ukitoa kauli hiyo lakini Wizara yako sasa hivi ndio inayofanya hivyo katika kujenga vituo katika masafa hayo, sasa hatuelewi kwamba Mhe. Haji unampendelea kwa kiasi gani kumjengea vituo hivi katika kila nyumba kumi manaake nadhani utafikia huko, kwamba kila nyumba kumi pawe ana kituo cha afya. Nadhani sera hiyo na mpango huo Wizara ya Afya hawana budi ku-*review*. Mimi nadhani inawezekana kwamba Kituo cha Bogoa sasa hivi ni kukifanyia uboreshaji zaidi na kuona kwamba tunapeleka madaktari sio kujenga vituo katika kila balozi. Kwa hivyo, naomba Mhe. Waziri utakapokuja uniambie kwa nini ukafanya hivyo na wakati majimbo mengine unatuzuwia na sisi tumekubali. Kwa hivyo hiyo ni *case study* ambayo nilisema niyarudie maneno yako Mhe. Waziri kwamba ikiwa unasema hivyo lakini upande mwengine katika majimbo ya maswahiba zako unafanya vitu kama hivyo.

Jambo la pili Mhe. Spika, ambalo nadhani lilikuwa ni muhimu, baada ya kujenga vituo vya afya pamoja na hospitali ilikuwa kwa kweli tuelekeze nguvu zetu katika kuwa na madaktari, wauguzi, *nurses* na vitu vingine. Kwa sababu hata tukawa na vituo vizuri kama hatujawa na wataalamu hawa itakuwa kazi yetu ni bure na katika hili naomba kwa mara nyengine tena niipongeze Serikali kwa namna inavyojitahidi kuwasomesha watu wetu hawa. Lakini tatizo linaendelea kubakia pale pale, kwamba Serikali inajitahidi wataalamu hawa wakifika hapa wanaondoka.

Juzi nilikuwa nazungumza na jamaa akanambia kwamba wauguzi wanaosomeshwa katika chuo chetu hapo zaidi ya asilimia 70 wanatorokea Bara, sijui lina ukweli kiasi gani nadhani baadae Waziri atakapokuja yeye ndiye anayeweza akatupa ufafanuzi. Lakini kama hivyo ndivyo kwamba zaidi ya asilimia 70 wauguzi sijui *clinical officers* na wengine wanakimbia kwa kweli tutakuwa hatufanyi kitu cha maana hata kidogo na tutakuwa fedha tunazozitumia, nguvu kubwa tunazotumia kwa ajili ya kuwasomesha hawa zitakuwa hazina tija yoyote, na kama utafanya tathmini

pengine utaweza kuona kwamba wanachokimbilia ni tofauti ya shilingi laki moja tu, hicho wanachokifuatia huko Bara na hicho wanachoondokea hapa ni tofauti ya shilingi laki moja tu.

Kwa hivyo, katika hili basi naiomba Serikali iangalie gharama inayochukua katika kuwasomesha vijana na namna gharama inayopoteza katika watu hawa kutukimbia, ikiwezekana Serikali ifanye kadiri inavyowezekana tofauti iliyopo hiyo kwa wataalamu wetu hawa irekebishwe ili kuendelea kuhifadhi fedha za umma. Kwa sababu kumsomesha mtu kwa fedha nyingi lakini akakukimbia kwa shilingi laki moja hiyo itakuwa ni mchezo wa kitoto. Naiomba Serikali ifanye kadiri inavyowezekana iweze kuwabakisha wataalamu hawa na wananchi wetu wafaidike.

Jambo la tatu Mhe. Spika, ambalo nadhani lilikuwa ni muhimu ni suala zima la kuwa na dawa za kinga na tiba. Kadiri tutakavyotenda katika masuala haya kama hatuna dawa za kinga na tiba itakuwa kazi yetu ni bure.

Katika bajeti hii imeoneshwa katika kila fungu unalokwenda kuna fedha zimetengwa kwa ajili ya ununuzi wa dawa, lakini tatizo linalojitokeza Mhe. Waziri unapokwenda katika vituo vyetu kwa kweli dawa hazionekani. Miaka ya nyuma nilikuwa nikiliuliza suala hili mara kwa mara Serikali inafanya nini? Kwa sababu Serikali inatuhakikishia kwamba dawa ziko lakini wananchi wanapokwenda dawa hazionekani, sasa hapo ilikuwa Serikali iweke mkono wake kwamba ikiwezekana itoe *circular* na iwaambie wananchi kwamba wananchi tunachowaambia kwamba katika kipindi cha mwezi huu dawa hii na hii inapatikana bila ya malipo yoyote.

Mhe. Spika, nadhani katika masuala ambayo kipindi cha nyuma tulikuwa tukiuliza moja ni hilo la kuiomba Serikali pale inapopata dawa iweze kuiambia jamii kwamba dawa fulani na fulani zinapatikana hospitali. Lakini sasa nyinyi Wizara mkikaa kimya wananchi wetu wakienda kule hakuna dawa nani atakaekuwa anawasaidia wananchi na tayari Baraza hili Mhe. Spika, lishaidhinisha fedha kwa ajili ya ununuzi wa dawa.

Kwa hivyo, katika kupitisha fungu hili sitoweza kupitisha mimi mmoja mpaka Serikali inambie kwamba inajiandaa vipi kuhakikisha kwamba fedha tunazoziidhinisha kwa ajili ya ununuzi wa dawa Serikali wataziratibu vipi kuona dawa hizi zinawafikia wananchi masikini.

Mhe. Spika, na jambo jengine ambalo tulipaswa jambo la nne nilisema mambo manne kuwekeza sana katika Sekta ya Afya ni suala la elimu ya afya. Mhe. Spika, elimu ya afya ni suala muhimu sana, laitani Wizara ingelikuwa inajitahidi kutoa elimu ya afya maradhi mengi ya kijinga jinga haya yangeliondoka na hivyo taifa lingelihifadhi fedha nyingi sana. Kwa sababu kuna maradhi kwa kweli ni matatizo yetu sisi wenyewe tu kuwepo, mathalani tungelielimishwa kuhusiana na suala la usafi na mazingira na elimu hiyo ikawafika wananchi na wananchi wakaikubali elimu hiyo maradhi kama vile matumbo, malaria, kipindupindu yasingekuwepo. Leo tujjulizeni ni kiasi gani taifa linapoteza fedha nyingi kwa ajili ya maradhi kama hayo ambayo yana uwezekano kabisa kabisa kutibika.

Kwa hivyo, napendekeza pamoja na mambo mengi yaliyomo katika Wizara, elimu ya afya ni suala la msingi sana. Mhe. Spika, laitani tungelikuwa na elimu ya lishe, elimu ya lishe ni elimu kubwa sana, laiti tungelikuwa na elimu ya lishe basi mambo ya watoto wetu kuwa na utapia mlo, mambo ya kinamama kukosa damu wakati wa kujifungua, mambo ya *pressure*, mambo ya kisukari, magonjwa yote hayo ni kutokana na mambo ya ukosefu wa lishe watu kufakamia fakamia tu mapweza, madude gani, mtu utamkuta anafakamia tu siku mbili tatu *pressure*, kisukari na vitu vingine, laitani tungelikuwa na elimu mambo kama haya yanawezekana kabisa kabisa Mhe. Spika, kuweza kuyaondoa.

Mhe. Spika, baada ya kueleza hayo yanayohusiana na maendeleo ya afya sambamba na uelekezaji wa nguvu kubwa ya Serikali katika kuimarisha hii sekta ya afya sasa niangalie kwa ufupi sana suala la mpangilio wa bajeti.

Mhe. Waziri nakupongeza kwamba ulipotuletea mafungu haya kwa kweli yanasomeka vizuri, hayatishi sana. Sasa kutokutisha sana maana yake sisi wajumbe hayatutishi lakini yanatutisha kwamba mafungu yako mengi yamekonda kiasi cha kwamba unaweza kufika pahala ukajiuliza kulikoni. Kwa kweli sikufanya kazi vizuri sana lakini inaonekana labda niseme ni *reasonable* kwetu sisi wapitisha bajeti, isipokuwa tu kuna kitu kimoja kinatutesa suala zima linalohusiana na posho za vikao na kamati Mhe. Spika, bado inaendelea mimi binafsi kunitisha.

Mathalani Ofisi Kuu Pemba umetenga shilingi 4.2 milioni kwa ajili ya posho za vikao na kamati, yuko Waziri mmoja nilimuuliza hivi vikao, vikao gani na kamati gani, au ni zile kamati zetu zinapokwenda kule huwa

linaandaliwa posho lakini hatuoni. Kwa hivyo, hii Ofisi Kuu Pemba shilingi 4.2 milioni Idara ya Mipango na Sera shilingi 30 milioni. Shilingi 30 milioni kwa ajili ya vikao vya kamati sijui na nini, Idara ya Uendeshaji mmetoka shilingi milioni tatu mpaka 24 milioni tofauti kubwa, mara hii mmepanga vikao vipi maana yake kutoka shilingi milioni tatu za mwaka jana mpaka 24 milioni za mwaka huu.

Idara ya Kinga kuna shilingi 20 milioni, Hospitali ya Mnazi Mmoja kuna shilingi 45.4 milioni, posho za vikao na kamati mnazungumza nini. Pahala penye Wizara maana yake kunakuwa na mipango watendaji kazi yao ni kufuata mipango, inapotokezea kufuata ni namna ya kutathmini tu. Sasa hizi posho za vikao posho za vikao ni Baraza la Wawakilishi ndiko kwenye kamati pamoja na vitu kama hivi. Sasa naomba katika suala la utendaji Mhe. Waziri atakapokuja atwambie.

Katika hapo hapo humu sikuona sana mambo ya ununuzi wa majarida na magazeti, lakini katika Wizara nyingi zilizopita kuna majarida na magazeti na hapa najiuliza tena suala jengine, huu utaratibu wa bajeti unakuwaje kwamba wizara nyengine iwe na *item* hii, wizara nyengine kuwe hakuna *item* kama hizi, hivyo nyinyi hamsomi magazeti? Kwa nini wizara nyengine kuwe kuna kusomwa magazeti.

Mhe. Spika, nilikaa na Dr. Salmin hapa kuna idara moja fedha zilizotengwa kwa ajili ya ununuzi wa magazeti tulipiga hesabu katika idara tukapata kwa siku yanatakiwa yanunuliwe magazeti 90 Zanzibar Leo, idara moja tu. Tukapiga hesabu kwa mwaka, tukaja kwenye mwezi mpaka kwa siku tukakuta kwamba gazeti la shilingi 400 la Zanzibar Leo yanatakiwa kwa fedha zilizotengwa magazeti 90 katika idara moja tu.

Mhe. Spika, ofisi yako hii kuna gazeti moja hapo juu na magazeti sijaingia katika ofisi yako, lakini na gazeti moja katika ofisi ya Katibu, magazeti mawili, maofisi mengine yote sioni hata kama yapo basi hayazidi sita. Lakini idara moja kuna magazeti zaidi ya 90 sasa na hii vile vile najenga hofu huu upangaji wa bajeti unakuwaje kwamba katika wizara moja kuwe na hii wizara nyengine kusiwe na vitu kama hivyo.

Mhe. Spika, naomba niulizie suala tunacho kituo kimoja kizuri sana *PHL* Pemba, kituo hiki kwa kweli ni fahari ya Zanzibar kwa sababu kituo kama hiki katika Afrika ya Mashariki nasiki kipo katika nchi yetu. Lakini tulipokwenda walitulalamikia kwamba ile *dividend* ya Serikali haiingii pale kama inavyopaswa, wafadhili pekee ndio wanaopeleka tu fedha lakini gawio la Serikali halilingii. Sasa Mhe. Wazairi hebu naomba utakapokuja kwa nini kile kituo ambacho ni kituo kizuri tumesaidiwa lakini kwa nini mgao wa serikali hauingii katika kituo kile. Hatuoni kwamba ikiwa hatukupeleka fedha zile tunawavunja moyo wanaotusaidia.

Sambamba na hilo kituo kile kwa vyovyote vile kwa sababu nchi nyingi huja zikafanya utafiti je, kituo kile hakizalishi fedha kuingia Serikalini, au wanachopata hula wao wenyewe, maana yake ndio Serikali hamtoi. Kwa hivyo, hilo naomba utakapokuja unijibu.

Lakini la mwisho Mhe. Spika, naomba niseme kwamba hospitali zetu zimejengeka kwa daraja, tuna *referral hospital*, tuna hospitali za Mkoa na Wilaya. Katika Pemba tuna hospitali mbili za mkoa na tuna hospitali nyengine za wilaya. Hospitali ya Mkoani ni hospitali ya Mkoa ya Vitongoji ni ya Wilaya, ile ya Chake Chake bado mimi hoja yangu iko pale pale, ile Hospitali ya Chake Chake iko katika daraja gani, si yangu kama ni ya jimbo semeni tu ni ya jimbo nijue mwenyewe vya kufanya.

Na jambo la mwisho Mhe. Spika, naomba nimalizie kwa kusema kwamba pamoja na mapungufu tuliyonayo katika Hospitali yetu ya Mnazi Mmoja *ICU* lakini kwa mgawanyiko wa visiwa vyetu hivi viwili Pemba tunahitaji kuwa na *ICU*, wagonjwa mahatuti hutokea Pemba na mtu akiwa mahatuti huwezi tena kumhangaisha, huwezi tena kumpanidisha Serengeti pamoja na Seagul, kwa vyovyote vile wagonjwa mahatuti Pemba wanatakiwa wabakie Pemba kwenye *ICU* Mwenyezi Mungu na rehema zake, kwa vyovyote vile na Pemba nako tunahitaji kuwa na *ICU* tena basi *ICU* hiyo iwekwe katika hospitali ambayo iko katikati ya kisiwa cha Pemba ni Chake Chake.

Mhe. Spika, nakushukuru sana.

Mhe. Nassor Salim Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi hii ya kuchangia kidogo hotuba ya Mhe. Waziri wa Afya. Mhe. Spika, kwana nichukue fursa hii kukupongeza wewe na kumpongeza Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi katika dhamira yake ya kuiweka Hospitali ya Mnazi Mmoja kuwa hospitali ya rufaa.

Halikadhalika Mhe. Spika, nimpongeze pia Mhe. Waziri katika kutekeleza vyema ilani ya Chama cha Mapinduzi katika kuleta mabadiliko katika Wizara ya Afya. Hospitali ya Mnazi Mmoja ndio hospitali ambayo tunaitegemea na katika dhamira hii ya kuibadilisha kuwa hospitali ya rufaa kuna changamoto kubwa au nyingi inazozifanya hospitali hii iwe hospitali ya rufaa.

Mhe. Spika, Hospitali ya Mnazi Mmoja kuna mambo mengi ambayo yanahitajika kufanywa ili kuweza kufikia kuwa Hospitali ya Rufaa. Katika taarifa yake Mhe. Waziri ameeleza pia changamoto na matatizo makubwa ambayo yako katika hospitali ile, moja ambalo nataka kulisema na ambalo liko katika ukurasa wa 41 ni ile sehemu inayosema kwamba, moja kati ya tatizo sugu la Hospitali ya Mnazi Mmoja ni msongamano mkubwa wa jamaa wa wagonjwa wanaokuja kuwatazama au kuwasaidia kuwapa huduma wagonjwa wao na hio inatokana na upungufu wa wauguzi kuweza kukidhi wingi wa huduma za wagonjwa kwa wakati.

Mhe. Spika, kweli hili ni tatizo na tatizo sugu, lakini Mhe. Spika, nimeshawahi kutembelea pale katika Hospitali ya Muhimbili Dar es Salaam na hospitali nyengine katika nchi mbalimbali. Hospitali za rufa huwa na utaratibu mzuri tu wa kuweza kujenga maeneo ya kuwahudumia wale wananchi au wenye wagonjwa wao wanapokwenda kuwaangalia na kutoa huduma nyengine. Sasa Mhe. Spika, ningemuomba Mhe. Waziri kwamba ipo haja ya kujenga eneo maalum katika Hospitali ya Mnazi Mmoja ili wale wanaokwenda kuangalia jamaa zao, ndugu zao, watoto wao, wazee wao, kabla haujafika wakati wa kuwaangalia wagonjwa wale basi kuwe na mahali ambapo wanafikia na kuwe na utaratibu maalum ambao utakuwa unawekwa pale ili kuondoa msongamano ule.

Suala la pili Mhe. Spika, nataka kuzungumzia Hospitali ya Mwembeladu, hospitali hii ni hospitali ambayo kwa kweli ina mchango mkubwa katika kusaidia kinamama wetu wajawazito wanaokwenda kujifungua pale, ili kuondoa msongamano katika Hospitali ya Mnazi Mmoja.

Mhe. Spika, katika taarifa yake Mhe. Waziri amesema kwamba kwa dhamira ya kupunguza msongamano unaotokea katika hospitali kuu ya Mnazi Mmoja, imekusudia kuimarisha huduma hospitali hii kwa kuipatia madaktari bingwa wa uzazi ili iweze kutoa huduma ya upasuaji. Hiyo ni Hospitali ya Mwembeladu Mhe. Spika.

Mhe. Spika, hospitali hii katika kiambatanisho nambari 8 kinaonesha pale kwamba ni wazazi karibu 2871 wanachukuliwa pale katika mwaka mmoja, halikadhalika wanaozalia katika njia za kawaida takriban 2545. Sasa inaonesha ni wazi kwamba hospitali ya Mwembeladu inasaidia sana na inaondoa msongamano mkubwa, lakini sasa tatizo kwamba hospitali ile haina daktari bingwa na haina huduma ya upasuaji. Sasa kama kungekuwa na daktari bingwa na huduma hizi za upasuaji basi ingelipunguza zaidi msongamano katika Hospitali ya Mnazi Mmoja. Kwa hivyo ningelimuomba Mhe. Waziri basi ajitahidi apatikane daktari bingwa pale na kuweka huduma hizi za upasuaji.

Nikiendelea Mhe. Spika, nije katika Bodi ya Chakula, Dawa na Vipodozi. Mhe. Spika, katika ukurasa wa 23. Bodi hii ya Chakula na Vipodozi Mhe. Spika, imezungumzia masuala ambayo wale ambao wamechunguzwa, kuna maduka, *super markets* ambazo zimeangaliwa, kuna vyakula mbali mbali vimeangaliwa ambavyo vimepitwa na wakati. Lakini Mhe. Spika, ukenda hapa katika *super markets* ambazo tunazo katika mji wetu wa Zanzibar utakuta kwamba kuna vyakula ambavyo vimefikia kumaliza muda, siku mbili kabla ya kumaliza muda wake yaani *expiry date*, kuna tabia ambayo imekuwa ikiendelea ma-*super market* haya kwa kuweka bei ya *sale* pale kwa kuuzia wananchi wetu vyakula vile ambavyo tayari vimekwishakupitwa na wakati.

Sasa hili ningemuomba Mhe. Waziri kuhakikisha kwamba suala hili linachukuliwa hatua kwa wale wanaofanya tabia hizo na kuondolewa wananchi wetu kupata vyakula ambavyo vimekwisha muda wake.

Mhe. Spika, hili ni tatizo sugu ingawa niipongeze Bodi hii ya Vyakula na Vipodozi kwa kazi nzuri waliyoifanya kwa kuweza kutambua ule mchele mbovu ambao ulionekana na kuweza kurejeshwa huko ulikotoka, na hii ni kazi nzuri ambayo imefanywa na Mhe. Waziri pamoja na Mhe. Naibu Waziri wake na watendaji pamoja na Bodi hii kuhakikisha kwamba wananchi wanapata vyakula vilivyo bora na vyenye lishe, Mhe. Saleh Nassor amekuwa akilisemea sana hili wananchi kupata lishe bora. Kwa hivyo Mhe. Spika, suala hili Mhe. Waziri alichukulie kwa kina kabisa na kuweza kulifanya kazi kuhakikisha kwamba tunapata chakula bora.

Mhe. Spika, kwa kumalizia na mimi niende katika suala hili la madaktari. Mhe. Spika, madaktari wetu kwa kweli wamekuwa wakikimbia na kwenda kufanya kazi katika nchi mbali mbali ikiwemo Tanzania Bara na nchi nyengine.

Hili limekuwa ni tatizo, serikali imekuwa inapoteza fedha nyingi za kuwasomesha lakini siku ya siku utakuta vijana au madaktari wetu wanakwenda na kufanya kazi katika nchi mbali mbali. Kwa hivyo ningelimuomba Mhe. Waziri pamoja na serikali kwa ujumla, kuhakikisha kwamba madaktari wanapata mishahara inayostahiki ili kuweza kusaidia na kuweza kutumia ile taaluma yao kwa kuwahudumia wananchi wetu.

Baada ya kusema hayo Mhe. Spika, mimi kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Rahaleo, naunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja. (Makofi).

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Spika, ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuendelea kuturuzuku neema zake tukiwa hai na wazima wa afya, na hivyo kutuwezesha kuendeleza shughuli hizi za Baraza letu kujadili mambo yanayogusa wananchi wetu.

Mhe. Spika, nikushukuru na wewe kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia na mimi katika bajeti hii ya wizara muhimu kwenye wizara za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Wizara ya Afya.

Lakini tatu nimpongeze Mhe. Waziri wa Afya Mhe. Juma Duni Haji na timu yake yote ya watendaji kwa kazi nzuri ambayo wameifanya. Mimi ninaamini kuingia kwa utendaji makini wa Chama cha Wananchi CUF kuongoza wizara hii, kumesaidia pakubwa sana kubadilisha utendaji katika wizara hii, na kwa hilo ninataka nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa kupeleka ule umahiri na umakini wa ki-CUF aliozoea pale Makao Makuu alipokuwa Naibu Katibu Mkuu akaupeleka katika uongozi wa wizara. Mhe. Spika, mabadiliko yameweza kuonekana kwa sababu kwa muda mrefu wizara hii ilikuwa na matatizo mengi. (Makofi).

Mhe. Spika, naomba vile vile nimpongeze Mhe. Waziri sio tu kwa bajeti yake na mafanikio ambayo ameyataja, sina muda wa kuyataja ili kuokoa muda kuyataja hapa yanajieleza wenyewe, lakini ninataka pia nimpongeze kwa utayarishaji mzuri wa bajeti yake, kwa maana ya vifungu mbali mbali. Hii ninampongeza yeye na watendaji wake wakiongozwa na Katibu Mkuu.

Mhe. Spika, wewe ni shahidi tangu tumeanza tumekuwa tukikosoa vifungu vingi katika bajeti mbali mbali. Leo asubuhi nilipopewa *bundles* tatu hizi, kidogo nilishtuka nikawa sijui nikamate ipi lakini hatimae nikagundua kumbe ilikuwa katika kujumuisha tu lakini zinafanana zote. Lakini hata nilipolinganisha katika lile buku kubwa ni maeneo mawili hasa yaliyokuwa yana marekebisho, maeneo mengine yote ni sawa.

Kwa hivyo ni kusema kwamba si kama maeneo haya yalirekebishwa baada ya kuona watu wanapiga kelele humu. Kwa hivyo hili ninataka kuwapongeza kwamba wamefanya kazi nzuri. Hata vile vifungu ambavyo wengi tumekuwa tukivihoji, hivi huvikuti vimenona kama ambavyo vimekuwa katika wizara nyengine, lakini vipo vifungu vichache sitaki kupoteza muda kuvirejea kwa sababu Mhe. Omar Shehe ameshavigusia, nitaomba na mimi niingie tu kwenye *record ya hansard* kwamba Mhe. Waziri akija atusaidie maelezo katika vile.

Katika idara nyingi hasa idara ya Mipango na utafiti, unakuta kidogo kuna mambo hayo na vile vile katika Hospitali ya Mnazi Mmoja. Kwa hivyo ninadhani akija atusaidia Mhe. Spika.

Lakini katika kumalizia shukurani Mhe. Spika, itakuwa sitendi haki kama sikuwapongeza kamati ya Ustawi wa Jamii ya Baraza lako Tukufu kwa kazi nzuri waliyoifanya. Kwanza kuweza kugundua uvujaji wa mapato ambao haukujumuishwa katika wizara hii. Na mimi ninataka niseme kwamba imeonekana tofauti Mhe. Spika, ukiangalia buku la *expenditure* la mwanzo, ilikuwa imekisiwa wizara hii kukusanya shilingi mia nane na tano milioni laki tano, lakini marekebisho tuliyoletewa pana mia tisa na tisini na tano milioni laki tano, maana yake pamegundulikana mia moja na tisini milioni na ziada zinaweza kupatikana zikaingia pale. Hiyo ninataka niwapongeze wamefanya kazi nzuri. (Makofi).

Lakini vile vile Mhe. Spika, ninadhani na marekebisho ya kamati, nimevutiwa mno katika bajeti ya Hospitali ya Mnazi Mmoja kwenye fungu linalohusu operesheni lilikuwa na shilingi milioni saba laki mbili thamanini elfu, lakini katika marekebisho ambayo ndio pekee yaliyofanywa baada ya haya, pameongezeka hadi milioni mia moja thamanini na saba laki mbili thamanini elfu.

Haya yanaonesha umakini kwamba kumbe ushauri wa kamati unapokuwa na watendaji wasikivu na Waziri msikivu yalizingatiwa kuona kwamba wapi panapaswa kupewa kipaumbele. Mhe. Spika, ninaipongeza kamati kwa kusaidia

hilo na ninaipongeza wizara kwa kuwa wasikivu kwa kuyakubali marekebisho hayo ambayo walikuwa wameyafanya.

Mhe. Spika, kabla sijaondoka hapo nilikuwa ninasema hili la kwamba kamati imegundua mapato ya ziada ikaitanabahisha wizara, mimi ninadhani lisiishie hapa tu, tunapongeza kwa hatua hiyo lakini ninadhani Waziri akija atusaidie kwamba kama hivi kamati isingea mapato haya yalikuwa yanaingia mifukoni mwa nani ili tuwajue watendaji wasiokuwa waaminifu Mhe. Spika, tuwape fundisho, hatuwezi kukubali tena kwamba fedha za wananchi wetu maskini, mtu hana pesa anahangaika nyumba hadi nyumba kutafuta pesa ili akahudumie mgonjwa wake, halafu pesa hii haingii katika mapato ya serikali. Hili linaleta mashaka makubwa. Hivyo nilikuwa naomba Mhe. Spika, akija Mhe. Waziri anisaidie. (*Makofi*).

Mhe. Spika, naomba vile vile katika hilo la mapato ambalo Mhe. Omar Shehe amezungumza hapa kwamba ukiangalia ripoti za kamati, ripoti ya mwaka huu tuliypokea na tukaijadili hapa katika mwezi wa Machi/Aprili, nilichangia katika ripoti zile kwamba katika wizara ambayo inaongoza kwa kuwa na *queries* nyingi kutoka kwa Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na PAC wakathibitisha basi ni Wizara ya Afya.

Kuanzia fedha za ndani mpaka fedha za miradi ya maendeleo lakini hasa huku kuna mafungu mengi Mhe. Spika, nilimuomba siku ile Mhe. Waziri atusaidie majibu, akasema atayafuatilia. Nilikuwa ninadhani wakati huu ndio kipindi chake atusaidie Mhe. Waziri.

Hata zile fedha za washirika wa maendeleo, wakija hapa zikiingizwa hapa msaada kwa wananchi wa Zanzibar walipa kodi. Sasa kulikuwa kuna mafungu pale Mhe. Spika, mengi yalikuwa hayana maelezo kuanzia ukurasa wa 77 wa ripoti ya PAC wakati ule yalikuwa yapo, kwa mfano kulikuwa na malipo yasiyokuwa na stakabadhi shilingi milioni kumi na tatu laki tano na arobaini elfu, kulikuwa na hoja nambari 391.6, shilingi milioni tatu laki tisa sabini elfu, kwenye kitengo cha ukimwi kulikuwa na shilingi milioni tano laki tatu kumi na tano elfu, ule mradi wa *Zanzibar Age Control* kulikuwa na shilingi milioni tatu laki nne elfu kumi, kuhusu malipo yasiyokuwa na stakabadhi mengine ni milioni tatu, kwenye mradi wa kuzuia vifo vya mama na watoto kuna US Dollar 35,928.90, kwenye malipo yasiyokuwa na stakabadhi mengine ni US Dollar 51,600, kwenye mradi wa afya kitengo cha mama na mtoto pana shilingi milioni kumi laki nane arobaini tatu elfu.

Mhe. Spika, haya ni matumizi ambayo Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali alishindwa kupata vielelezo, na PAC wakenda kuthibitisha baada ya kufanya kazi yao, wakatuorodheshea katika ripoti hii na Mhe. Spika, hapa ndio Baraza linapofanya kazi yake. Kwa hivyo nilikuwa naomba Mhe. Waziri akija atusaidie kwamba maelezo juu ya vifungu hivi kwa sababu *otherwise* itakuwa hakuna faida kupokea ripoti ya kila mwaka, halatu tuna-*record* tunajadili, tunaweka upande tunakuja mwaka mwingine Mhe. Spika. Nilikuwa ninadhani tunahitaji kupata maelezo ya matumizi haya ili tuidhinishe fedha hizi nyengine kwa ajili ya mwaka huu.

Mhe. Spika, sasa niondoke kwenye mahesabu niende katika *sustentative issues*. Mhe. Spika, mimi nilikuwa napenda nianze kuungana mkono na wenzangu wote waliotoa maoni kuhusu suala zima la Hospitali ya Mnazi Mmoja. Ninataka nimpongeze Mhe. Waziri na watendaji kwa sababu itakuwa hatutendi haki kama panapokuwa na *improvement* tukanyamaza.

Ukenda Hospitali ya Mnazi Mmoja ukilinganisha na hali ilivyokuwa yapo mabadiliko. Lakini nilikuwa naomba yapo baadhi ya maeneo Mhe. Spika, Mhe. Waziri bado ayatizame. Bado kuna tatizo kwamba hospitali yetu ukienda tofauti na hospitali nyengine kubwa katika nchi mbali mbali ukienda hakuna utaratibu unaoeleweka. Hili mwaka jana nililichangia Mhe. Spika, na mwaka huu ninalichangia tena.

Bado ule utaratibu wa kueleweka hasa kwamba unafika wapi, unapokelewa wapi mgonjwa, akifika mgonjwa anapokelewa wapi, akitaka kwenda katika huduma ya X-ray, unaweza ukenda katika huduma ya X-ray mara sita, hili nililizungumza sana mwaka jana. Nilikuwa hili Mhe. Waziri alitazame bado kuna tatizo kubwa la utaratibu usioeleweka.

Mhe. Spika, pana *some sorts of chaos* katika utaratibu mzima wa kumpokea mpaka kumfikisha mgonjwa wodini kama inabidi kulazwa au kama kutoka ikiwa ni *out patient*.

Mhe. Spika, mwaka jana tulipongeza sana utaratibu kwamba kuna watu walisema kuna *file system* katika Hospitali ya Mnazi Mmoja. Tunadhani hii ni muhimu kuweka *record*, mgonjwa ni vizuri kuwekwa *record* zake anapokwenda kutibiwa akajulikana historia yake ya maradhi ya hapo nyuma.

Imefanyika lakini naomba iendelee kupewa uzito lakini kubwa Mhe. Spika, ni la uchafu. Bado hospitali yetu katika hali ya usafi hairidhishi. Inawezekana ninasema ninawapa *benefit of doubt* kutokana na bajeti ndogo, lakini bajeti ya mwaka huu nimegundua hapa ongezeko zuri tu, pameongezeka imefikia kupatiwa mwaka huu thamanini na tisa nukta tano milioni katika bajeti ya usafi kwenye hospitali ya Mnazi Mmoja peke yake.

Sasa Mhe. Spika, ninataka fedha hii tuione ikajiakisi katika ile hali ya usafi pale hospitali. Mhe. Spika, haipendezi ukenda katika hospitali ya Mnazi Mmoja unakuta pale pameandikwa weka mazingira katika hali ya usafi, kile kibango cheneyewe kichafu kinachoeleza hayo weka mazingira katika hali ya usafi kimetanda mabuibui na kila aina ya vumbi na uchafu. (*Makofi*).

Sasa Mhe. Spika, vitu hivi ni vidogo vidogo lakini vinaonesha taswira na pale ni jamii nzima. Kuna vifaa chakavu kila kona ukenda vitanda vibovu, vigari vibovu vya kubebea wagonjwa Mhe. Spika, haipendezi. Ukenda kwenye hospitali za wenzetu tunaona, hata usiende mbali, ukenda hapo Hospitali ya Muhimbili tu Dar Es Salaam hailingani na hali yetu. Kwa hivyo ninasema hebu pawekwe *system* au utaratibu ambao unaoeleweka.

Mhe. Spika, kasema Mhe. Waziri kwamba tuna tatizo la msongamano la jamaa wa wagonjwa. Ni kweli lakini mwenyewe kajibu katika hotuba yake kwa sababu hakuna wauguzi unatakiwa mwenyewe uhudumie. Lakini kama kungekuwa na pahala pa kupumzikia hawa wangekuwa na utaratibu maalum, lakini hawana pahala pa kupumzikia wote wanakusanyika katika *corridors* zile wanasubiri maelezo ya daktari au wauguzi wengi waliopo pale.

Kwa hivyo nilikuwa ninadhani hili watusaidie wao kwanza, la kuwajengea jamaa wanaokwenda pale kutizama wagonjwa kuweza kukaa, kama nilivyosema kama haipendezi wamejaa katika *corridors* kila njia ya mlango pamejaa watu, matokeo yake huduma inakuwa inazidiwa sana.

Lakini jengine Mhe. Spika, alitazame sana ilisemwa hapa bado kuna tatizo la wafanyakazi wasiokuwa waaminifu katika hospitali zetu. Alisema Mheshimiwa mmoja na mimi ninataka kuliongezea hapa Mhe. Spika. Dawa tunaambiwa zinapatikana na mwaka huu tunashukuru, na mwaka jana nilisema kwamba haipendezi serikali kwamba inategemea mia saba milioni halafu imesema imetoa serikali, mwaka huu naona bajeti imepanda ni bilioni moja nukta nne sita serikali yenyewe itatoa.

Jambo la kupongezwa na kufurahisha. Pahala pa kupongeza Mhe. Spika, siku zote tunapongeza sisi, hatuwezi tukasema kwamba tupo hapa kuja kutoa lawama. Lakini ninasema kama dawa zinanunuliwa labda tutolewe matangazo tujue, ili hawa wanaotumia utaratibu huu kujifichia kwa sababu unakwenda pale unaambiwa dawa hapana, lakini ukiitaka unaambiwa ulete pesa ukenda ukatafutiwa ukapewa, huu utaratibu unawaumiza wananchi wetu hasa wananchi maskini Mhe. Spika.

Mhe. Spika, katika eneo jengine ambalo ninasema tulitizame katika Hospitali ya Mnazi Mmoja ni katika eneo la *maternity*. Nilikuwa ninapewa kesi moja na mmoja katika mpiga kura wangu, ananiambia kwamba kenda mke wake kujifungua pale, *maternity* moja katika mradi wake ni kugawa vyandarua, lakini *maternity* yenyewe hakuna vyandarua. Mzazi mwenyewe na mtoto anayezaliwa ni mthani mtupu. Sasa ninasema haya pia Mhe. Waziri labda akitembelea atayaona.

Lakini Mhe. Spika, katika hotuba yake ya mwaka jana na hili ninafikiri litakuwa la kufungia kwa hospitali ya Mnazi Mmoja, alitwambia kwamba anataka kuanzisha utaratibu *quality assesement tool*, kwamba wananchi wenyewe wanahojiwa juu ya ule utaratibu wa utoaji wa huduma ili wizara ipate *feed back* ya wale wanaopewa huduma.

Na hili ingekuwa uzuri zaidi kuliko maneno yetu sisi pengine wale wana siasa wanasema tu, lakini hatukuona katika ripoti katika hotuba yake yote kwamba jee utaratibu ule ulianza kazi, na kama ulianza kazi mwaka jana kama alivyotwambia kwenye hotuba yake mwaka jana, umepata mafanikio gani au umepata matatizo gani. Ninadhani atwambie Mhe. Waziri.

Mhe. Spika, niondoke katika hospitali ya Mnazi Mmoja. Sasa ni je katika suala la pili la wafanyakazi wanaohitajika katika hospitali ya Mnazi Mmoja na nyengine. Mhe. Spika, katwambia Mhe. Waziri wana upungufu mkubwa wa wafanyakazi wanaohitajika, na akatwambia wameomba kuajiri watumishi 502. Lakini pia kwenye hotuba yake katwambia kwamba ukilinganisha na idadi ya wanaostaafu na wanaoajiriwa hakuna uwiano. Wamestaafishwa watu 85 lakini wameruhusiwa kuajiri watu 39. Kwa hivyo hakuna uwiano, nilikuwa naomba hili kwa Ofisi ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, katika pahala pa kuwapa kipaumbele ni kulikabili hili na kuwaruhusu Wizara ya Afya kupata hawa wafanyakazi wanaotaka ili tukabili huu upungufu wa wafanyakazi, ninafikiri hata ile *chaos* nyengine inayokuwepo katika hospitali itapungua ikiwa watapatiwa wafanyakazi ambao wamewaomba.

Lakini na mimi niungane na Mhe. Jaku Hashim Ayoub Mhe. Spika, kasema bado ukiangalia kiambatanisho nambari 10, na idadi ya watumishi wanaotakikana pale inatupa mashaka kwamba jee katika Hospitali ya Rufaa kweli wale wanasheleza? Kwa hivyo akija Mhe. Waziri atosheleze nimefanyika kitaalamu lile katika kukisia waliopo pale.

Mhe. Spika, niende katika eneo jengine ni katika Kitengo cha Lishe. Nimeshtushwa na aliyotwambia Mhe. Waziri kwamba wamegundua kuna chumvi inayotengenezwa ambayo haina *iodine*, yaani madini joto. Hii inatia mashaka Mhe. Spika, kwa sababu inawezekana hili pengine likawa ndio sababu ya maradhi mengi ambayo yanaongezeka. Kuna maradhi watu wengi hapa wanauliza hapa Mhe. Spika, mbona hapo zamani yalikuwa hayasikilikani. Kama kensa hizi, maradhi mengine ya ajabu ajabu pengine vitu kama hivyo kwa sababu watu wa zamani walikuwa makini walikuwa hawapelekei kupata maradhi kama haya. Nilikuwa Mhe. Waziri pia akija na hili atusaidie atachukua hatua gani ili kulikabili.

Mhe. Spika, halafu naomba pia Mhe. Waziri anisaidie maelezo. Nilipokuwa nikimsikiliza kwa makini katika hotuba yake na kama ulivyotwambia tulikuwa tukisikiliza kwa makini kweli kweli, likilinganisha takwimu za wagonjwa waliopewa huduma katika hospitali za Unguja na Pemba, zile kubwa za Wilaya, za vijiji, nimegundua na uwiano wa watu waliokuwa wakifariki kulinganisha na watu waliohudumiwa, basi kwa Pemba kuna wastani wa asilimia 2 mpaka 3, lakini kwa Unguja hata katika hospitali za *cottages* kama Makunduchi na Kivunge kuna wastani wa asilimia 1.

Sasa nilikuwa ninajiuliza. Ninadhani yeye kwa uchunguzi wake ni nini kwamba Pemba kuna upungufu zaidi ya vifaa, kuna upungufu zaidi wa madaktari, kuna upungufu zaidi ya huduma au kuna kitu gani kinachosababisha uwiano ukawa unatofautiana.

Mhe. Spika, sasa niende kidogo vile vile katika suala la *Public health*. Mhe. Omar kazungumzia kuhusu kitengo cha elimu ya afya. Mimi ninataka kwenda katika *public health*. Mimi ninadhani maradhi mengi haya tutaweza kuyakabili ikiwa tutaviimarisha vitu kama hivi vya kinga.

Mhe. Spika, tukiangalia hali ya maeneo kwa mfano masoko ambapo *public health* inapaswa kuwa ndio *concern number one*. Bado hali ya masoko yetu ni machafu. Tumezoea kuona samaki wanaburuzwa katika maeneo watu wanatema makohoo humo humo, uchafu barabarani, watu wanaochukua nyama zile, utakuta mtu kichwa wazi kabeba nyama anakwenda kukuuzia nyama hiyo hiyo.

Kwa ufupi Mhe. Spika, hata mavazi wanayovaa, utaratibu wa *public health* tumerudi nyuma, ukaguzi inasikitisha kwamba kwa mwaka ripoti imekagua vyanzo vya maji vinane tu. Mhe. Spika, inaonekana bado katika *public health* hatupo vizuri. Nilikuwa naomba atwambie Mhe. Waziri atachukua hatua gani ili kuimarisha *public health* kwa kupunguza vyanzo vya maradhi.

Mhe. Spika, la mwisho kabisa kwa leo ninataka kulizungumzia ni fungu linalohusu matibabu nje ya Zanzibar. Mhe. Spika, bajeti ya mwaka huu imeombewa mia tatu thalathini na tano milioni katika eneo hili, na kwa mujibu wa hotuba ya Mhe. Waziri kasema hata hizo pengine hazitoshi. Lakini ni *improvement* kubwa mwaka jana kulikuwa na milioni kumi na moja laki moja sitini elfu.

Sasa Mhe. Spika, mimi sizungumzii habari ya fungu lakini ninazungumzia kwamba wananchi wanalalamika sana juu ya huduma wanazopata hasa wanaopelekwa. Kwanza kuipata hiyo nafasi mbinde, lakini hata ukishapata yapo malalamiko ambayo ninamuomba Mhe. Waziri na watendaji wake wayafanyie kazi, watwambie tatizo lipo wapi.

Kwanza kuna suala la wagonjwa wengine kupelekwa bila ya kuruhusiwa mtu wa kufuatana naye Mhe. Spika. Matokeo yake akifika kule wanatekelezwa hawahudumiwi ipasavyo.

Lakini jengine kuna wagonjwa wamepelekwa lakini hawatibiwi kwa sababu fedha zilizo dhinishwa ni kidogo, hivyo inakuwa hazisaidii chochote unafika pale unamuongezea gharama tu, na hapa nilitaka kumtaja mgonjwa mmoja *specifically* Mhe. Spika.

Kuna mgonjwa anaitwa Ali Hamad yupo mwezi wa pili katika hospitali inayopelekwa wagonjwa, lakini hajafanyiwa operesheni kwa sababu fedha zilizoingiziwa hazitoshi. Kwa hivyo matokeo yake anaendelea kukaa kule, anaongeza gharama lakini huduma hapati.

Mhe. Spika, kuna wagonjwa wanadhaliwa mpaka kufika kuhamishiwa vyumba kwa sababu kaja raia wa nchi nyengine, kwa mfano wa nchi za Arabuni wenye fedha zaidi wanahamishwa wao. Sasa jee wizara haisimamii vizuri utaratibu huu.

Mhe. Spika, kuna kukosekana kiungo baina ya wagonjwa na madaktari, lugha hawafahamiani. Tunawapeleka watu wengine hawana msaidizi, lugha taabu wanaishia kukaa pale hawapati huduma. Lakini vile vile wagonjwa wanapodai, mimi umenipeleka kwa mfano Mhe. Spika, umeniidhinisha kwamba nitatumia dola elfu tano au sita, zile zimeidhinishwa na serikali yangu mimi, nina haki mimi ya kuomba *break down* ya matumizi yale, wakifika kule wakisema *break down* hawapewi wanaambiwa yanapelekwa moja kwa moja katika wizara inayohusika. Lakini mimi ndiye ninayeweza nikathibitisha kwamba hii pesa niliyoambiwa nimezitumia, nimezitumia kweli kwa utaratibu uliowekwa, hakuna kupewa wagonjwa Mhe. Spika.

Sasa mimi ninadhani Mhe. Spika, kuna *concern* kubwa wanayosema watu kwamba hii inaweza inakuja kwa sababu hospitali yenyewe imebadilika, hiyo tunayopeleka huko tunayofunga nayo mkataba, kwamba imeshughulikia zaidi kufanya biashara kuliko kutibu, kwamba watu wengi wanatoa labda wizara imefika pahala ione haja ya kuangalia hospitali nyengine kwa kufanya makubaliano kuliko hii hospitali ya zamani, ambayo inaonekana imejikita zaidi katika kufanya biashara, haya matatizo yamejaa kwa sababu hawa nani, hawa Wazanzibari fedha yenyewe ndio hivyo hivyo ya mashaka mashaka akija mwingine anapewa *priority*.

Kwa hivyo nilikuwa ninadhani wizara itazame vizuri inaweza ikapata hospitali ambayo itakayoweza kuwahudumia watu vizuri. Lakini pia watizame hata katika watendaji wa Wizara ya Afya wenyewe, hakuna mchezo mchafu hapo katika mambo haya. Isije ikawa tunaishabikia hospitali ile kwa sababu kuna mambo yetu na sisi tunayapata humu ndani. Kwa hivyo nilikuwa ninasema hilo Mhe. Waziri alitazame kwa kina aje atusaidie.

Mhe. Spika, kama nilivyosema hayo ninamuongezea katika changamoto ili kusaidia kuboresha au kuzifanya huduma ziwe bora zaidi katika wizara yake na huduma wanazotoa kwa wananchi. Lakini ninampongeza tena kwa utendaji wake kwa *improvement* ambayo tunaiona, tunakutakia kila la kheri na nikipata maelezo haya Mhe. Spika, ya hoja ambazo nimezitoa nitaiunga mkono hoja hii mia kwa mia. Ninakushukuru sana Mhe. Spika, ahsante sana.

Mhe Mahmoud Muhammed Mussa: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi ya kuweza kuchangia mawili matatu katika bajeti hii ya Wizara ya Afya.

Kwa kusema kweli Mhe. Spika, waliokwisha tangulia wamekwishaelezea baadhi ya mambo ambayo tayari nimeya-*note*. Lakini naona kwamba haina haja ya kurudiarudia. Lakini kusema kweli wizara hii imejitahidi sana na imefanya mabadiliko kwa namna Fulani, na kuna mambo ambayo yanaonesha juhudi za maendeleo kutokana na uhalisia ambao tulikuwa nao katika kipindi kilichopita.

Mhe. Spika, mimi nikianza naomba ninukuu kitabu chetu cha Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, mapitio ya hali ya uchumi na utekelezaji wa mpango wa maendeleo 2011/2012.

Mhe. Spika, tunaanza katika sekta ya afya. Tunasema kwamba sekta hii ina majukumu ya kutoa huduma ya afya, na kuzingatia sera ya afya ya mwaka 2000 na kufanya kazi pamoja na wadau mbali mbali katika ngazi zote.

Sekta ya afya inatekeleza dira ya 2020, kwa kuhakikisha kuwa jamii inapata huduma bora za afya ifikapo mwaka 2020. Mhe. Spika, pamoja na malengo haya ya serikali mwaka jana nilipokuwa ninachangia katika wizara hii, kuna mambo nilipendekeza.

Mhe. Spika, naomba kukariri baadhi ya mambo ambayo nilikuwa nimependekeza. Mhe. Spika, ndani ya Zanzibar yetu kwa sasa tuna matatizo ya maradhi haya ya aina tofauti ambayo yapo hapa, ikiwa ni pamoja na maradhi ya BP, moyo, mabusha na mambo mengine.

Mwaka jana nilipokuwa ninachangia katika bajeti hii nilimuomba Mhe. Waziri wafanye utaratibu wa kiutafiti, ili tuweze kuona katika mwaka huu wa fedha unaokuja serikali imejipanga namna gani kuhakikisha kwamba tunaelekea kuweza kuondosha maradhi ambayo yanawakabili watu ni nguvu kazi ya taifa letu katika miaka yetu ya mbele.

Lakini nimejaribu kusoma hiki kitabu na kusikiliza baadhi ya maelekezo ambayo Mhe. Waziri alikuwa akiyatoa, sikupata maelekezo kuhusiana na suala hilo. Sasa namuomba hapa Mhe. Waziri atakapokuja atusaidie kidogo kutupa mwelekeo wa wale mambo ambayo nimeyaomba kuhusiana na tafiti, pamoja na mikakati ya serikali juu ya maradhi haya ambayo kwa sasa yamekuwa yameenea sana kwa watu wetu.

Mhe. Spika, jambo jengine ambalo nilikuwa nimeligusia mwaka jana ambako kwa mwaka huu kidogo kuna afuweni kidogo, kwa sababu kuna nusu kwa nusu katika mgawano wa mahesabu. Mwaka jana katika suala la vifo vya akinamama na watoto, tulikuwa katika kila kina mama 422 ilikuwa kunatokea vifo 287. Lakini mwaka huu baada ya kuangalia humu katika vitabu nimekuta kwamba katika kila kinamama 1,000 basi kuna vifo 284, ukipiga mahesabu utakuta kwamba vile vifo vimepungua kwa nusu ya asilimia ya vifo ambavyo vilikuwa viko katika miaka ya nyumba iliyokuwa imepita.

Kwa hivyo, ningewaomba Wizara ya Afya wajitahidi zaidi ili kuhakikisha kwamba hawa watu wanawasaidia zaidi, ili tuweze kuondokana kabisa na tatizo la vifo katika maeneo yetu.

Mhe. Spika, eneo jengine ambalo nilikuwa nataka kulizungumzia ni hali ambayo inajitokeza katika hospitali vile vile. Bado ningemuomba Mhe. Waziri ajitahidi katika masuala ya usafi katika hospitali yetu ya Mnazi Mmoja. Hilo moja.

Lakini la pili ni suala la madaktari wale ambao wanatakiwa wawepo pale hospitali, tujitahidi sana Mhe. Waziri ili tuhakikishe kwamba wagonjwa wanaofikishwa hospitali, sio kwamba yule ambaye amefika na mgonjwa pale aweze kutafuta nauli ya kutoa kwa ajili ya kwenda kufuatwa daktari nyumbani kwake. Daktari ambaye amelazwa pale kwa ajili ya kuwasaidia wananchi. Mhe. Spika, tungemuomba Mhe. Waziri daktari yule abakie pale, ajitume pale na lolote litakalotokezea pale ili aweze kukabili nalo baada ya kurudi nyumbani kwenda kusubiri hatua nyengine.

Jengine Mhe. Spika, ningependa vile vile kuchukua nafasi hii kumshukuru Mhe. Rais kutokana na utaratibu wake na mpango wake mzima wa kuondoa ada zile za akina mama katika masuala ya uzazi. Lakini pamoja na yote hayo Mhe. Spika, ningependa kutoa wito maalum kwa madaktari, kuondoshwa kwa ada ile ya shilingi 40,000 pale hospitali kwa wazazi ambao watakuwa wanakwenda kujifungulia watoto wao, isiwe sababu ya manyanyaso pamoja na lugha chafu kwa wagonjwa au kwa wale watu ambao wanawapeleka wagonjwa katika hospitali ya Mnazi Mmoja.

Baada ya maelezo hayo Mhe. Spika, kwa sababu wachangiaji tuko wengi. Mimi ningependa kukomea hapa, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kikwajuni kwa ujumla wao naunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia, ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Ali Salum Haji: Mhe. Spika, na mimi nianze kwa kukushukuru kwa kupata fursa hii kuchangia jioni hii ya leo na nichangie kwa ufupi sana, kwa sababu mengi ambayo nimepanga kuchangia wenzangu wameshagusia sana tu na haina haja ya kurudia hayo kwa hayo.

Mhe. kwanza nianze kumshukuru Mhe. Babu Duni, Waziri wa Afya kwa jitihada ambazo amezionesha katika kuleta mabadiliko kwenye hospitali ya Mnazi Mmoja. Pongezi zaidi nimepelekee Mhe. Naibu Waziri, ni imani yangu kwamba uzoefu wake wa udaktari ndio umepelekea kupata mabadiliko ya haraka katika hospitali yetu ya Mnazi Mmoja na hospitali zetu nyengine.

Mhe. Spika, nilikuwa nataka nizungumzie katika suala la hospitali yetu ya Mnazi Mmoja, hususan katika kitengo cha watu wa ajali. Wengi wamezungumza Mhe. Spika, kwamba bado, pamoja jitihada ambazo zimeletwa katika hospitali yetu, lakini bado matatizo madogo madogo katika hospitali yetu yapo. Tunashuhudia matatizo ambayo yanajitokeza.

Mimi mwenyewe Mhe. Spika, nimeshashuhudia tatizo moja kubwa na la kusikitisha sana. Kuna siku nilifika pale saa moja za usiku, kulikuwa na kijana amepata ajali wakati anatoka mpirani, kwa bahati mbaya amekatika kiganja cha mkono, lakini ndio yale ambayo tunazungumza. Cha kusikitisha kabisa, tangu ameletwa wakati wa saa moja, tulikwenda mbio kufanya jitihada za kumtafuta daktari, angalau kuweza kunusuru maisha ya mtu yule, madamu mengi yalikuwa yanamvuja. Lakini mafanikio yake yalichukua muda mkubwa sana, lakini kwa sababu Mwenyezi Mungu alikuwa bado anamtaka kiumbe yule bado aishi, basi matibabu yalianza kufanyika saa sita za usiku, hii ni hali ya kusikitisha.

Mhe. Spika, tatizo kubwa ambalo lilitusumbua ni kuhangaika kutafuta simu za madaktari. Unapiga simu unaambiwa haipatikani, tumetoka na magari kwenda kumfuatia daktari unafika kwake unaambiwa hapa hayuko. Sasa mimi nahisi nimuombe daktari kwamba jitihada ambazo ameanza kuzionesha basi ni kutafuta mbinu ambazo zitarahisisha kwa wananchi ambao wanapata maafa, hususan ya ajali kwa sababu suala la ajali ni suala ambalo hujalitegemea. Kwa hivyo, imani yangu ni kwamba kutokana na nilivyozungumza, Mhe. Babu Duni pamoja na Mhe. Naibu Waziri, uzoefu wao utasaidia kuweza kulirekebisha hili tatizo hilo ili kuondosha usumbufu kwa wananchi wetu.

Mhe. Spika, baada ya hilo nilikuwa nataka nizungumze suala ambalo lilishazungumzwa, lakini nataka nilisisitize zaidi tu, kwa sababu suala hili nimeshawahi kulizungumza katika masuala yangu ya kawaida na nikawahi kupatiwa majibu, lakini hadi leo bado ufanisi wa suala hili haujapatikana. Suala la msongamano kwa watu ambao wanasubiri kwenda kutizama wagonjwa na nilitoa mfano mpaka kwenye ngazi watu wamekaa, hivyo wanapata tabu watu kupita kwenda juu kutokana na watu kusubiri zamu ya kwenda kuwaangaliwa watu wao.

Mhe. Spika, sio suala hili la msongamano tu, lakini pia linaleta usumbufu kwa wale watu ambao wanasubiri muda wa kwenda kutazama wagonjwa wao. Usumbufu wenyewe unatokezea pale hali ya hewa inapokuwa sio nzuri. Mfano, inapotokezea mvua basi watu wanatandika majamvi pale chini kwenye maeneo ya kuegesha magari, basi inakuwa ni tatizo wanakuwa hawana pahala pa kukimbilia.

Kwa hivyo, niliwahi kuuliza swali hili nikaambiwa kwamba jitihada zipo na muelekeo ulikuwepo wa kujenga eneo jengine mbele kule ya hospitali yetu ya Mnazi Mmoja kwenye *garden*, na nikaelezea sana suala hili kwamba eneo ambalo wazee wetu au viongozi wetu waliopita waliweka eneo maalum, lakini eneo lile sasa hivi limefanywa mabadiliko na zimewekwa baadhi ya ofisi. Sasa namuomba Mhe. Waziri anieleze basi zile jitihada zimefikia wapi na lini hali ile itaondoka. Kwa sababu kama nilivyo sema mwanzo Mhe. Spika, kwamba jitihada zinaonekana kwa sababu hata mkahawa tayari, watu ambao wanakwenda kuwaangalia wagonjwa wakitoka, wameshawekewa huduma pale hivyo mabadiliko yapo. Kwa hivyo, niombe tu nalo hili litapata ufumbuzi kwa muda gani.

Mhe. Spika, naomba niende katika kitabu kwenye ukurasa wa 63, katika suala la bodi ya chakula, dawa na vipodozi. Mhe. Spika, mara nyingi tunapofika hapa tunapiga makelele kuwa huduma sio nzuri, hali sio nzuri, madawa kupatikana tabu. Lakini kuna kitu ambacho tunakuwa tunakisahau sisi kama binadamu, kwamba haya maradhi yanasababishwa na vitu. Kwa hivyo, niwapongeze sana waliokaa na kuwaza na kuunda sheria nambari 2 ya mwaka 2006, kuweka ubora na usalama wa chakula, dawa na vipodozi, kwa sababu kinachotuathiri ni vile vyakula ambavyo tunakula na wenzetu kwa sababu ya tamaa zao wanatulisha vyakula ambavyo havistahiki, ndivyo ambavyo vinaleta usumbufu kwa wananchi na kuleta maradhi.

Mhe. Spika, kubwa katika mchango wangu nimekuja kutoa pongezi za dhati kwa Mkurugenzi wa Bodi, ndugu yangu Dk. Burhan. Kama kuna watu mahiri kama Dk. Burhan basi ni imani yangu kwamba nchi hii maendeleo yake yatapatikana kwa haraka sana. Mkurugenzi huyu Mhe. Spika, hana muhali, haoni tabu pale ambapo sheria inataka ifuatwe. Hakuna suala gumu Mhe. Spika, kama kushughulika na wafanyabiashara. Mtu ambaye ameleta mali zake zaidi ya milioni, lakini leo unamuambia azirejeshe au unachukua hatua ya kuziangamiza, ushawishi unakuwa ni mkubwa. Lakini kijana huyu amekuwa mahiri kwa kutii sheria zilizowekwa. Naomba nimpongeze kwa dhati sana. Nampongeza kwa sababu tayari kwa wale ambao hawana uaminifu wameonekana.

Mhe. Spika, hivi karibuni tumesikia katika vyombo vya habari kwamba kuna maafisa ambao waliamua kuondosha mchele bandarini na mchele ule ukazagaa madukani, lakini kwa jitihada za Mkurugenzi, huko huko madukani amefuatilia na amebaini na waliamua ule mchele kuurejesha na kuutokomeza. Kwa hivyo, pongezi hizi na wale wengine katika vitengo vyao waige mifano ya watu hawa. Mhe. Spika, mimi huyu namwita Magufuli wa Zanzibar katika kutii sheria.

Mhe. Spika, baada ya hilo kwa sababu kama nilivyosema mwanzo kwamba michango mingi wenzangu wamezungumza na nishukuru kwa dhiti sana kwamba jitihada zinaonekana. Nilikuwa nataka kuingia kwenye masuala ya vifungu, lakini na mimi katika kuangalia, nashukuru zile jitihada na makelele yetu kwamba mabadiliko kidogo kwa Wizara ya Afya yamepatikana kwa nguvu sana.

Vile vile nashukuru kama Mhe. Jussa alivyozungumza hapa alielezea katika kifungu 1501 hospitali ya Mnazi Mmoja, kwenye kifungu kidogo 220506 vifaa vya usafishaji. Hapa kidogo fungu limeongezeka, tulianza kushtuka, lakini hatukushtuka zaidi baada ya kuona ile hali halisi ya Mnazi Mmoja, uchafu ulivyokithiri na tayari kwamba hapa fungu kidogo limenona. Kwa hivyo, na mimi niombe kwamba kilichonona kitumiwe kwa hali halisi iliyokusudiwa, ili kuleta mazingira mazuri katika hospitali yetu ya Mnazi Mmoja.

Mhe. Spika, kwa kumalizia tu nilikuwa naomba nipate ufafanuzi katika kifungu 0701 idara ya tiba. Mhe. Spika, hapa kidogo nilikuwa napata kigugumizi, kwa sababu katika fungu dogo 220905 chakula cha wagonjwa kimepanda, laini sio sana na mimi sina wasi wasi kwa sababu wagonjwa wanastahiki kupata vyakula vilivyokuwa bora. Lakini hofu yangu na ufafanuzi ninaouhitaji, kwamba kwa upande wa Unguja kwa mwaka huu zimetengwa milioni 24,848,000. lakini kwa upande wa Pemba zimetengwa milioni 69,600,000. Sasa nilikuwa najiuliza kwamba Pemba kuna wagonjwa wengi zaidi kuliko Unguja, haya ndio mashaka yangu na nitamuomba Waziri atakapokuja anisaidie ufafanuzi. Fungu kubwa 0701, fungu dogo 220905.

Baada ya hayo Mhe. Spika, kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Kwahani, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja, ahsante sana.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Ahsante Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii kwa mara nyengine, baada ya kuikosa pale mwanzo. Mhe. Spika, nilipeleka mapema na pale mchana ulinitaja kuwa nitakuwa miongoni mwa wachangiaji wa mwanzo sana. Lakini kwa bahati mbaya nilipata dharura nikalazimika kuondoka kidogo. Kwa hivyo, nimerejea nashukuru angalau umenihurumia.

Mhe. Spika, mimi nataka nianze na ukurasa wa 107 kwenye hiki kitabu cha Mhe. Waziri. Kwa kweli katika ukurasa huu kuna takwimu, anasema mwenyewe kiambatisho nambari 10, hali halisi na mahitaji ya wafanyakazi katika hospitali ya Mnazi Mmoja. Mhe. Spika, sura hii inaonesha hapa inatisha sana, kwa sababu mahitaji ya wafanyakazi wa hospitali ile ya Mnazi Mmoja ni watu 712, lakini waliopo ni watu 349. Kwa maana hiyo waliokuwa hawapo ni 363, hii ni karibu asilimia hamsini na ngapi sijui, mimi sio mtu wa hesabu, lakini kwa kweli uwezo wetu ni chini ya asilimia 50 ya kuweza kupata. Hii ni hospitali ya Mnazi Mmoja tu na ni hospitali ambayo kwa kweli kuna kila sababu ya kupewa kipaumbele. Ni hospitali yetu ya rufaa, na ni hospitali ambayo iko kitovuni kwa mji lakini ina mapungufu haya, maana yake nini. Maana yake ni kwamba na hospitali nyengine zitakuwa na mapungufu makubwa zaidi kuliko haya.

Kwa hivyo, tunaweza tuka-*conclude* kwamba uwezo wetu wa kuweza kutoa huduma ya afya sasa, maana huduma ni hawa watumishi pamoja na madawa, lakini ni watumishi. Sasa ikiwa tuko chini ya nusu maana yake sasa ni sawa sawa na kusema kwamba Serikali sasa inashindwa kubeba hii dhima kubwa ya kutoa huduma ya afya, ndio maana yake. Mimi nataka nimshukuru sana Waziri kwa hili hakulibania, kaliona ni changamoto na kalisema wazi wazi, huu ndio uwazi ambao tunaouhitaji na huu ni uungwana mkubwa.

Sasa Mhe. Spika, mimi nilikuwa najiuliza na nilikuwa naomba sana Mhe. Waziri afanyekazi kidogo na anipatie jawabu ya maswali haya ambayo yanakuja. Je, tunahitaji wafanyakazi wangapi nchi nzima wa afya na tulionao ni wangapi. Maana tunahitaji wangapi na tulionao ni wangapi.

Lakini je, kila daktari mmoja anatakiwa awahudumie wagonjwa wangapi kwa siku. Maana wanasema wataalamu tukiwa na takwimu ndio tunaweza tukajipangia malengo yetu vizuri, tunaweza tukajijuwa tukowapi na tunahitaji

kwenda wapi na mapungufu yetu ni yapi. Kwa hivyo, namuomba sana Mhe. Waziri haya maswali ayachukuwe na aje atujibu ili Wazanzibari waone mapungufu tuliyonayo katika nchi yetu.

Lakini niliowanishe hili na pale alipokuwa akitaja changamoto Mhe. Waziri, sijui iko ukurasa wa ngapi nimesahau kidogo. Katika changamoto zake moja akasema ni upungufu wa wataalamu. Pia kwa uungwana wake mkubwa akakiri kwamba moja katika masuala yanayosababisha tuwe na upungufu wa wataalamu, na huo upungufu unatokana na yale maslahi duni ya wafanyakazi.

Hili Mhe. Waziri kalikiri mwenyewe katika ukura wa 91 ukiangalia pale utaona, huu ni uungwana mwingine. Mimi siku zote huwa namsifu sana Mhe. Babu Juma Duni kwa sababu habanii maradhi, maana ukificha maradhi hutapata tiba, lakini yeye yuko wazi kueleza hili ni tatizo. Pia nawashukuru kwa mikakati yao waliyoipanga kwa kushirikiana na Waziri wa Nchi Ofisi ya Ris Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kujaribu kuangalia upya maslahi ya wafanyakazi. Mhe. Spika, tunapoteza nguvu kazi nyingi kutokana na malalamiko haya ya maslahi duni.

Mhe. Spika, nilikwenda Dar es Salaam mara moja na mtoto wangu alikuwa anatatizo la moyo, nilifika kwenye *dispensary* moja ya Dk. Alokhatar nafikiri ndiye mtaalamu wa moyo kule Tanzania Bara. Sasa yule karani wake tu, alimtizama yule mtoto kabla hajamuweka kwenye kompyuta, alitumia vipimo hivi vya kawaida tu, akaniambia mtoto huyu ana tatizo kweli, lakini tatizo hili lilikuwa hata halihitaji kuja huku Bara ni tatizo ambalo linaweza kujitatu lenyewe. Hajamuweka kwenye kompyuta wala hajamfanya chochote. Sasa ile semasema yangu akaipata yule kijana, akaniuliza wewe ni Mpemba, nikamwambia ndio mimi ni Mpemba. Akaniambia basi na mimi ni mwenzako mimi ni Mpemba wa Ziwani.

Sasa Mhe. Spika, ukanijia uchoyo kidogo, huyu hospitali za huku kwetu nimehangaika naye mpaka Mnazi Mmoja. Sikusudii kuwadharau madaktari wetu, lakini mpaka Mnazi Mmoja wakaniambia kesi ya mtoto wako ni lazima uendenaye India, lakini kwanza nenda Muhimbili. Sasa nimefika pale karani tu, wala sio daktari mwenyewe akanipa ufumbuzi na nilipofika kwa daktari na yeye vile vile akamuweka kwenye kompyuta, akaniambia hili tatizo hata kidonge mimi sikupi rudinaye mtoto wako hana tatizo.

Mhe. Spika, mimi nilikuwa nasema yule angekuwepo hapa angetusaidia. Lakini kwa nini akaondoka, kwa sababu ya maslahi duni. Kwa hivyo, ndio nikasema namshukuru sana Babu Juma kwa kuiona hii changamoto. Lakini pia namshukuru tena kwa kuandaa mikakati ya kuangalia maslahi ya madaktari. Mhe. Spika, kama kuna jambo la kupewa kipaumbele basi ni kuangalia maslahi ya madaktari ni sekta moja muhimu sana. Tusisubiri mpaka likaja kutokea balaa Mwenyezi Mungu atupishe mbali. Lakini wenzetu kule Bara wana balaa sasa. Kwa hivyo, sisi ni vyema tukachukua hatua mapema, pamoja na unyonge wetu, lakini masuala haya tuwe tunayaangalia.

Mhe. Spika, nilikuwa na wazo ikiwe uwezo wetu wa kutoa huduma hii ya kijamii tuko chini ya asilimia 50 ya mahitaji yetu, basi nilikuwa nadhani tuangalie upya sera zetu na mikakati yetu. Mhe. Spika, katika sekta mbili, sekta ya elimu na sekta ya afya kumejitokeza wawekezaji binafsi wengi ambao wana nia ya kueleza na wanajitahidi kueleza katika sekta mbili hizi. Sekta binafsi ikifanya kazi vizuri, basi itasaidia sana kuipunguzia serikali mzigo wa huduma hizi. Kwa hivyo, lilinjia wazo nikaona kwa nini serikali haitowi kipaumbele maalum tena maalum kwa mkakati kabisa ili kuziwezesha sekta binafsi iweze kufanyakazi vizuri, ili iweze kuisaidia serikali mzigo huu wa kutoa huduma ambao ni mzito na serikali katika kitabu hiki maana yake ni kwamba serikali inakiri kwamba sasa inakaribia kushindwa ndio maana yake.

Kwa hivyo Mhe. Spika, wapo watu binafsi ambao wamefungua *dispensary* zao, wanatoa huduma. Lakini huduma zao ni ghali kwa sababu ya mambo ya kodi na leseni na kwa sababu wao ni wafanyabiashara ni lazima huduma zao ziwe zinawaletea tija. Mimi nilikuwa naona serikali iandae utaratibu wa kuwapunguzia hizi kodi ili waweze kufanyakazi vizuri na wananchi wetu waone kwamba wakienda pia kwenye hospitali binafsi wanaweza kuhudumiwa kwa unafuu na kwa malipo madogo. Tukifanya hivyo tutakuwa tumeisaidia sana serikali mzigo huu wa kubeba hili jukumu ambalo hatuliwezi tena. Hilo ni wazo ambalo nimelitoa, tuangalie kwenye sera na kwengineko lakini tuweze kusaidia hii hali ambayo kwa kweli ni hali ngumu sana.

Mhe. Spika, jambo jengine ambalo ni dukuduku kwangu mimi, nilisema niliseme na uzoefu nilionao kwamba tukisema jambo mara nyingi hapa katika Baraza, basi hatimaye serikali huliona lina maana na wakalifanyia kazi. Mfano mzuri ni juzi tu Mhe. Rais katoa agizo kwamba akina mama wanaohitaji kujifungua kwa upasuaji, badala ya

kutozwa shilingi 40,000, sasa wafanyiwe bure. Hii ni matija ya yale makelele yetu ambayo tunaiambia serikali kwa kupitia Baraza hili.

Sasa hivi kuna changamoto nyengine Mhe. Spika, na hii wala haina gharama kubwa, nafikiri ni Mhe. Waziri na watendaji wake wakajipanga tu. Mhe. Spika, kuna tatizo la madaktari wa kiume kuwahudumia wagonjwa wa kike, lakini na madaktari wa kike kuwahudumia wagonjwa wakiume. Hili jambo linaudhi wala sio jambo ambalo linakwenda na itikadi na silka zetu Mhe. Spika. Mimi sifurahi hata siku moja Mhe. Spika, kumuona daktari wa kiume akimzalisha mjamzito, au akimfanyia upasuaji mjamzito, sio jambo linaloridhisha hata kidogo.

Mhe. Spika, pia kinyume chake ni hayo mambo yote yanatokea. Hivi karibuni nilimpeleka mgonjwa hospitali ana tatizo la tabaali. Mhe. Spika, jambo la kusikitisha, mmi nina hakika madaktari wa kiume wapo wa kutoa huduma ile, lakini aliyemuhudumia alikuwa ni kadaktari wa kike. Mgonjwa wa kiume aliyemuhudumia tena kumtia mpira ni daktari wa kike, inasikitisha Mhe. Spika, sio jambo zuri hata kidogo.

Kwa hivyo, nilikuwa namuomba sana Mhe. Waziri wa Afya, suala hili halihitaji gharama kubwa, maana yake *magyner* tunao wanaweza kuwahudumia wanawake wenzao na madaktari wa kiume tunao wanaweza wakawahudumia wanaume wenzao. Kwa nini tusifanye hivyo na tunafanya vyenginevyo. Silka zetu hazikubali.

Jambo jengine Mhe. Spika, hili nilitaka nimkumbushe Mhe. Waziri wa Afya. Kuna vijana walisoma hapa Chuo cha Afya Mbweni. Kozi yao nafikiri ilikuwa inachukua karibu miaka minne, kozi za afya mara nyingi hazina muda mfupi. Walipokuwa wakisoma waliambiwa kwamba wanasoma diploma, lakini bahati mbaya sana walipomaliza hawakutambuliwa kama wao ni diploma, na mpaka leo mazungumzo yanaendelea ama wapewe vyeti vya diploma au wasipewe. Kwa bahati mbaya sana sasa wengine wana nia ya kujiendeleza, lakini wanakwama kwa sababu hawajui hasa *level* yao ya elimu ni ipi. Je, mtu aombe kama yeye kamaliza cheti au aombe kama yeye kamaliza diploma na hata maslahi yao yatakuwa na tofauti. Kuna wenzao waliokwenda kozi kwa mwaka mmoja na wao, lakini wao walipelekwa Dar es Salaam wakasoma kozi ile ile na muda ule ule wao wenzao wana vyeti vyao vya diploma.

Sasa Mhe. Waziri wananung'unika hawa vijana, hivyo nilidhani ni vizuri uongozi wa Wizara ya Afya ukae na kuangalia namna ya kuwapa vyeti vyao, ili wawafungulie milango wakitaka kujiendeleza wenyewe basi wajiendeleze.

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, una dakika tatu

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Mhe. Spika, nimemaliza na nakushukuru sana na naunga mkono hii bajeti, ahsante. (*Makofi*).

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Nakushukuru Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Afya Babu Duni. Mhe. Spika, kwanza nimshukuru sana Mhe. Waziri wa Afya, pamoja na watendaji wake na wafanyakazi wote wa wizara hii kwa kazi nzuri wanayoifanya kwa taifa letu. Maana Mhe. Spika, kazi hii ni kazi ya kujitolea, kazi hii kama kazi ya ualimu, yaani ujitolee ndio ufanye. Kazi hii sio ya kutegemea tija ni kujitolea zaidi.

Mhe. Spika, mimi nianze mchango wangu kwenye ukurasa wa 27 wa kwenye kitabu cha Mhe. Waziri wa Afya, ukurasa wa 26 kuingia 27 hospitali za vijiji. Niende kwenye Hospitali ya Kivunge. Mhe. Spika, kwanza nimpongeze sana Mhe. Waziri wa Afya kwa jitihada zake akishirikiana na watendaji wake kwa kutimiza ile ahadi yake ya kuweza kuweka uzio katika hospitali hii, nimshukuru sana Mhe. Waziri aliahidi hilo kuwa atahakikisha kwamba analifanya na kweli amelifanya, ingawa hajamaliza kidogo, lakini yuko mbioni kumaliza na nina hakika imani yangu inaniambia kwamba bila shaka ndani ya wiki moja au mbili zijazo itakuwa tayari amekamilisha. Kwa hivyo, nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa hilo. (*Makofi*)

Lakini pamoja na mazuri hayo, nimuombe Mhe. Waziri angalie zaidi juu ya huduma zinazotolewa katika hospitali ile. Kwa kweli Mhe. Spika, huduma zinazotolewa pale hazijawa za kuridhisha katika nyanja zote. Kwa mfano, tukija kwenye upande wa hawa watoa huduma, yaani daktari nafikiri labda kama tunae ni moja kwenye hospitali ile.

Kwa hivyo, namuomba sana Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, tena nilimwambia kwenye bajeti yake ya mwaka jana na aliniahidi kwamba kuna madaktari watatoka na watakapotoka, basi katika hospitali ambazo zitapata nyongeza ya madaktari ni Hospitali hii ya Kivunge, nadhani mpaka hivi sasa ile nyongeza bado haijafika kwetu. Kwa maana hiyo, namuomba sana Mhe. Waziri akatuongezea wataalamu hawa.

Mhe. Spika, kwa kweli hospitali ile ni tofauti vile inavyoitwa ni *Cottage Hospital* ya kijiji, mimi naita ya Mkoa kabisa na wala sio ya kijiji. Kwa mfano, ukiangalia takwimu kwenye kitabu chake hapa Mhe. Waziri, nafikiri ndio hospitali iliyoongoza kutoa huduma kwa watu wengi, yaani imehudumia watu wengi zaidi, karibu watu elfu 20 na tofauti na hizi hospitali nyengine. Kwa hiyo, namuomba sana Mhe. Waziri aweze kuiangalia vizuri zaidi tofauti kidogo na wale wenzetu wengine.

Sambamba na hilo kuna suala la mgao wa dawa. Mgao wa dawa unaopata hospitali ile ni kama *hospital* nyengine za *cottage*, sasa ukiangalia takwimu zake za huduma inazotoa, pale inatoa huduma kwa watu wengi zaidi, hivyo na mgao wa dawa ukiwa ni kama ule, ndipo pale inapokuta zililetwa leo sinakaa siku moja na siku ya pili zimekwisha na wananchi walalamika kwamba dawa hakuna.

Sasa tunapomwambia Mhe. Waziri dawa hakuna, anasema ata! Nimeuliza watu wangu na wamesema zimepelekwa jana, kweli jana zimepelekwa, lakini kutokana na wingi wa watu wanaopewa huduma pole haziwezi kukaa kama hivyo. Kwa hivyo, namuomba sana Mhe. Waziri aangalie sana suala hili kuhusu huduma pamoja na upatikanaji wa dawa.

Vile vile Mhe. Spika, nitoe pongezi zangu sana kwa Mhe. Rais kwa kuweza sasa kutoa huduma za akinamama bure. Kwa kweli suala hili lilikuwa tatizo kubwa sana kule kwetu. Kwa mfano, akinamama wetu wanapokwenda kujifungua pale wanahitajiwa watoe mchango wao na mama zetu wale ni masikini sana na mchango ule ulikuwa ukiwashinda na hata ukimwambia kanunue hiyo *gloves*, ambazo ni shilingi 1,500/= basi pia kwake yeye inawezekana ikawa ngumu. (*Makofi*)

Lakini tatizo lile ni sugu Mhe. Spika, kwa sababu mtoto akiwa tayari anataka kutoka huna vya kumzuia lazima mama yule ajifungue tu. Kwa hivyo, natee pongezi kubwa sana kwa Mhe. Rais kwa kutoa ahadi kwamba sasa akinamama wale watapata huduma zile bure, tena namuomba sana Mhe. Waziri kupita kwako Mhe. Spika, hili alisimamie. (*Makofi*)

Mhe. Spika, nilizungumza wakati nilipokuwa nikitoa mchango katika ile Hotuba ya Bajeti Kuu ya Serikali. Sasa narejea tena kwa Mhe. Waziri wa Afya, kwamba inawezekana hilo tayari limeshaagizwa lakini ule utekelezaji ukawa sugu kidogo na hapo ndipo kwenye shughuli.

Kwa hiyo, namuomba sana Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, akae na watendaji wake juu ya jambo hili, kwa sababu wazee wetu wameshaambiwa kwamba ni bure, lakini inawezekana ikawa ni bure ghali, mtu ameshafika pale na kuambiwa aaa! Sisi tulipokea *gloves* tano tu hapa na tayari nimeshawazitumia kwa watu watano na zimeshakwisha kanunueni na yakawa ndiyo yale yale, kwamba anarudi tena na kuambia akanunue na ametoka huko hana kitu na wala hatofanya kitu.

Mhe. Spika, namuomba sana Mhe. Waziri, tuangalie hata ule wingi wenyewe wa wale mama wanavyojifungua, basi na vile vifaa vyenyewe viende kwa wakati na viwepo. Kwa kweli mtu hapigi simu kama kesho nakuja kujifungua na wale yeye mwenyewe hajui inawezekana, isipokuwa anajua ni karibu na linapotokeza ndipo anapokimbilia pale.

Mhe. Spika, hospitali yetu Mhe. Waziri yeye mwenyewe ni mwenyeji wa kule anajua, kwamba haihudumii tu watu wa eneo la pale, isipokuwa wanatoka sehemu mbali mbali, ndipo pale niliposema hospitali ile ni kama ya mkoa kwa wingi wa watu ambao wanapata huduma pale.

Nikiendelea na mchango wangu sasa niende kwenye ukurasa wa 32 kuhusu suala la matibabu ya nje. Mhe. Spika, na mimi nataka Mhe. Waziri atakapokuja kufanya majumuisho aje atusaidie kidogo kuhusu namna ya utaratibu mzima unaotumika juu ya wagonjwa wanaosafirishwa.

Tumekuwa tunapata malalamiko sana kwa wananchi wetu, wanafika pahala na kuambiwa maradhi yako hayatibiki hapa unatakiwa kusafirishwa, lakini hizo *process* za kupita mpaka akapata huo usafiri haujulikani wapi pakuanzia,

kwani mtu akienda sehemu moja anaambiwa aende sehemu nyengine na wala hakuna utaratibu mzuri uliowekwa juu ya suala hili.

Kwa hiyo, namuomba Mhe. Waziri wakati atakapokuja kufanya majumuisho atueleze hasa na wananchi wetu wasikie, kwamba utakapoambiwa wewe unatakiwa usafirishwe nje, basi ukienda sehemu fulani labda kuna watu wa watatu na unakaa foleni au peke yako unakwenda haraka zaidi, hivyo ni vyema aje atupe muongozo hasa unaotakiwa ufuatwe mpaka watu hawa wakasafirishwa. Mhe. Spika, hali hii inatambulikana na imeshakuwa maarufu, kama huna mwenyeji au kitu kidogo husafiri kwenda. (*Makofi*)

Sasa namuomba sana Mhe. Waziri aje atusafishie juu ya hili, je hizi tuhuma ni kweli na kama si kweli basi atueleze huo utaratibu mzuri ambao umepangwa hasa. Kwa mfano, mtu akitoka kule Uyagu moja kwa moja akeshakuambiwa wewe unatakiwa uende nje sasa, aende wapi na afanye vipi mpaka apate hiyo safari yenyewe.

Vile vile kuna jengine kwenye safari hizi hasa kwa *Nurses* wetu wanaosafirisha hawa watoto wanaokwenda nao kule kuna tatizo Mhe. Spika hapa, kutokulipwa zile stahiki zao za safari, aidha watakopeshwa waambiwe subirini na wanaporudi wanagaiwa shilingi 500,000/= na shilini 200,000/= subiri kwanza hatuna kitu. (*Makofi*)

Lakini mimi nashangaa Mhe. Waziri au Katibu Mkuu akisafiri kibindoni anazichukua kabisa. Sasa kwa nini hawa wa kada ya chini mnakuwa mnawakopa, nadhani ni vyema Mhe. Waziri wakati atakapokuja aje atueleze kidogo suala hili linatokana na nini, kama Mhe. Waziri wewe au Katibu Mkuu wako mnakopwa basi itakuwa ni mambo mazuri na tuone kama mnakopwa nyote ama wanakopwa hawa wadogo tu. (*Makofi*)

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, ili Mhe. Waziri asiye kukujiibu hapo hapo, basi hayo maneno yalete huku na halafu yaende pale. (*Makofi*)

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Mhe. Spika, ahsante sana. (*Kicheko/Makofi*)

Sasa niinge kwenye ukurasa wa 33 kuhusu Mpango wa Damu Salama. Mhe. Spika, kulikuwa na malalamiko kwenye kitengo hichi juu ya mambo mbali mbali hasa masuala ya mafao haya, namna ya ulipwaji wao, nafikiri Mhe. Waziri aliwahi kuja kutujibu hapa kidogo, lakini bado lile tatizo linaonekana halijamaliza vizuri.

Kwa hiyo, naomba nitumie fursa hii Mhe. Waziri atakapokuja aje atusaidie juu ya suala hili la migogoro ya malipo kwa wale wafanyakazi wa Kitengo cha Damu Salama limeishia wapi?

Sasa naomba nizungumzie kuhusu Hospitali ya Mnazi Mmoja. Mhe. Spika, Hospitali ya Mnazi Mmoja sisi wanyonje ndio kimbilio letu na sehemu ambayo unaweza kuona oohwe unaweza kumfukuza Izrail kidogo akasubiri muda, ndipo pahala petu. Kwa kweli inasikitisha huduma bado ziko chini sana Mhe. Spika, mimi napata mshangao na tatizo sijui nini.

Jambo la kushangaza zaidi Mhe. Spika ni kwamba wafanyakazi wale waofanyakazi pale, ukiwakuta huku *private* ni tofauti kabisa na wanavyokuwa pale. Sasa sijui zile nguo wanazovaa mule zinakuwa kidogo zinakasirisha na kule zinafurahisha. Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri atusaidie kidogo, kwa sababu daktari au mhudumu yule ukimkuta pale na sehemu nyengine ni tofauti, nadani kuna tatizo.

Mhe. Waziri namuomba sana kupitia kwako Mhe. Spika, tatizo hasa ni nini watu wetu wanapata matatizo wanapokwenda pale kwani huduma zinakuwa dhaifu. Kwa mfano, tumeshawahi kwenda na mgonjwa wakati wa saa 4 za usiku unamkuta mtu tayari ameshajikunjulia shuka na wewe unakwenda na mgonjwa, anasema aaa! Mimi niacheni kwanza au anaumwa na nini huyo, anahoma, basi lete hilo buku, yumo ndani ya shuka anaandika dawa mule na hata kujifunua hajifunui ukamuona sura, anaandika dawa na haya buku hilo katafuteni dawa huko, unakwenda zako.

Kwa kweli kitendo hichi si kizuri na hasa katika kada hii, maana kada hii ni ya huruma na nilisema mwanzo kwamba kada hii ni ya kujitolea zaidi na wala si kada ya faida. (*Makofi*)

Lakini katika hospitali ya Mnazi Mmoja kuna matatizo kidogo. Mhe. Spika, kuna wafanyakazi ambao hawajabadilishiwa au wahajapata stahiki zao kuhusu yale mabadiliko ya pamoja katika Serikali kuu. Kwa mfano,

kwenye mwezi wa Oktoba hawakupata zile stahiki, mwezi uliofuata wakapata na miezi ilioendelea na ule waliambiwa watapewa na mpaka hii leo bado hawajapata. Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri atakapokuja aje atusaidie majibu ya tatizo hili.

Vile vile kuna suala jengine ambalo Mhe. Mohammed Said Mohammed nadhani alilizungumza kuhusu kitanda cha *Martinet*. Mhe. Spika, kweli kitanda kibovu wanachozalishia madaktari wetu na wameshalalamika sana.

Kwa hivyo, tunakuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, awatafutie kitanda chengine pale *maternity*, madaktari wetu waweze kufanya kazi ile inayostahiki, maana daktari akiwa mrefu kidogo inabidi ainame sana na hali kama hiyo hawezi kufanyakazi vizuri. Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri aliangalie vizuri suala hili. (*Makofi*)

Lakini ile *scheme of service* ya mshahara kwa kada ya udaktari inaonekana pia haijakaa vizuri. Mhe. Spika, nadhani Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Utumishi wa Umma na Utawala Bora na Mhe. Waziri wa Afya kwa pamoja watasaidiana katika kulitolea maelekezo.

Kwa kweli *doctor* au *nurse* wote kule kwetu kijijini tunawaita madaktari tu kwa kuwa wanafanyakazi mule, lakini wenyewe mna majina yenu, kama vile mnamjua huyu ni *doctor* na yule *nurse*, hebu hizi *scheme of service* za mishahara zikae wazi, ili waweze kuzijua wenyewe. Kwa mfano, mtu mwenye *diploma* anaweza kupata mshahara mkubwa kuliko mwenye *degree*. Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri atusaidie hili na waliweke sawa, ili likae vizuri.

Mhe. Spika, pia tuliwahi kuuliza katika swali la msingi kuhusu madaktari ambao wanatukimbia, ni sababu zipi wanatukimbia hawa. Madaktari wetu tunawasomesha kwa gharama kubwa kabisa, ambao ni watoto wetu au ndugu zetu ama vijana wetu na baadaye wanarudi hapa na kufanyakazi muda mchache sana hapa na wakesha wanaondoka.

Sasa namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika atueleze hasa hizi sababu za msingi, maana kwa haraka unaweza kuziona kwamba mafao hayako vizuri. Kwa hivyo, suala hili mnafanya vipi suala hili, ili liweze kukaa sawa na hawa vijana wetu tunaowasomesha kwa gharama zetu waje watutumikie hapa na hili ni tatizo.

Vile vile nataka kujua kwamba hawa madaktari wetu ni wangapi ambao wametukimbia hapa kwetu. Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri wakati atakapokuja nipate majibu hayo.

Nikiendelea na mchango wangu sasa niingie kwenye hili daktari la mahesabu kwenye mafungu ya Mhe. Waziri, yaani ametuletea hapa misahafu karibu miwili kwa mitatu na mimi sijui niusome upi, kwa sababu kila ninaoutizama hapa naona huu umekata kona huku na mwengine umekata kona kule na wala siupati vizuri.

Kwa hivyo, namuomba sana Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, atueleze tuusome upi, kwani haya mafungu mengi yamepisha, kama vile tukichukua kitabu kikubwa, tukichukua cha masahihisho ya kwanza na kile chengine cha masahihisho ya pili na haya ametupa kwa pamoja na wala siyaoni.

Sasa hapa kuna mafungu nitakuja kupiga buti Mhe. Spika, mpaka aje atusaidie ufafanuzi wale mzuri hasa kwenye masuala haya ya chakula cha hospitali. Kwa mfano, alizungumza Mhe. Ali Salum Haji hapa inaonekana lile la Pemba limenona zaidi kuliko la Unguja tena kwa mara tatu ah! Au alikosea Mhe. Waziri lile la Pemba lilikuwa likae Unguja na lile la Unguja ndio likae Pemba.

Lakini kuna mafungu pia kuhusu posho za vikao na mambo mengine hii! Yamenona mno. Kwa hiyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, wakati atakapokuja kufanya majumuisho atupate uchanganuzi zaidi kwamba hivi vikao vipi, kwa sababu idara hiyo moja hapa Unguja itaiona ina vikao milioni kadhaa, pia idara hiyo kwa upande wa Pemba utaona kuna vikao milioni kadhaa na hapa kidogo nimepata shaka.

Vile vile kuhusu fungu la safari za nje, maana mafungu yale ameyatafutisha kidogo Pemba na Unguja, mimi naona kama huku Makao Makuu ndiko wanakoondokea hawa maafisa wako wote, lakini na kule Pemba inaonekana kuna mafungu ya safari za nje. Kwa hivyo, kidogo naomba nipatiwe ufafanuzi.

Mhe. Spika, nikiondoka hapo nje kwenye makusanyo pia kuna matatizo sehemu hiyo. Kwa mfano, Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii alilizungumza hili, kwamba kuna utata

kwenye masuala ya makusanyo. Mhe. Waziri hapa ndio umeshatupa maombi yako ya makusanyo, sasa Mhe. Mwenyekiti wa kamati anasema kuwa kuanzia tokea mwaka jana kuna tatizo hilo na mwaka huu limeonekana tena hivyo.

Mhe. Spika, hapa Mhe. Waziri anatuambia nini katika hili makusanyo yetu yanaingia mfukoni zaidi na hayaji huku tunakoyataka, kuna tatizo gani yakawa haya makusanyo yanafichwa.

Lakini mimi kuna hesabu kidogo namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, atakapokuja kufanya majumuisho aje atusaidie kuhusu makusanyo katika kile kitengo cha *First Track*, atupe makusanyo yake kwa kipindi cha miaka mitatu, maana huko tulikutoka hayakuonekana, je anakusanya vipi na watu wanakwenda na kulipa ah! Kama tunalipa zinakwenda wapi, kwa sababu huku hazionekani na zinaingia kwenye fungu lipi?

Kwa hiyo, namuomba Mhe. Waziri aje atusaidie vizuri fungu ambalo anumia kutuwekea, kwani sisi hatukumpa idhini ya makusanyo katika kitengo kile, kwa sababu hukuyaleta na hivyo hakukuidhinishia, lakini tukienda kule tunalipa *First Track* pale, sasa fedha hizi zinakuwaje.

Mhe. Spika, naomba kupata ufafanuzi pamoja na hayo mafungu mengine, ili niweze kujiridhisha na kuweza kuipitisha bajeti yake Mhe. Waziri ikiwa haina tatizo, lakini kama sikupata maelezo ya kutosha katika hili na haya maswali ambayo nimeyauliza Mhe. Spika, basi nitakuwa mgumu sana kumridhia Mhe. Waziri bajeti yake hii.

Baada ya kusema hayo Mhe. Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi hii na kuangalia muda wako unanitikishia kichwa kwamba muda umekishwa. Nakushukuru Mhe. Spika na ahsate sana. (*Makofi*)

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, nakushukuru sana pamoja na Waheshimiwa Wajumbe wote. Sasa naakhirisha kikao hichi hadi kesho tarehe 11/07/2012 saa 3:00 za asubuhi.

(*Saa 1:45 usiku Baraza liliakhirishwa hadi tarehe 11/07/2012 saa 3:00 za asubuhi*)